Nipashe
Alhamisi Oktoba 3, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580039
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Je, unajua pombe na cocaine inazaa kifo?
Mabinti maelfu kufunzwa mbinu kukabili ngono zembe, Ukimwi
Wataalamu wa wizara wafukua yaliyojificha maziwa ya mama
Mradi Sayansi Udongo Bagamoyo unavyokaribisha mageuzi kilimo

UKURASA 13



## Wataka udhibiti wa pombe za kienyeji kuepusha vifo vya watu

UKURASA 3

# Washtakiwa zaidi wajipeleka kwa DPP



• **Wamo** kigogo PCCB, Wambura wa TFF, Tibaijuka aamua kuachia 'pesa ya mboga'... *Endelea ukurasa 2*


James Rugemarila


Kulthum Mansoor


Michael Wambura

## Kimbunga chapindua mtumbwi hifadhini

UKURASA 3



## Risiti EFD, rushwa ngono vyaitoa jasho Takukuru

UKURASA 2

MICHEZO YANGA KUISHUSHIA POLISI HASIRA ZOTE UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

# Machinjio Vingunguti, Kisutu kuchunguzwa

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema inafuatilia miradi mbalimbali ukiwamo mradi wa ujenzi wa machinjio ya Vingunguti na soko la Kisutu, jijini Dar es Salaam na mpaka sasa wamebaini mapungufu.

Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Ilala, Christopher Myava, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa katika ufuatiliaji wa miradi hiyo wamebaini thamani inayoonekana kwenye miradi hailingani na fedha iliyotolewa. "Tutafuatilia mradi wa ujenzi wa soko la machinjio la Vingunguti wenye thamani ya Sh. bilioni 12, kama mnavyofahamu mradi ule unafuatiliwa kwa karibu sana na sisi Takukuru tumekuwa tukifuatilia ili kuhakikisha hakuna uvujaji wa fedha za umma," alisema.

Myava alisema wataendelea kufanya ukaguzi ujenzi wa Soko la Kisutu kwa sababu ni miongoni mwa miradi ya kimkakati ambayo inaendelea.

Pia alisema katika kipindi cha miezi mitatu kilichoanzia Julai, mwaka huu wamekagua miradi yenye thamani ya Sh. milioni 200.6 inayoendelea Mkoa wa Ilala.

"Kupitia ukaguzi huu tunajiridhisha iwapo kuna thamani ya fedha katika utekelezaji wa miradi ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za serikali zinazotolewa ili kuitekeleza, tumegundua thamani inayoonekana kwenye miradi hailingani na thamani ya fedha iliyotolewa.

"Mara nyingi thamani ya miradi huwa chini, huku fedha iliyotolewa zikiwa nyingi na zinaonekana zimetumika zote, tunapokutana na kitu kama hiki au mapungufu hayo tunachunguza kwa kina na wahusika waliohusika kuhujumu miradi ya ujenzi wa miradi ya maendeleo huchukuliwa hatua."

Alisema lengo la kufuatilia miradi ya maendeleo ni kuangalia thamani ya fedha za umma kwenye ujenzi wa miradi hiyo ili kuthibiti uvujaji wa fedha.

"Katika kipindi hiki tumefanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo miwili, mradi wa umaliziaji wa kisima cha maji Kata ya Majoe na usambazaji wa maji, tumefuatilia fedha za ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa elimu bila malipo Mkoa wa Ilala," alisema.

Alisema katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, wamejipanga kufanya warsha ya kujadili soko la samaki la Feri na mianya ya rushwa katika ununuzi wa umma.

"Tulifanya ufuatiliaji wa mapato katika soko la Feri na tumebaini kuna mapungufu wakati hatua nyingine zikiendelea kuchukuliwa, tumepanga kufanya warsha zilizolenga kutatua changamoto hii," alisema.

Pia alisema wamejipanga kufanya ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi wa jengo la utawala na maabara katika Shule ya Sekondari ya Juhudi ambapo itagharimu Sh. milioni 150.

# Washtakiwa zaidi wajipeleka kwa DPP

**Na Waandishi Wetu**

MKURUGENZI wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathimini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor na Makamu wa Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, wamemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kukiri makosa yao ili wapate msamaha.

Mansour na Wambura wanakabiliwa na kesi tofauti za uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha fedha.

Wakili Elia Mwingira, anayemtetea Mansour alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kevini Mhina, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Mwingira alidai kuwa mteja wake ameandika barua kwa DPP kwa ajili ya kukiri kosa dhidi ya kesi yake.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo iliyepangwa jana kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hata hivyo, upande wa utetezi uliwasilisha hoja yao kwamba umemwandikia DPP barua ya kukiri na kwamba Jamhuri iharakishe kutoa majibu.

"Mheshimiwa ni vyema Jamhuri wakaharakisha tupate majibu ili mshtakiwa apate haki yake kwa wakati. Ni vyema tarehe ijayo itakayopangwa tukapata majibu kuhusu barua hiyo," alidai Wakili Mwingira.

Hakimu Mhina alisema kesi hiyo itatajwa Oktoba 16, mwaka huu, na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, Mansoor anakabiliwa na mashtaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477.

Inadaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2013 na Mei 2018, mshtakiwa alighushi barua ya ofa ya Agosti 13, 2003, kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo huku akijua kuwa si kweli.

Katika mashtaka ya pili, inadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017 katika maeneo ya Upanga, Ilala jijini Dar es Salaam, mshtakiwa kwa kudanganya alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika ambaye ni mfanyakazi wa Takukuru kama malipo ya kiwanja kilichoko Kijiji cha Ukuni, Bagamoyo.

INAENDELEA UK.26



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (wa tatu kulia), akipata maelezo kutoka kwa Katibu wa Kiwanda cha Nyuzi Tabora, Pascal Jotham (kulia), alipokagua viwanda mbalimbali mkoani Tabora jana. Waziri huyo, hakuridhishwa na utendaji wa kiwanda hicho na kuahidi kupitia mkataba wa ubinafsishaji wake. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Risiti EFD, rushwa ngono vyaitoa jasho Takukuru

**Na Salome Kitomari**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imeeleza jinsi ilivyo changamoto kukabiliana na rushwa ya ngono maeneo mbalimbali.

Akizungumza na wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Takukuru, John Mbungo, alisema rushwa ya ngono ni miongoni mwa makosa yanayopelekwa kwenye taasisi hiyo.

Rushwa ya ngono ipo katika makosa 24 ya rushwa ambayo alisema taasisi hiyo imeweka mkakati maalum wa kupambana nayo. Pia inafanyiwa kazi kama makosa mengine, na kwamba malalamiko yako mengi, lakini yanayowafikia na kufanya uchunguzi ni machache kutokana na aina ya makosa na tabia za kwenye jamii. "Kwa kutambua ugumu wa kutolea taarifa, Takukuru ilichukua mfumo wa kuweka mkakati wa kulishughulikia na Siku ya Mwanamke Duniani tulitangaza tuna dawati la kushughulikia malalamiko ya aina hiyo," alisema Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa, Sabina Seja.

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, alisema mwezi Oktoba hadi Desemba watafanya utafiti wa kuangalia rushwa ya ngono inavyotokea, visababishi na mbinu zinazotumika.

"Tunaanza na vyuo vikuu na baadaye tunakwenda kwa wadau wengine, baada ya hapo tutatoa hali halisi na kuangalia namna ya kushauri mamlaka na kuweka namna ya kusaidia wananchi na waathirika, kwa sababu tabia zinabadilika na ni lazima twende na namna zinavyobadilika," alisema.

Kwa mujibu wa Seja, wanatarajia kuboresha mitaala ya kuhusu masuala ya rushwa na wanajadiliana na mamlaka nyingine ili kuwa na mtaala kama huo ngazi ya vyuo vikuu.

"Tutafungua na kuimarisha klabu za wapinga rushwa shuleni ili wawe mabalozi wema wa kupambana na rushwa, tunajua tabia ikijengeka inachukua muda lakini tukianza na vijana watajifunza tabia mpya za kukataa na kuacha kujihusisha na rushwa," alibainisha.

Naye Mkurugenzi wa Intelijensia wa Takukuru, Emmanuel Kiyabo, alisema mbinu zinazotumika kwenye rushwa zimebadilikwa kwa kiasi kikubwa na mbinu mpya zinabuniwa.

"Kitendo cha rushwa ya ngono kinafanyika kwa siri na wananchi wengi hawaoni kama ni mtu kutoa taarifa, tunawaomba waje kwetu, wanafanyiwa vitu vingi, lakini hawasemi, wanaokuja kwetu hatujawahi kuwaangusha, maana tukiweka mtego tunawanasa," alisema.

Naye Mchunguzi Mkuu wa Takukuru, Kassim Ephrem, alisema rushwa ya ngono ni kosa, lakini mazingira ya kuripoti yanahitaji ujasiri.

"Idara ya uchunguzi tunawaomba wananchi watoe taarifa kwenye madawati yetu kwenye ofisi zetu, kuna watu maalum wa kuwasikiliza kwa umakini na kama hawatasaidiwa ni vizuri taarifa zikafika kwetu, tuna watu makini ili watoe ushauri, tuna mbinu mbalimbali za jambo hili katika kukusanya ushahidi," alisema.

# HABARI KITAIFA

## Kesi ukomo urais kusikilizwa Okt. 10

**Na Hellen Mwango**

KESI ya Kikatiba iliyofunguliwa na Dezydelius Mgoya maarufu kama Mkulima, kuhusu ukomo wa urais imepangwa kusikilizwa ambayo ni maombi ya Chama cha ACT -Wazalendo ya kujiunga na kesi hiyo Oktoba 10, mwaka huu.

Maombi hayo yalipangwa kusikilizwa jana, lakini kwa sababu Mkulima hakufika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imepigwa kalenda.

Maombi ya ACT-Wazalendo kujiunga na kesi hiyo yameshindwa kusikilizwa jana mbele ya Jaji Dk. Benhaj Masoud na Mahakama imekiagiza Chama ACT-Wazalendo kutangaza wito wa kumwita mahakamani kwenye magazeti mawili yanayosomwa na wengi.

Awali, ndani ya mahakama, Wakili wa ACT-Wazalendo, Jebra Kambole, alidai mbele ya Jaji Dk. Masoud kuwa mara ya mwisho walipokwenda mahakamani hapo walichukua wito wa kumuita Mgoya, lakini walishindwa kumfikia kwa sababu hawakujua anuani yake na mahali anapopatikana.

Wakili Kambole alidai kutokana na unyeti na uharaka wa jambo hilo, wanaweza kumtangazia wito huo kwenye gazeti ili naye aweze kwenda kusikiliza.

Baada ya kutolewa kwa hoja hiyo, Wakili wa Serikali, Daniel Nyakiha, aliiomba mahakama iwape muda wa siku saba ili kama wana hoja zozote za kupinga maombi ya ACT- Wazalendo waziwasilishe.

Jaji Masoud alitoa siku saba upande wa mlalamikiwa kama watakuwa wanapingamizi na maombi hayo wawasilishe majibu yao ndani ya siku hizo.

Pia alikubali Mkulima atangaziwe wito kwenye magazeti yanayosomwa zaidi ili Oktoba 10, mwaka huu, afike mahakamani hapo kuisikiliza kesi hiyo.

Kadhalika, Jaji Masoud alisema Mkulima huyo apewe nyaraka ili na yeye kama ana utetezi wowote autoe juu ya ACT- Wazalendo kujumuishwa kwenye maombi hayo.

Mgoya alifungua kesi hiyo chini ya kifungu cha 4 cha sheria ya utekelezaji haki na wajibu, sura ya 3 ya mwaka 1994 chini ya Ibara ya 30(3) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia Afya, Miundombinu na Uwekezaji, Josephat Kandege, akifungua mkutano wa wadau wa usafirishaji wa mabasi yaendeyo kasi, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kulia ni Mtendaji Mkuu wa mabasi yaendayo kasi, Ronald Lwakatare. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Serikali yaombwa udhibiti unywaji pombe za kienyeji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa udhibiti wa pombe za kienyeji ambazo hazina viwango vya vilevi, kutokana na uzalishaji wake kufanyika kiholela hasa maeneo ya vijijini.

Pia imependekezwa kupitia sheria na kuweka masharti kuhusiana na matangazo ya uhamasishaji, uzalishaji, uuzaji na udhamini wa pombe, kuonyesha onyo la athari za pombe kwenye vilevi ili kupunguza matumizi kwa jamii. Mapendekezo hayo yalitolewa jana na Mtandao wa wadau unaopambana na unywaji wa pombe kupita kiasi (TAAnet).

Akisoma tamko la maadhimisho ya Siku ya Kutokunywa Pombe Duniani, Mwenyekiti wa Tanzania Public Health Association (TPHA), Dk. Mashombo Mkamba, alisema endapo kutakuwa na sera ya udhibiti matumizi mbaya ya pombe, jamii hasa wanaume watawajibika zaidi na kuacha matumizi ya vileo yaliyopitiliza.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2016, zaidi ya watu milioni tatu duniani hufariki dunia kutokana na matumizi, ambapo zaidi ya robo tatu ya vifo hivyo ilikuwa wanaume.

Alisema matumizi ya pombe na athari zake ni tatizo linalozidi kukua nchini, ambapo linahitaji kudhibitiwa haraka iwezekanavyo ili kuzuia ongezeko la unywaji pombe katika jamii.

"Matumizi ya pombe kupita kiasi husababisha zaidi ya asilimia tano ya mzigo wa magonjwa duniani.

Hii ni kwa mujibu wa WHO katika ripoti yake ya hali ya dunia kuhusu unywaji pombe na afya 2018," alisema.

## Kimbunga chapindua mtumbwi hifadhini

**Na Waandishi Wetu**

MTALII raia wa Ujerumani, amenusurika kufa baada ya mtumbwi aliokuwa anautumia kwenye shughuli za utalii kuzama kutokana na upepo mkali.

Mtalii huyo na nahodha wa mtumbwi walizama kwenye Ziwa Momela lililopo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Arusha, huku nahodha akiendelea kutafutwa. Tukio hilo lilitokea jana, kutokana na kimbunga kukumba mtumbwi waliokuwa wanautumia kwa shughuli za utalii.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imethibitisha kuwapo kwa upepo mkali katika mikoa ya Kaskazini ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara juzi. Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema tukio hilo lilitokea ghafla mchana mtalii huyo alipokuwa anatalii kwenye Ziwa Momela.

Muro alisema juhudi za timu ya uokozi ya wilaya zimefanikisha kumwokoa mtalii huyo aliyefahamika kwa jina la RoseBever Heike.

Hata hivyo, alisema jitihada za kumtafuta aliyekuwa nahodha wa mtumbwi huo, Samuel Gelda Mhina, zinaendelea.

"Jitihada zinaendelea kumtafuta kijana aliyezama ambaye alikuwa akimwongoza mtalii huyo, ambaye alizama baada ya mtumbwi kupinduka.

"Tumejitahidi na tumeokoa maisha ya mtalii huyo, ila kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kutoka Arusha bado kinaendelea kumtafuta kijana aliyekuwa nahodha aliyezama na hadi sasa bado hajapatikana," alisema Muro.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Koka Moita, alisema tukio hilo lilitokea kwenye kijiji cha Olkung'wado,

Kitongoji cha Momeala Kata ya Ngarananyuki, Tafara ya King'ori wilayani Arumeru.

Alisema kilitokea kimbunga ghafla wakati Heike na Mhina wakitalii, na kusomba mtumbwi na kuuzamisha katika ziwa.

INAENDELEA UK. 26


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AccessBank Tanzania Limited** imetoa idhini kwa Madalali wake Kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara, Magari, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) kwa dhamana ya nyumba au kiwanja. Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada kwa siku husika iliyopangwa. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| No. | | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SANGA/J, FREDRICK | SANGA/J, FREDRICK | NYUMBA | ILEMI – MBEYA | 17 OKTOBA 2019 |
| 2. | MWANGASA/W,AGNESS | SINKALA/A,ZACHARIA | NYUMBA | KYELA | 17 OKTOBA 2019 |
| 3. | RENDSCO GOLD LIMITED | BARAKUBA/C,INOCENSIA<br>RENDIS/ABDULRAHIM,DADRAHIM<br>OMARY/GULAMRASULY,AHMED | MAGARI<br>- T139 BZD<br>-T 969 DJC<br>-T 122 DJB<br>- T 123 DJB | KAHAMA | 17 OKTOBA 2019 |
| | | | KIWANJA | PLOT NO. 1259, BLOCK "Q", NYASUBI AREA, KAHAMA URBAN AREA | 16 OKTOBA 2019 |
| | | | KIWANJA | PLOT NO. 5 BLOCK- Q NYASUBI AREA, KAHAMA URBAN AREA | 18 OKTOBA 2019 |
| | | | KIWANJA | PLOT NO. 499 BLOCK "L"CERTIFICATE OF TITLE NO. 2843- LR- TABORA,<br>- 22114 LR- MWANZA<br>-19283- LR MWANZA,<br>KAHAMA URBAN AREA | 17 OKTOBA 2019 |
| 4. | DEO & JITU PLASTICS | MWABUSILA/JOHN DEOGRATIUS | NYUMBA | RESIDENTIAL LICENSE NO. 040426<br>TEMEKE, MBAGALA KUU,MAGHARIBI | 17 OKTOBA 2019 |
| | | ARIFACKSARD AMANA MEENA | NYUMBA | RESIDENTIAL LINCENSE NO. 038268<br>LAND NO. TMK/MIB/KKM12/29<br>TEMEKE, KEKO MACHUNGWA, MIBURANI | 19 OKTOBA 2019 |
| 5. | BURHANI/SALUM,SALMA | MAJALIWA/ALLY. SHARIFA | NYUMBA | RESIDENTIAL LICENSE NO. 011437<br>LAND NO. TMK/MBGK.KJC7/47<br>TEMEKE, MBAGALA KUU, MTONI KIJICHI | 18 0KT0BA 2019 |
| 6. | MBARUKU/NEGAGA, NZOBORA | FIKIRINI/HASSANI,ZUBERI | NYUMBA | RESIDENTIAL LICENSE NO. 004201<br>LAND NO.KND/MBB/JTG4/336<br>KINONDONI,MABIBO,JITEGEMEE | 19 OKTOBA 2019 |
| 7. | MAFITA/H, HUSSEIN | VURIVA/JUMA, ELIHUDI | NYUMBA | TITLE NO. 100791<br>L.O. NO. 253394<br>PLOT NO. 782<br>BLOCK E<br>KINONDONI, BOKO AREA | 18 OKTOBA 2019 |
| 8. | KOI/M, JOHARI | KOI/M, JOHARI | NYUMBA | PURCHASE CONTRACT<br>KIVULE,ILALA | 17 OKTOBA 2019 |
| 9. | VISENT/JOHANES,MASERO | MSANGI/RAMADHANI, SHADA | NYUMBA | TITLE NO. 145678<br>L.O.NO. 629891<br>PLOT NO. 50<br>BLOCK H<br>TEMEKE, BUZA KIPERA | 18 0KTOBA 2019 |
| 10 | RY INVESTMENT (TZ) LIMITED | KUNAMBI/JOACHIM, VICTORIA | NYUMBA | RESIDENTIAL LICENSE NO. 0020<br>LAND NO. ILA/ILL/SSH18/84<br>ILALA, SHARIFFSHAMBA | 19 OKTOBA 2019 |
| 11 | KHAKI/GULAMABBAS, ABBAS | VINTANI/K, JOSEPH | NYUMBA | RESIDENTIAL LICENSE NO. KND 023326<br>KINONDONI | 18 OKTOBA 2019 |
| 12 | M. SAID TRANSPORTER CO. | MPANYU/MIKIDADI, SAIDI | NYUMBA | RESIDENTIAL LICENSE NO. 039786<br>LAND NO. TMK/MBGL/KBG15/267<br>TEMEKE, MBAGALA, KIBURUGWA | 19 OKTOBA 2019 |
| 13 | SHUMA/JOHN, PROSPER | SHUMA/JOHN, PROSPER | NYUMBA | TITLE NO. 132246<br>L.O. NO. 468591<br>PLOT NO. 330<br>BLOCK 24<br>TEMEKE, GEZAULOLE | 18 OKTOBA 2019 |

**MASHARTI YA MNADA**

Dhamana zitauzwa mahali zilipo

Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.

Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.

Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

KWA MAELEZO ZAIDI PIGA: +255 677 860 000

WOTE MNAKARIBISHWA.

215443302

## Sekta ya mifugo yapigiwa chapuo

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kuhakikisha inaboresha afya za mifugo na upatikanaji wa dawa kwa wakati ili wafugaji wanufaike na mifugo yao.

Akizungumza baada ya kukutana na Mkurugenzi wa Taasisi ya ZOETIS A.L.P.H.A katika Bara la Afrika, Dk. Gabriel Varga, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, aliwaomba wafugaji kushirikiana na wataalamu katika kutambua magonjwa ya mifugo yao na kupatiwa elimu ya namna ya kuhudumia mifugo yao.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejipanga vyema kutekeleza majukumu yake kwa vitendo ili kuhakikisha matokeo chanya yanapatikana katika sekta ya mifugo nchini.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, anayeshughulikia Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema wizara inatarajia katika kipindi cha miaka miwili au mitatu kufanya kazi na taasisi hiyo, sekta ya uvuvi.

Alisema taasisi hiyo ambayo katika Bara la Afrika inafanya kazi na taasisi ya Bill and Melinda Gates (BMGF), malengo yao yanafanana.

Dk. Tamatamah alisema ufugaji samaki kwa sasa nchini unawekewa kipaumbele katika kuendeleza na kuongeza uzalishaji wa samaki kutokana kuongezeka kwa mahitaji wa walaji.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo barani Afrika, Dk. Gabriel Varga, aliwaambia makatibu wakuu wa wizara hiyo kuwa taasisi yake inatarajia kuanzisha maabara hivi karibuni katika mikoa ya Iringa, Dar es Salaam, Mwanza na Morogoro ili kuboresha afya ya wanyama.

Pia taasisi hiyo ambayo inahudumia nchi zaidi ya 100 duniani, imekuwa ikiwasaidia wafugaji wa Afrika kwa kuwapatia elimu ya huduma ya wanyama kuwasaidia kufuga kwa tija.



Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohamed Ghalib Bilal, akiagana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Angela Kairuki, baada ya kuhudhuria ufunguzi wa Kongamano la Mafuta na Gesi Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni mwandaaji wa kongamano hilo, Abdulsamad Abdulrahman, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), Salum Shamte. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri Kairuki, Kalemani wapigia debe matumizi gesi

**Na Enock Charles**

WATANZANIA wameombwa kuwekeza na kutumia nishati inayotokana na mafuta na gesi ili kukuza uchumi wa viwanda na kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na matumizi makubwa ya mkaa na kuni.

Akizungumza katika kongamano la mafuta na gesi lililoshirikisha nchi 67 duniani, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela

Kairuki, alisema licha ya uwekezaji katika sekta hizo kuhitaji mitaji mikubwa, ni muhimu kwa wazawa kujitokeza katika kuwekeza katika sekta hiyo aliyoielezea kuwa na manufaa makubwa.

"Tunatambua namna ambavyo mtaji unaoingizwa katika sekta hii ni mkubwa sana kwa ule mradi wa LNG wa kuchimba na kuchakata gesi... mtaji waliotumia mpaka sasa ni zaidi ya dola bilioni 30 si fedha ndogo na kwa mujibu wa ugunduzi uliofanyika, mpaka sasa hivi tumeelezwa kuwa gesi ya Tanzania ni moja kati ya gesi bora duniani," alisema Kairuki.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji imeweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwa wenyeji na wageni ili kurahisisha uwekezaji katika sekta hiyo ikiwamo mpango wa serikali wa kuboresha sera ya uwekezaji kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Naye Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema Tanzania ina gesi ya kutosha kiasi cha futi za ujazo Sh. trilioni 57 ambayo bado haijatumika, hivyo kuhitaji wawekezaji kutoka sehemu mbalimbali duniani kuwekeza.

Alisema umefika wakati kwa Watanzania kuachana na matumizi ya mkaa na kuni ili kuepusha uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa kupindukia wa miti katika kutafuta nishati na kuongeza kuwa matumizi ya gesi ni nafuu hata kiuchumi kuliko kuni na mkaa.

"Kutumia gesi kuna unafuu mkubwa kwa takribani asilimia 40 ya matumizi mengine ya kuni na mkaa, lakini vilevile matumizi ya gesi yanasaidia sana kujenga viwanda ambapo Watanzania wengi watajiriwa," Dk. Kalemani alisema.

Akieleza kuhusu ukubwa wa matumizi ya mkaa kwa sasa alisema zaidi ya magunia 500,000 hutumika kila mwaka kwa Jiji la Dar es Salaam pekee kwa ajili ya nishati ya majumbani, hivyo kuongeza athari za uharibifu wa mazingira, na hivyo kushauri gesi na mafuta kutumika kama nishati mbadala.

# Mganga wa kienyeji adaiwa kubaka mtoto wa miaka 8

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MGANGA wa kienyeji mkazi wa Ujiji, Venas Edward (48), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Mkoa wa Kigoma kwa madai ya kumbaka mtoto msichana mwenye umri wa miaka minane.

Akimsomewa shtaka hilo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Katoki Mwakitalu, mshtakiwa huyo alikana kutenda kosa hilo na yuko nje kwa dhamana.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Raymond Kimbe, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba mahakama kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali Wakili wa Serikali Kimbe, alidai kuwa Aprili 23, mwaka huu majira ya asubuhi eneo la Kasoko-Ujiji, mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo mwenye umri wa miaka minane na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri. Kimbe alidai siku ya tukio mtoto huyo alichukuliwa na mama yake mzazi (jina linahifadhiwa) na kwenda naye kwa mshtakiwa ambaye ni mganga wa kienyeji kwa ajili ya kupata matibabu. Alidai baada ya kufika kwa mganga huyo mama wa mtoto aliambiwa aende kununua kiwembe dukani na kumuacha mtoto na mganga huyo, ambaye anadaiwa alitumia nafasi hiyo kumbaka mtoto huyo. Kufuatia tukio hilo ilidaiwa mshtakiwa huyo alikamatwa na askari polisi na baada ya mahojiano alipelekwa mahakamani. Wakili huyo alidai upande wa mashtaka unatarajia kupeleka mashahidi watano pamoja na kielelezo kimoja cha PF 3 na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi. Hakimu Mwakitalu alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 9 kwa kusikilizwa.

HABARI KITAIFA

## Ujenzi bwawa Nyerere wazingatia uhifadhi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amesema nia ya serikali kujenga bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere iko pale pale na ujenzi wake unaendelea kwa kasi huku ukizingatia masuala ya uhifadhi katika Pori la Akiba la Selous.

Akizungumza juzi na wabunge wa Kamati ya Bunge ya Mazingira, Uhifadhi wa Maliasili na Usalama wa Nyuklia kutoka Ujerumani, Kanyasu alisema tathmini ya athari za mazingira imefanyika na kuonyesha kuwa ujenzi huo ni salama katika shughuli za uhifadhi.

"Serikali inatekeleza mradi huu kwa kutumia fedha zake kutoka vyanzo vya ndani. Mradi huu utachukua eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 1,250 ambalo ni sawa na asilimia tatu tu ya eneo lote la Pori la Akiba Selous lenye ukubwa wa kilomita za mraba 50,000," Kanyasu alisisitiza.

Kanyasu alisema kiwango cha umeme cha megawati 2,100 kitakachozalishwa katika gridi ya taifa, kitasaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa misitu inayokatwa kwa kasi kwa ajili ya nishati ya mkaa na kuni.

Aidha, Kanyasu amewaeleza wabunge hao kuwa ujio wa bwawa hilo la umeme limesababisha sehemu ya Pori la Akiba la Selous kupandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa ya Julius Nyerere.

Kutokana na hali hiyo, alisema hali hiyo ulinzi wa wanyamapori katika hifadhi hiyo utakuwa madhubuti zaidi ya ilivyokuwa mwanzo.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliwaeleza wabunge hao kuwa imelichukua suala la mabadiliko ya tabia ya nchi kwa uzito unaostahili na kwa kutambua athari zake kwa mwaka huu, imependisha hadhi mapori ya akiba manne na kuwa hifadhi za taifa, hivyo ulinzi wa hifadhi hizo umeongezeka maradufu.

Kiongozi wa ujumbe wa wabunge hao, Sylvia Kotting- Uhl, aliipongeza serikali ya Tanzania kwa mageuzi makubwa yanayofanyika katika masuala ya uhifadhi na kuahidi ushirikiano na nchi yake katika kujenga uwezo kwenye nyanja za kusimamia na kudhibiti taka za kielektroniki, uzalishaji wa umeme wa jua na kutoa mwaliko kwa ujumbe wa Tanzania kutembelea Ujerumani.



Mkuu wa Kitengo cha Usalama cha Shirika la Posta Makao Makuu, George Mwamgabe (kushoto), akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, akikabiliwa na mashtaka mawili ikiwamo la kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin na bangi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ofisa Usalama Posta kortini madai kusafirisha mihadarati

**Na Hellen Mwango**

WATUMISHI wawili wa Shirika la Posta Tanzania akiwamo Ofisa Usalama, George Mwamgabe (44), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka mawili likiwamo la kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin na bangi.

Mbali na Mwamgabe, mshtakiwa mwingine ni dereva Abdulrahman Msimu (54) na wote wawili walisomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustina Mmbando.

Wakili wa Serikali, Aldolf Lema, alidai kuwa Agosti 25, mwaka jana, katika eneo la Benki ya Posta jijini Dar es Salaam, washtakiwa kwa pamoja walisafirisha dawa za kulevya aina ya bangi zenye uzito wa gramu 124.55.

Katika shtaka la pili, Wakili Lema alidai tarehe hiyo, katika eneo la Posta, washtakiwa wote kwa pamoja walisafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin yenye uzito wa gramu 1.55. Washtakiwa wote walikana mashtaka hayo na upande wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika. Hakimu Mmbando alisema washtakiwa watakuwa nje kwa dhamana kwa masharti ya kila mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili mmoja kutoka ofisi za umma watakaotia saini bondi ya Sh. milioni tano kila mmoja. Hata hivyo, washtakiwa hao walishindwa kutimiza masharti ya dhamana na kurudishwa rumande mpaka Oktoba 16, mwaka huu, kesi itakapotajwa.

## Wazazi wenye watoto mtindio wa ubongo waomba mfumo

**Na Elizabeth Zaya**

WAZAZI wenye watoto wa mtindio wa ubongo wameiomba serikali kuweka mfumo maalum utakaokuwa unatoa ushauri nasaha kwa kinamama wanaojifungua watoto wenye tatizo hilo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wazazi wenye watoto wenye tatizo hilo, walisema kukosekana kwa ushauri kwa kinamama wanaojifungua watoto hao kunawaweka katika hatari zaidi watoto hao kukosa haki zao ikiwamo kupelekwa shule kutokana na wazazi wengi kuwaficha ndani.

Walisema asilimia kubwa ya kinamama wanaojifungua watoto wa namna hiyo hawajui mbinu za kuwalea watoto hao kulingana na hali yao.

"Mimi nilijifungua mwanangu mwaka 2010, nilikuwa sijui kama ana tatizo la mtindio wa ubongo, mwanzoni nilikuwa namuona ni mtoto wa kawaida, lakini baada ya miezi mitatu nikawa simuelewi, alikuwa haliii na hata nilianza kubaini kwamba hakuwa wa kawaida," alisema Zainabu Balaji, mzazi wa mtoto mwenye mtindio wa ubongo na mkazi wa Mbagala Charambe.

"Shingo yake ilikuwa imelegea muda wote na hata baadhi ya viungo vyake vilikuwa vinaonekana havina nguvu, ilibidi nimpeleke hospitali."

Baada ya kumpeleka hospitali na kuonana na daktari, alisema mtoto wake alipatiwa vipimo na kuambiwa kwamba ana tatizo hilo la mtindio wa ubongo.

"Daktari aliniambia kwamba ananiandikia barua ili nimpeleke katika hospitali nyingine ambako ndiko anatakiwa akaanze kupatiwa matibabu na kufanyiwa mazoezi na wakati huo huo nilikuwa sielewi ni namna gani natakiwa kumlea mtoto mwenye tatizo hilo na nilijaribu kumwomba anielekeze, lakini aliniambia huko ninakompeleka ndiko wataniambia."




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Baada ya magogo tuangalie machinjio

**ITAKUMBUKWA** kuwa Septemba 30, 2019 ndiyo mwisho wa kutumia magogo kukata nyama kwenye mabucha.

Tunaipongeza serikali kwa kuliona hili na kuondoa utaratibu huo uliokuwa unawalisha watu nyama zilizojaa vibanzi vya mifupa na miti, harufu au shombo kutokana na gogo kutunza nyama zilizovunda kwa muda mrefu.

Gogo hilo lilikuwa halisafishiki wala kufanyiwa usafi wa aina yoyote kwa muda wote, hata kama kulikuwa na tatizo.

Tunashukuru kwani kero haipo na sasa ni wakati wa kutumia misumeno kukata nyama, kujenga maduka yenye milango ya vioo na wavu kuzuia inzi kujaa buchani pamoja na kuwa na friji kwa ajili ya kutunza kitoweo hicho.

Tunapongeza juhudi hizo na sasa tunategemea kuona mamlaka kama Bodi ya Nyama ikifuatilia na kufunga bucha ambazo hazina viwango ili kuhakikisha afya za walaji zinazingatiwa na kila mmoja analishwa chakula bora.

Pamoja na ufuatiliaji huo tungependa kuona kuwa mashine za kukatia nyama zinapatikana na kuuzwa kwa bei isiyowaumiza wafanyabiashara, kwani inavyoelekea wengi wanatumia misumeno mikuukuu au mitumba.

Lakini, pamoja na mafanikio hayo mijini, tunaiomba serikali itizame suala hilo na jinsi ambavyo linaweza kutekelezwa vijijini kwani kutokana na ukosefu wa umeme wananchi wataendelea kulishwa nyama za magogo.

Pengine ni wakati wa Shirika la Uendelezaji Viwanda Vidogo (SIDO) na Mamlaka za Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta), kuangalia namna bora ya uchinjaji nyama vijijini ambao utaepuka kutumia magogo na kuwalisha wananchi nyama zenye vimelea vya maradhi uchafu na vibanzi vya miti na mifupa.

Sido na Veta zinaweza kubuni utaratibu bora kwa ajili ya kukata kitoweo hicho ambacho mara nyingi huuzwa 'kienyeji' na kwa ujumla katika mazingira ambayo si salama.

Lakini, pamoja na jitihada za kuboresha mazingira ya nyama kwenye mabucha mengine ambayo ni pasua kichwa na machinjio ambayo nayo yanahitaji utatuzi kwa vile yanaathiri afya za walaji.

Tunaomba kama ambavyo jitihada nyingi zinafanyika kupata maduka ya kisasa yanayotumia msumeno kukata nyama badala ya shoka, ndivyo pia kuwa na machinjio ya kisasa yanayofuata taratibu zote za kitaalamu.

Mara nyingi tumesikia kuhusu ujenzi wa machinjio ya kisasa kama mpango uliotangazwa wa kutumia ardhi ya kilichokuwa kiwanda cha nguo cha Kilitex kilichoko Gongo la Mboto Dar es Salaam kuweka machinjio ya kisasa.

Mara kadhaa Jiji na Manispaa zake zimetoa ahadi za kuboresha machinjio lakini hatujaziona zikileta mafanikio.

Ikumbukwe kuwa kukosekana kwa machinjio za kisasa Dar es Salaam kunasababisha wateja wa kimataifa kununua ama kuagiza nyama kutoka mataifa jirani.

Viongozi wa Bodi ya Nyama watakubaliana nasi kuwa jijini Dar es Salaam kuna maduka ya nyama ambayo kitoweo cha nguruwe huuzwa mpaka hadi Sh. 50,000 kwa kilo.

Nyama hizo zinazozalishwa nchi jirani hutumiwa na wateja wa jumuiya ya kimataifa ambao wanajali ubora, viwango na ladha ya kitoweo ambayo hawaipati hapa Tanzania.

Tunaweza kusema kuwa hatujaona juhudi na bidii zikifanyika katika kuimarisha machinjio ya nyama katika halmashauri zetu. Pamoja na kwamba kumekuwa na jitihada za kuvutia wawekezaji wa kigeni kujenga machinjio ya kisasa, jukumu la kujenga machinjio ya kisasa kama kitega uchumi cha halmashauri na majiji ni jambo lisilokwepeka hata ikibidi kuingia ubia. Tunatoa wito kwa halmashauri na mamlaka zinazosimamia kitoweo kuhakikisha kuwa sambamba na kuboresha misumeno na kuondoa magogo, nyama nazo zinachinjwa na kuandaliwa katika machinjio safi na salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wahudumu wa afya nchini mmemsikia Waziri Mkuu?

**MSIMAMO** wa serikali inavitaka vituo vyote vya umma kutoa huduma bora na za haraka kwa wazee wenye vitambulisho, pia vitenge dirisha maalumu kwa ajili yao.

Lengo la kufanya hivyo ni kuwafanya wazee wasiwe na muda mrefu kwenye foleni wanaposubiri kupata huduma hizo za afya, hali inayoweza kuwasababishia usumbufu usio wa lazima.

Mbali na hilo, halmashauri zote nchini zinaagizwa kuhakikisha zinafanikisha utambuaji na kuwapatia vitambulisho wazee wasio na uwezo, linakuwa endelevu kwa ajili ya kuwanufaisha bila ya malipo, pindi wanapougua.

Kupitia maagizo hayo, ni wazi baadhi ya watendaji wa serikali wenye dhamana za kuamua, kama vile wakurugenzi wa wilaya wamewahi kulalamikiwa kukwamisha Sera Taifa ya Wazee ya Mwaka 2007, watakuwa wamemwelewa.

Hiyo ni kauli ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokuwa mkoani Mtwara katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee Duniani, ambako ndiko kulikufanyika hafla ya kitaifa.

Kiongozi huyo, anawaambia Watanzania kwamba serikali itaendelea kuwalinda wazee dhidi ya vitendo vya ukatili, kwa kuwawekea miundombinu na mazingira bora yanayolinda nafsi zao.

Mazingira bora yanatajwa ni katika mazingira kama vile matumizi ya vyombo vya usafiri, pia kuwekwa utaratibu na vigezo vya kuwawezesha kulipwa pensheni, pia mashirika ya wazee yaelekeze rasilimali wanazozipata kutoa huduma za msingi kwa wazee. Njia mojawapo ya kufanikisha anayoitaja Waziri Mkuu, ni kuepuka kutumia fedha nyingi kwenye mikutano, warsha na kongamano, yasiyowafaidisha moja kwa moja wazee wenye uhitaji maalum.

Anaeleza kuwa utoaji huduma kwa wazee, ni moja ya vipaumbele vya serikali na kwamba itaendelea kuchukua hatua kuboresha maisha yao, ikiwamo kuimarisha ustawi na maendeleo yao.

Nikirudia hoja husika, ni kwamba hatua zinazochukuliwa na serikali kwa sasa ni wazi malalamiko yao ya muda mrefu yanaweza kupungua, kama siyo kumalizika kabisa.

Kinachotakiwa kufanywa ni wahusika kuzingatia maelekezo ya serikali, ili kuwaondolea wazee usumbufu ambao wamekuwa wakiupata wanapokwenda kwenye vituo vya afya kupata matibabu.

Changamoto ambayo wazee wamekuwa wakikutana nayo kwenye baadhi ya vituo vya afya, ni kukaa kwenye foleni kwa muda mrefu kusubiri huduma na wakati mwingine wanakosa hata sehemu ya kukaa.

Hali hiyo, inawalazimu wakati mwingine wasimame kwa muda mrefu kwenye foleni wakisubiri kumuona daktari, lakini kama wangepewa kipaumbele, vituo vya afya visingelalamikiwa kama inavyosikika kila siku.

Jambo la kuzingatia ni kila mtu kwa nafasi yake akumbuke kuwa ipo siku atakuwa mzee, panapo majaliwa ya Mwenyezi Mungu kama atafikia umri huo.

Pia watoa huduma za afya watambue miaka itakwenda, nao watazeeka na wajibu wao pia unawataka kuwahudumia wazee hao na katika mazingira hayo, watahitaji kuhudumiwa au kupata huduma za afya bure.

Niseme, kwa mustakabali huo, hao wahumdumu wa afya, kila mmoja kwa nafasi yake anawajibika kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakielekezwa kwao.

Ikumbukwe, serikali ilishatoa maelekezo kupitia mwongozo wa matibabu bure kwa wazee wenye umri kuanzia miaka 60, wanatakiwa kupata huduma za afya bure katika hospitali zote za umma.

Hata hivyo, utekelezaji kwenye baadhi ya maeneo umekuwa ukilalamikiwa kuwa bado ni wa kiwango cha chini, huku ikidaiwa wazee wanalazimika kutoa fedha kununua dawa.

Bado ninaamini hatua ya serikali kutaka vituo vya afya kutoa huduma bora na za haraka kwa wazee katika dirisha maalum, dhamira sahihi kumaliza adha hiyo.

Vilevile ni hatua nzuri ya wazee 1,837,162 kutambuliwa, kati yao 684, 383 wameshapewa vitambulisho kuwawezesha kupata huduma bila ya malipo.

Ni muhimu kuzingatia kaulimbui ya mwaka huu isemayo "Safari ya Kuzeeka Kwa Usawa" inayoonyesha kutambua malengo ya maendeleo endelevu, kwamba yatafikiwa iwapo watu wa umri wote watakuwa wamejumuishwa.

# *Tutumie vyema madaraja haya*

**Mhariri,**

*KATIKA moja ya maendeleo yaliyofanyika ndani ya Jiji la Dar es Salaam, ni kujengwa daraja la wapita njia kuvuka kwa juu katika barabara zenye magari mengi.*

*Ni zaidi ya miaka 10 tuliona katika eneo la Manzese, ambako baada ya maboresho ya barabara kujengwa mbili, kuliwekwa ya kupita juu.*

*Sehemu nyingine ya kutoa mfano, ni katika sehemu ya Buguruni ambako kulijengwa baadaye daraja kama hilo la Manzese.*

*Hali kadhalika, kunakopita njia za mabasi ya mwendokasi tumeziona daraja, mfano wa Kinondoni barabara ya Kawawa na Kimara.*

*Kwanza baada ya ujenzi huo, moja ya mambo ninayaona kuwa kero mwanzoni nikirejea kule Manzese, bado lilikuwa ngumu kuona watu wanatumia daraja waliloandaliwa, badala yake kuendelea kuvuka chini na kuendeleza hatari za ajali.*

*Sambamba na hilo, ninavyoona Buguruni na Manzese ni kuendelea kuwapo tabia watu wanapanda juu ya daraja kufanya kama vile wako ufukweni kushuhudia vinavyopita chini.*

*Huko nyuma kulishuhudiwa Manzese, ambako wahuni walikuwa wanakaa juu na kufanya uporaji kwa wapita njia.*

**Maguni Shabani,**
**Dar es Salaam**

# Uchaguzi Takukuru wapo kazini, zisituponze kofia, fulana, vinywaji



Wapigakura wakisubiri kutimiza haki yao. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Beatrice Moses**

JIEPUSHE na rushwa, kwani zimekuwa zikiibuka kwenye uchaguzi mbalimbali nchini, licha ya kuwapo sheria zinazoikataza.

Hivi sasa tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu, taifa likiwa bado chini ya uongozi wa Rais Dk. John Magufuli.

Fikra na mihemko ya kisiasa upya imeibuka, maana kuna michuano na misuguano ya kuwania nafasi ndani ya chama na nje ya hapo. Ni zama za moto wa siasa kuwa juu. Hili inajulikana kote nchini na hata nje ya mipaka.

Kuna wakati vitendo hivyo vinachochewa na baadhi ya wanasiasa, wapiga debe, wagombea au wapigakura wanaojipanga na kujionyesha kuwa wanahitaji kupewa chochote, ndipo wahamasike kwenda kupiga kura, wakisahau kabisa ni haki yao ya msingi.

Zipo sheria zinazohusika moja kwa moja. Hapo nitataja Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007; Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa ya mwaka 1985; na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979.

Ni wazi, vita ya kupambana na rushwa nchini inaweza kufanikiwa, iwapo kila mtu ataelewa na kutambua umuhimu wa kukomesha vitendo hivyo, hivyo anashiriki kutoa taarifa, ili wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (Takukuru), imeonyesha juhudi kubwa za kuwajibika kwenye utendaji wake.

Kuna taarifa kadhaa za kimataifa, zinazobainisha Tanzania kupiga hatua katika utendaji wake. Hapo inajumuisha ikiwamo 'Transparency International Corruption Perception Index, 2017' imeiweka Tanzania kwenye nafasi ya 103 kati ya nchi 180 vinara wa rushwa.

Kupitia hilo, Tanzania imepata alama 36, ikilinganishwa na nafasi ya 119 na maksi 31 ya mwaka 2014. Utafiti uliofanywa na taasisi ya nchini - Twaweza, mwaka 2017 ilionyesha zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania waliohojiwa, walikiri rushwa nchini imepungua.

Utafiti mwingine, Taasisi ya Repoa katika mwaka huo, 2017, imeonyesha wastani wa wananchi saba kati ya 10, kwa maana ya asilimia 71, wanasema ushiriki wa serikali kupambana na rushwa ni mzuri. Imani hiyo iliongezeka kutoka asilimia 37 ya utafiti ya mwaka 2014/15.

Orodha ya makosa yanayohusishwa na rushwa, ni pamoja na kukirimu na kushinikiza na kuna kifungu kisheria kinachoeleza kwamba mtu atakayetenda kosa la kutoa hongo kukirimu au kushinikiza, ataangukia katika tendo la rushwa.

Pia inabainisha kwamba mtu akitiwa hatiani na amna kupokea au kutoa rushwa, atakabiliwa na adhabu ya faini isiyozidi fedha za kitanzania, Sh. 500,000 au kifungo kisichozidi miaka mitano, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Sambamba na hilo, kuna tafsiri nyinginezo kisheria zikitamka adhabu kwa anayekutwa na hatia ya hongo, kabla au wakati wa kampeni au kwa kumtumia mwingine,

Hapo kuna vigezo kadhaa kama vile kukopesha, kukubali, kununua au kuahidi fedha yeyote au kitu cha thamani kwa mpiga kura au mtu yeyote kwa niaba ya mpigakura ili apigiwe kura.

Inabainishwa kwamba, kuzuia kupiga kura au wakati wa kampeni wakala wake au chama chake kwa niaba yake kikitoa au kununua au kukubali kutoa upendeleo wa kitu au maslahi ya aina yeyote kwa mpiga kura, au mtu yeyote kwa niaba ya mpiga kura ili kumshawishi kupiga au kuacha kupiga kura.

Wigo wa kudhibiti rushwa ndani ya uchaguzi ni mkubwa, kabla au wakati wa uchaguzi. Hapo inajenga maana kwa mtu, wakala au chama kwa niaba yake wanatoa zawadi au ahadi, mkopo, kununua au mkataba kwa mtu yeyote kumshawishi au kununua uteuzi wa mtu kama mgombea wa chama au uchaguzi wa mtu yeyote kama mbunge.

Inaelezwa, kupata zawadi, ahadi, mkopo, mkataba kwa mtu akanunua au akajihusisha kwenye ahadi au juhudi za kununua uteuzi wa mtu kama mgombea wa chama kwa matarajio ya kupigiwa kura, inaangukia katika kosa.

Huo kimsingi, ni mtazamo unaoangukia katika dhumuni la kuwezesha kampeni za uchaguzi au wakati wa uchaguzi kutoa fedha kwa matumizi ya mwingine yeyote, kwa nia ya kuhonga katika uchaguzi husika.

Inabainishwa, kutoa au kulipa gharama yote au sehemu ya gharama ya chakula, vinywaji na viburudisho kwa nia ya kumshawishi mtu huyo au mtu mwingine kupiga kura au kuacha kupiga kura, au kukubali au kuchukua chakula, vinywaji au viburudisho nayo ni rushwa dhahiri.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema mgombea, mpiga debe na mpiga kura kuwa makini na kuwa mwadilifu na mwaminifu, ili kuepuka kuingia kwenye matatizo ya kunaswa na mkono wa dola.

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Wananchi watulizwa mradi bomba la mafuta

**Na Boniface Gideon,** TANGA

WIZARA ya Nishati imesisitiza kwamba mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanzania eneo la Chongoleani mkoani Tanga, upo na unaendelea kutekelezwa.

Kulikuwapo na madai kuwa mradi huo umekwama kutokana na tofauti ya serikali ya Uganda na wawekezaji.

Hayo yalisemwa na Mratibu wa Mradi wa EACOP kutoka Wizara ya Nishati, Salum Mnuna, wakati wa kikao cha kutoa mrejesho kwa watendaji wa mkoa, wilaya na serikali za vijiji mkoani Tanga kuhusu mradi huo. Alisema tofauti ya Uganda na wawekezaji ilitokea katika manunuzi ya hisa za moja ya waombaji wa kampuni ya Dalo kukamilishwa, huku akieleza kwamba kuna kazi zimesimama, lakini kazi za msingi zimekamilishwa ikiwamo usanifu wa mradi na utambuzi wa njia.

Alisema wanataka viongozi wa mkoa na wilaya kuwaambia wananchi waendelea kufanya shughuli za muda mfupi kwenye maeneo yao ikiwamo kuacha kupanda mazao ya kudumu kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella, alisema mradi unaelekea kwenye hatua ya kutwaliwa ardhi pamoja, lakini alisema kumekuwapo changamoto kwa wenzao wa Uganda.

Alisema changamoto hizo ni za kawaida kwenye miradi mikubwa, hivyo serikali inawahakikishia, itashughulikiwa ikiwezekana mwakani shughuli zote za msingi ziwe zimekamilika na ujenzi uanze.

"Twende kuwafikisha ujumbe huu wananchi ambao mradi utapita waendelee kuwa na subira... mradi unakuja, wajiande kunufaika na fursa za bomba," alisema Shigella.

Kwa mujibu wa Shigella, wataendelea kuwahamasisha, kuwajengea uwezo wa kielimu, kiujuzi na kitaalamu ili fursa zitakapopatikana kusiwe na watu watakaokosa fursa katika ujenzi wa mradi huo.

"Lakini nisisitize kwamba fursa za ajira na nyingine hazijaanza rasmi kwa sababu utekelezaji wake upo hatua ya mwanzo. Pasiwapo watu ambao wanatangaza fursa za ajira za bomba la mafuta, " alisema Shigella.

Alisisitiza kuwa wasijitokeza watu na kuanza kuwatapeli watu na kwamba atakayeonekana anafanya hivyo, ahesabike ni mwizi na atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.



Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Dk. Jesca Lebba, akiwaeleza viongozi wa chama cha wafanyakazi wa serikali za mitaa (TALGWU) mkoani Manyara, juu ya ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya hiyo inayojengwa juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wachimbaji tanzanite walia baruti haishikiki

**Na Allan Isack,** MIRERANI

WACHIMBAJI wa tanzanite walioko katika Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, wameiomba Wizara ya Madini kuwapunguzia gharama za kununua kibali cha milipuko kutoka Sh.100,000 fedha walizokuwa wakitozwa hapo awali.

Wachimbaji hao waliyasema hayo kwenye migodi iliyoko mkoa wa Manyara, wakati wa mkutano uM wa Mirerani, kikao kililenga kuiomba serikali kupunguza bei ya baruti.

Abubakari Madiwa, mmoja wa wachimbaji wa madini ya tanzanite, aliyemwomba Waziri wa Madini, Dotto Biteko, kuwapunguzia ada ya kiwango cha kibali cha kununua milipuko.

Madiwa alisema, Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), kinapaswa kulisemea jambo hilo na kumwomba Waziri Biteko, kufuta kanuni elekezi kwani wachimbaji wanaumia.

"Viongozi wetu wa Marema simameni kidete suala hili kwani wamiliki wengi wa migodi wanalalamika kuhusu ongezeko hili zana zinapandishwa bei kila siku," alisema Madiwa.

Mmoja wa mameneja wa migodi, Rashid Bakari, alisema kiwango hicho siyo rafiki kwa wachimbaji madini kwani kinazidi kuwadhoofisha kiuchumi.

Alisema awali walikuwa wanalipia kibali hicho, kwa Sh. 20,000, lakini ghafla bei ikapanda hadi kufikia Sh.100,000, jambo ambalo ni fedheha kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Mjumbe wa Marema Tawi la Mirerani, Dk. Curtius Msosa, alieleza mikakati waliyoweka juu ya jambo hilo na kusema wapo mbioni kulifikisha wizarani ili litatuliwe ufumbuzi.

# Wadau kahawa watoa mtihani

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WADAU wa kahawa wanaounda Mradi wa Pamoja wa Vyama 32 vya Ushirika wa Kahawa mkoani Kilimanjaro (G32 KNCI-JVE Ltd), wameitaka Wizara ya Kilimo kufikiria upya namna ya kuhamasisha uwekezaji mkubwa wa kilimo hicho.

Aidha, wameipa wizara hiyo changamoto ya kuleta wazo la uwekezaji wa viwanda vya kisasa vya kusindika na kukoboa kahawa vinavyozingatia mahitaji ya soko la dunia, badala ya kuruhusu matumizi ya mitambo ya kizamani kuendelea kutumika.

Meneja wa mradi huo wa G 32, Gabriel Ullomi, aliieleza Nipashe kuwa ili kuimarisha soko la ndani, serikali hainabudi kuhamasisha uwekezaji mkubwa katika sekta ya kahawa, kwa kuanzishwa viwanda vikubwa na vidogo vya usindikaji ili kuongeza thamani kahawa ya Tanzania.

Kwa mujibu wa Ullomi, kwa sasa soko kubwa la kahawa inayolimwa na kustawishwa katika mikoa kadhaa ya Tanzania, lipo Japan.

Alisema ili kuimarisha soko la ndani, serikali haina budi kufanya jitihada za ziada kuhamasisha wananchi kunywa kahawa kuliko chai.

Alieleza Vietnam na Colombia ni wazalishaji wakubwa wa kahawa, lakini asilimia 60 wanatumia kwa matumizi ya ndani tofauti na Tanzania.

Mradi huo, unauza gunia moja la kilo 50, kati dola 220 hadi 260 za Marekani kutokana na ubora wake na kwamba msimu wa mwaka 2018/19, waliuza tani

# Mwenyekiti Bunge asaidia ujenzi bwalo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Bunge la Tanzania, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Najma Jiga, ametoa msaada wa mabati 100, yenye thamani ya Sh. milioni mbili, kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula la shule ya Sekondari ya Leguruki.

Shule hiyo inamilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha.

Pia, ametoa msaada wa mashine ya kudurufu (photocopy), yenye thamani ya Sh. milioni mbili kwa Ofisi ya Jumuiya ya Wazazi ya chama tawala Mkoa wa Arusha, kwa ajili ya kurahisisha uendeshaji wa shughuli za jumuiya hiyo.

Licha ya Mkoa wa Arusha kupewa mashine hiyo, Najma aliahidi kutoa mashine za 'photocopy' kwenye ofisi zote za mikoa za Jumuiya ya Wazazi nchi nzima.

Najma ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (Wazazi), alitoa msaada huo wakati wa ziara yake shuleni hapo, ambapo aliongozana na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Erasto Sima, pamoja viongozi mbalimbali wa jumuiya hiyo Mkoa wa Arusha.

# Marekani yazipa azaki mil. 574/- za Ukimwi

**Na Enock Charles**

UBALOZI wa Marekani nchini umetoa Sh. milioni 574 kwa asasi 11 za kiraia katika mkakati wa kupambana na Ukimwi kutoka katika mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani kwa ajili ya kupambana na Ukimwi (PEPFAR).

Ruzuku hiyo ambayo hutoka katika mfuko wa dharura, imelenga katika kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa kijamii maalum iliyo katika hatari ya kupata maambukizi hayo.

Miongoni mwa makundi hayo ni ya vijana wa kiume na wa kike walio katika umri wa kubalehe, watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi.

Akizungumza katika ya kutunuku vyeti kwa asasi 11 zilizoshinda kati ya 223 zilizoomba kutoka mikoa yote nchini, Kaimu Balozi wa wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, alizitaka asasi hizo kufanya kazi kwa bidii ili kupunguza unyanyasaji uliopo kwenye VVU na Ukimwi kwa kutoa elimu itakayoongeza ufahamu kuhusu VVU na Ukimwi. "Wanufaika hawa wafahamu kwamba wanaoishi na VVU wanaweza kuishi maisha ya kawaida ili mradi wanaendelea kudumisha matumizi ya sawa.

Pia wafahamu wanaume hasa vijana wanaopima ni wachache kulinganisha na wanawake Balozi Patterson alisema.

Miongoni mwa asasi zilizoshinda baada ya kuandika andiko lenye ushawishi ni Bakwata National HIV/AIDS Program, Foundation for Development Organization (FODEO), Jitambue Lembuka Tanzania (JLT), Jumuiya ya Kuelimisha Athari za Dawa za Kulevya, Ukimwi na Mimba Katika Umri Mdogo (JUKAMKUM) na Tanzania Data Lab (dLab).

Mmoja ya washindi wa andiko bora kutoka Asasi ya FODEO, Salum Marwa, alisema fedha watakazokabidhiwa kutoka mfuko huo wa dharura kutoka kwa Rais wa Marekani katika kupambana na Ukimwi (PEPFAR), zitasaidia katika kutoa elimu katika makundi maalum ya kijamii kuhusu VVU na Ukimwi.

"Sisi asasi yetu tumewalenga wasichana na wamama wenye umri mdogo tutawahamasisha kutambua hali zao za afya na wapate ujasiri wa kupima na kuwahamasisha waume zao pia."



Mkurugenzi wa Taasisi ya Nakua na Taifa Langu, ambaye ni mjasiriamali na mshindi wa Malkia wa Nguvu 2019, Jessica Mshama, akisoma risala kwa watu wenye ulemavu kwenye uzinduzi wa mafunzo ya wajasiriamali kwa makundi maalum ya walemavu yaliyofanyika katika kijiji cha Buigiri Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wadau kahawa watakiwa kutafakari ongezeko uzalishaji

**Na Beatrice Moses**

WADAU katika sekta ya kahawa nchini wameshauriwa kutafakari kwa kina jinsi ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo, na kukabiliana na changamoto kadhaa ikiwamo kuyumba kwa bei ya kahawa duniani.

Changamoto nyingine zimetajwa kuwa ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi na kushuka ubora wa kahawa inayozalishwa na vijana kutokujihusisha na kilimo cha zao hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kipi Warioba, aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya Siku ya Kahawa Duniani, iliyofanyika wilayani humo.

Aliwataja wadau hao ni pamoja na watafiti, wakulima, wakoboaji, wakaangaji, waonjaji, wamiliki wa migahawa ya kahawa, taasisi za serikali na sisizo pamoja wanywaji wote wa kahawa.

Warioba pia alisema ni vyema kutafakari ni kwa namna gani wadau husika wanaweza kuongeza uzalishaji wa kahawa siku za usoni ili kuendana na mahitaji ya zao hili ambayo yanaendelea kukua siku hadi siku. "Ili zao la kahawa liweze kuwa endelevu kila mdau anapaswa kutimiza wajibu wake katika sehemu ya mnyororo alipopo," alisema.

Alibainisha kufanya hivyo tutaongeza uzalishaji na pia upatikanaji wa malighafi ya viwanda ambako tutakuwa tumetimiza azma ya serikali ya awamu ya tano ya uchumi wa viwanda, pamoja na kufufua zao la kahawa ambalo ni moja ya mazao ya kimkakati.

Alisema soko la ndani ambalo ndio mkombozi namba moja wa matatizo ya kuyumba kwa bei na kuongeza ajira bado linakua kwa kasi ndogo.

"Jambo hili limeendelea kuifanya nchi yetu kutegemea kwa zaidi ya asilimia 90 ya uzalishaji wetu kwa masoko ya nje," alisema Warioba.

Alitoa wito kwa Bodi ya Kahawa na wadau wote kwa ujumla kuendelea na uhamasishaji kwa jamii kuhusu faida nyingi zitokanazo na unywaji wa kinywaji hiki pendwa cha kahawa na kuondoa dhana potofu iliyojengeka miongoni mwa jamii kuwa kuna madhara kwa afya. "Kinywaji hiki kinafaida kubwa kiafya zikiwamo kupunguza uwezekano wa kupata magonjwa mbalimbali, pia kinywaji hiki huchangamsha mwili na kumfanya mnywaji kuwa na furaha wakati wote," alisema. Sekta ya kahawa ina mchango mkubwa kwenye uimarishaji sekta ya viwanda na hivi sasa nchini kwetu Tanzania tuna viwanda 3,028 kati ya hivyo ni vya kukaanga kahawa na viwili ni vya kutengeneza kahawa ya mezani/unga (Instant coffee).

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa nchini (TCB), Primus Kimaryo, alieleza kuwa kahawa imekuwa kinywaji kinachopendwa zaidi duniani baada ya maji.

Alisema hiyo inajidhihirisha kwa takwimu kutoka Shirika la Kimataifa la Kahawa (ICO) kuwa takribani vikombe billioni tatu hunywewa kila siku duniani.

Kaulimbiu ya maadhimisho haya ya mwaka huu kitaifa imebeba ujumbe unaosema: "Mustakabali wa Sekta ya Kahawa unatutegemea sote".

## Uhakiki wa taasisi dini, jamii mikoa 6 Jumatatu

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii na Taasisi za Kidini kuanzia Jumatatu itaanza uhakiki wa jumuiya za kijamii na taasisi za kidini mikoa sita.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara, Meja Jenerali Jacob Kingu, mikoa hiyo ni Mwanza, Geita, Mara, Simiyu, Kagera na Shinyanga.

Meja Jenerali Kingu alisema taasisi ambazo zitashindwa kuhakikiwa kwa mujibu wa ratiba ya eneo husika zitalazimika kwenda makao makuu ya wizara, Dodoma kwa ajili ya kazi hiyo.

"Iwapo zitashindwa kufanyiwa uhakiki kwa muda uliopangwa zitaondolewa kwenye daftari la msajili," alisema.

Pia alisema kwa taasisi za dini na jumuiya za kijamii ambazo hazijasajiliwa zinatakiwa kufika wakati wa uhakiki kwa ajili ya kupewa utaratibu wa kupata usajili.

"Uhakiki huu ni wa nne utafanyika katika kituo cha uhakiki kilichopo katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kuanzia asubuhi hadi jioni.

"Nyaraka ambazo zitahitajika kwenye uhakiki huu ni pamoja na cheti halisi cha usajili na kivuli chake, stakabadhi ya mwisho ya malipo ya ada iliyolipwa hivi karibuni na Katiba ya jumuiya au taasisi husika iliyopitishwa na msajili."

Alitaja mambo mengine ambayo yanahitajika kwenye uhakiki ni barua inayothibitisha uwepo wa jumuiya au taasisi kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Mtaa au Kata mahali ilipo ofisi husika.

Pia Meja Jenerali Kingu alisema taasisi na jumuiya hizo zinatakiwa kuwa na taarifa ya mkutano mkuu wa mwaka na taarifa ya fedha ya mwaka.

Fomu ya uhakiki inapatikana kwenye tovuti ya wizara kwa anuani ya www.moha.go.tz na kwenye kituo cha uhakiki.

# Taasisi Mkapa yazindua mpango kazi wa bil. 156/-

**Na Faustine Feliciane**

TAASISI ya Mkapa imezindua mpango mkakati wake wa miaka mitano, huku wakitenga kiasi cha Sh. bilioni 156 kwa ajili ya kuinua sekta ya afya Tanzania Bara na Visiwani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mpango huo ulioanza Julai 2019 mpaka 2024, Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo, Ellen Mkondya-Senkoro, alisema malengo ya taasisi hiyo katika mpango huo wa miaka mitano ni kuhakikisha wanatoa huduma bora ya afya na kuwafikia watu wengi kwa gharama nafuu.

Pia kuboresha mifumo ya kuongeza kasi ya kufikia malengo ya kitaifa ya afya kwa wote pamoja matumizi madhubuti ya taarifa kwa kubuni mikakati yenye matokeo.

"Pia tunataka kuona tunasaidia juhudi za serikali katika kutoa huduma bora za afya na kuwafikia watu wengi Bara na Visiwani na kuongeza utendaji wa kitaasisi," alisema Ellen.

Alisema katika kipindi hicho taasisi itaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine kuhakikisha wanafikia malengo yao.

Katika kongamano lililofanyika kabla ya kuzindua mpango huo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliipongeza Taasisi ya Mkapa huku akisisitiza serikali kuendelea kushirikiana nao kufikia malengo ya kimataifa ya huduma za afya.

"Tunatambua kazi ya taasisi hii hasa katika kipindi hiki ambacho serikali inalenga kuimarisha zaidi huduma za kinga za magonjwa ya kuambukiza sambamba na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa ambayo ni tatizo linalokuja kwa kasi kubwa na inaigharimu serikali na familia fedha nyingi katika kupata matibabu husika," alisema Dk. Ndugulile.

Mwanzilishi wa taasisi hiyo, Rais mstaafu Benjamin Mkapa, aliwashukuru washirika wa taasisi hiyo, ambao wamefanikisha kufikia malengo yao.

Aidha, aliipongeza serikali kwa kuimarisha mifumo ya afya ikiwamo upanuzi wa miundombinu ya vituo vya tiba zaidi ya 400 vinavyotoa huduma ya msingi maeneo mbalimbali nchini.



Mkazi wa Dagoni Mafia, Hassan Omar maarufu Mzee wa Lumbesa, akionyesha nyaraka kwa Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, kuhusiana na mgogoro wa ardhi wakati waziri huyo, akiwa katika ziara wilayani Mafia, mkoani Pwani jana, kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi pamoja na kukagua masijala ya ardhi. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Polisi ngangari uchaguzi S/Mitaa

**Na Beatrice Shayo**

JESHI la Polisi nchini limesema limejipanga vizuri katika kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ili kudhibiti vitendo vyote vya rushwa.

Kamishna wa Polisi Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Benedict Wakulyamba, alisema hayo kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, wakati akifungua mafunzo kwa maofisa wa Jeshi la Polisi kuhusu masuala ya uchaguzi.

Wakulyamba alisema, watahakikisha wanadhibiti vitendo vya rushwa kwa asilimia kubwa na yule ambaye atabainika kutoa rushwa atawajibishwa.

"Viongozi wa kweli wanapatikana kwa mifumo na taratibu iliyowekwa kwa mujibu wa sheria na si kwa rushwa, niwahakikishie kuwa tupo vizuri na tutawashughulikia wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwa lengo la kuwalaghai wananchi," alisema Wakulyamba.

Aliyataka makundi ambayo yanasimamia uchaguzi kuhakikisha wanafuata sheria zilizowekwa bila kuzivunja.

"Yapo makundi mbalimbali kama vyombo vinavyosimamia uchaguzi na vimeundwa kwa mujibu wa sheria. Wajibu wao ni kuhakikisha suala la uchaguzi linakwenda vizuri na jamii pia ina jukumu la kusimamia uchaguzi kwa kuhakikisha unakwenda vizuri," alisema.

Alisema pia kuna vyombo vya usimamizi wa sheria yaani polisi ambao wana wajibu wa kusimamia uchaguzi na kuhakikisha unafanyika kwa amani na utulivu.

Alitahadharisha kuwa polisi hawataacha kujipanga kuhakikisha wanausimamia vyema uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na uchaguzi mkuu.

Alieleza kuwa suala la uchaguzi ni jambo la kikatiba na kila mtu ana majukumu ya kuilinda Katiba na hawategemei kuona mtu anasimamia kuivunja.

"Suala la uchaguzi ni la kijamii ambalo linagusa hisia, mawazo na fikra za jamii ni lazima uchaguzi usimamiwe kwa kuheshimu mawazo ya watu na sio vinginevyo," alisema.

Amewataka wananchi kushiriki kikamilifu katika chaguzi hizo zinazokuja ili waweze kupata viongozi watakaowaletea maendeleo.

Naye Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema wameandaa mafunzo hayo kwa lengo la kukutana na kukumbushana majukumu ya kila mdau ili kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na salama.

Alisema wanatambua kuwa kwa mujibu wa Katiba wenye wajibu wa kusimamia na kuhakikisha masuala yote ya usalama yanakuwapo katika kipindi chote cha uchaguzi ni Jeshi la Polisi hivyo ni muhimu kukutana na watu hao mara kwa mara kukumbushana wajibu huo.

"Kipindi cha uchaguzi ni wakati ambao kama hautasimamiwa vizuri kuna uwezekano mkubwa wa kuvunjika kwa amani na mshikamano, hivyo ni muhimu uchaguzi ukasimamiwa kwa haki na usawa ili kusitokee machafuko kama yaliyopo nchi zingine," alisema Olengurumwa.

Alisema watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakilisaidia Jeshi la Polisi kwa kuibua matukio mbalimbali yakiwamo ya ukatili wanayofanyiwa watu hasa watoto na wanawake.

# Makonda achukia mradi kukwama

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameendelea na ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ambayo imekwama kutokana na sababu mbalimbali, huku akionekana kuchukizwa na mradi uliokwama.

Makonda juzi alitembelea miradi ya maendeleo Wilaya ya Kinondoni ukiwamo wa maboresho ya Mto Ng'ombe, unaogharimu Sh. bilioni 32 ukiwa na urefu wa kilometa 7.5.

Akiwa katika mradi huo, Makonda, alichukizwa kuona hakuna chochote kinachoendelea kwenye mradi licha ya viongozi wa wilaya kumdanganya kuwa mkandarasi yupo kazini akiendelea na majukumu yake.

"Tukiwa kwenye kikao kazi kilichofanyika siku 6 zilizopita kwenye ukumbi wa Karimjee, viongozi wa wilaya walisema kuwa mkandarasi yupo 'Site' wakati hayupo kazini," Makonda alisema.

Kutokana na changamoto hiyo, Makonda amemwagiza mshauri wa mradi kumwita mkandarasi huyo mara moja ofisini kwake ili aeleze sababu za kazi kutofanyika kwa wakati mkataba umesainiwa tangu Juni 16, mwaka huu.

Aidha, Makonda alimwagiza mkandarasi huyo kuhakikisha kazi hiyo inakamilika na kukabidhiwa ndani ya miezi 10 kuanzia sasa tofauti na miezi 18 waliyoomba awali.

Kadhalika, aliwaonya watendaji wanaoendelea kumpa taarifa za uongo viongozi wa mkoa huo na kwamba ili kudhibiti udanganyifu huo watatembelea miradi yote kujionea kazi zinazoendelea.

Akiwa katika mradi wa ujenzi wa soko la kisasa Magomeni linalogharimu Sh. bilioni 8.9, Makonda alimtaka mkandarasi kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha soko hilo linakabidhiwa mwezi Desemba mwaka huu.

Pia Makonda aliielekeza Manispaa ya Kinondoni kuitisha kikao na wafanyabiashara wa soko hilo ili wakubaliane namna ya kuweka jiografia ya soko hilo ikiwa ni pamoja na sehemu za maduka, vizimba na eneo la kushusha mizigo.

Alitembelea pia mradi wa ujenzi wa soko la Tandale unaogharimu Sh. bilioni nane na kuelekeza manispaa hiyo kuhakikisha mkandarasi anafanya kazi usiku na mchana ili akabidhi kazi ndani ya miezi sita kuanzia sasa.

HABARI KITAIFA

# Wawili wahofiwa kufa kwa kufukiwa na kifusi

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

WATU wawili wanahofiwa kufa baada ya kufukiwa na kifusi katika mgodi wa wachimbaji wadogo unaomilikiwa na Tereza Buhuru, uliopo katika kijiji cha Imaranguzu Kata ya Lwamgasa wilayani Geita.

Tukio hilo linadaiwa kutokea majira ya saa 12 alfajiri juzi, wakati wachimbaji hao wakiwa katika harakati za kulipua mwamba ndani ya shimo moja kwenye mgodi huo.

Akizungumza na gazeti hili mgodini hapo, mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Evansi Kigongo, alisema kuwa tukio hilo limetokea wakati wakiwa ndani ya shimo hilo na wenzake wanne wakifanya kazi ya kutoa vifaa kwenye shimo hilo ili wafanye kazi ya ulipuaji wa mwamba.

Alisema wakiwa ndani ya shimo hilo ghafla kifusi kiliporomoka na kuwafukia, huku wao watatu wakifanikiwa kujiokoa na wenzao waliokuwa mbali wakifukiwa na kifusi hicho.

Alisema waliojiokoa walikwenda kutoa taarifa kwa uongozi wa mgodi huo na hivyo kuanza jitihada za ukoaji.

"Tulikuwa watano kwenye shimo hilo tukifanya kazi wenzetu wawili walikuwa maalumu kwa ajili ya kulipua mwamba, wao walikuwa mbele yetu kifusi kikawafunika," alisema manusura huyo.

Mkurugenzi msimamizi wa mgodi huo, Allison Zabron, alisema chanzo cha ajali hiyo ni shimo la mgodi jirani lililokuwa limefungwa muda mrefu kuporomoka.

Mhandishi kutoka Ofisi ya Madini Mkazi Geita, Joseph Ng'itu, alisema chanzo ni kifusi kuporomoka wakati wachimbaji hao wakijiandaa kufanya ulipuaji wa mwamba kwenye shimo hilo.

Alisema kuwa shimo hilo lina urefu wa zaidi ya mita 80 waliofukiwa walikuwa umbali zaidi ya mita 80 na walionusurika walikuwa umbali mita 35 kwenda chini ya ardhi.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Geita ambaye ni Mkuu wa wilaya hiyo, Josephat Maganga, aliwataja waliofukiwa na kifusi kuwa ni Kulwa Joseph, Carlos Paulo na walionusurika ni Lazaro Deus, Amos Cosimas na Evansi Kigongo.

Alisema kazi ya kuwatafuta wachimbaji walifukiwa na kifusi bado inaendelea na kwamba katika kuhakikisha wanafanikiwa wameuomba mgodi wa GGM kusaidia vifaa vya ukoaji na ufukuaji.



Sehemu ya vijana wakiwa na mbwa wao waliposhiriki katika chanjo ya kichaa cha mbwa, mjini Kahama, mkoani Shinyanga hivi karibuni.
**PICHA: NEEMA SAWAKA**

# Siku 7 kukamata watuhumiwa ubakaji waliokimbilia Zambia

**Na Felix Mwagara,**
KALAMBO

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ametoa siku saba kwa Jeshi la Polisi mkoani Rukwa, kuwasaka na kuwatia mbaroni watuhumiwa wanne wa wabakaji waliokimbilia Zambia.

Lugola alisema watuhunmiwa hao lazima wakamatwe na waletwe nchini kwa sababu jeshi hilo lina mbinu zote za kuwasaka wanaodaiwa kukimbia kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa baada ya kubainika kufanya uhalifu huo wilayani Kalambo.

Akizungumza na mamia ya wananchi wa Mji wa Matai wilayani Kalambo mkoani Rukwa, Lugola alisema wilaya hiyo inakabiliwa na matukio mengi ya ubakaji, ambapo polisi tayari imewatia mbaroni watuhumiwa wa ubakaji 11 na bado wanne wanaendelee kutafutwa ili wakamatwe.

Lugola alisema kero alizopewa na wananchi hao katika mkutano wa hadhara zikiwamo ubakaji kuwa juu pamoja na idadi kubwa ya wanafunzi kuachishwa masomo kwa ajili ya kufanyishwa kazi wakiwa na umri mdogo, pamoja na wanafunzi kubakwa na kupewa mimba.

"Haiwezekani wahalifu waichezee serikali, lazima wakamatwe, wasakwe kwa nguvu zote na mnipe taarifa mtakapowatia mbaroni watuhumiwa hao," alisema Lugola.

Aliongeza kuwa, wahalifu mbalimbali wakiwamo majambazi, kutokana na uimara wa Jeshi la Polisi wamesambaratishwa na wanaendelea kusakwa katika kona zote nchini mpaka jambazi wa mwisho atakapotiwa mbaroni.

Aidha, Lugola aliwataka wananchi kutoa taarifa kwake na kwa viongozi wa Polisi wa Wilaya na Mkoa endapo kuna mwananchi atabambikiziwa kesi au kuombwa rushwa wakati anamwombea dhamana ndugu yake.

"Hili nilishaliagiza na pia naendelea kuliagiza, ni marufuku kwa askari polisi yeyote atakayemwomba rushwa mwananchi ili ndugu yake apewe dhamana, dhamana ni haki ya mwananchi na ukiingia polisi bure na kutoka ni bure," alisema Lugola.

Kaimu Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kalambo, Deokresi Mkandala, alipokea maagizo ya Waziri Lugola likiwamo la kuwasaka wahalifu hao waliokimbilia Zambia na kuahidi kuyafanyia kazi.

## Benki ya Exim yazindua akaunti mpya ya akiba

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuboresha huduma zake kwa wateja, Benki ya Exim Tanzania, imezindua huduma mpya zinazolenga kuhamasisha wateja wake na jamii kwa ujumla kuhusu uwepo wa akaunti zake mpya tatu.

Akaunti hizo zinazofahamika kama Akaunti ya 'Haba na Haba', Akaunti ya 'Haba na Haba Plus' pamoja na Akaunti ya 'Mzalendo' zote zikilenga kuwawezesha wateja hao kuhifadhi fedha bila makato ya mwezi kwa matumizi ya kuweka akiba na kwa shughuli za kila siku.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma mpya kwa wateja jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Amana wa Benki ya Exim Tanzania, Agnes Kaganda, alisema huduma hizo zinalenga wateja wote ikiwamo wenye kipato cha chini, kati na kipato kikubwa.

"Akaunti hizi za Haba na Haba zinalenga kukidhi mahitaji ya wateja ambao wanahitaji kuhifadhi fedha zao kwa matumizi ya siku zijazo. Huduma zote zimelenga kutatua changamoto ya ukosefu wa namna iliyo bora ya kuhifadhi fedha miongoni mwa Watanzania walio wengi bila kuwa na akiba isiyopungua pitia makato ya kila mwezi," alisema.

Akifafanua kuhusu akaunti ya Haba na Haba, Agnes Kaganda, alisema inawalenga watu wenye nia ya kuweka akiba kwa ajili ya malengo ya baadaye huku akitaja faida zinazombatana na ufunguaji wa akaunti hiyo kuwa ni pamoja na kunufaika na kiwango cha juu cha riba, hakuna makato ya mwezi na huduma ya haraka katika matawi yote ya benki hiyo.

"Pia inatoa fursa ya kuweka kiwango chochote cha akiba kwa wateja, aidha, kila mwezi au kwa muda wowote ambao wateja wataona ina manufaa kwao katika kutimiza malengo yao, wateja wataweza dunduliza akiba zao kupitia simu za mikononi kutoka Mpesa/ Tigopesa/ Airtelmoney/ Zantel kwenda kwenye akaunti ya Haba na Haba,"' alisema.

Kaganda alisema mteja anapaswa kuwa na picha mbili sampuli ya hati ya kusafiria (passport size), nakala moja ya kitambulisho ambacho kinaweza kuwa hati ya kusafiria, kitambulisho cha kitaifa, au leseni ya udereva, uthibitisho wa makazi au kibali cha makazi kwa raia wa kigeni na barua kutoka kwa serikali ya mtaa pamoja na fedha kiasi cha Sh. 50,000 kama kiasi cha kuanzia.

# TRA yahimiza utafiti kabla ya biashara

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA wilayani Kahama mkoani Shinyanga wametakiwa kufanya utafiti kabla ya kuanza biashara zao ili waone kama zina tija waziendeleze au kuziacha.

Aidha, utafiti unaweza kusaidia kuondokana na hasara wanayoweza kupata kutokana na mzunguko wa fedha kuwa mdogo.

"Tunawashauri wafanyabiashara kufanya utafiti kabla ya kuanza kufanya biashara ili kujua kama eneo hilo lina mzunguko mkubwa wa biashara au mdogo hali ambayo inataleta faida au hasara kwa mwekezaji," alisema Willison Makaranga.

Makaranga ambaye ni Meneja Msaidizi wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) Mkoa wa Kikodi wa Kahama, alieleza hayo juzi katika semina ya wafanyabiashara yenye lengo la kutoa elimu juu ya mabadiliko ya sheria za kodi.

Aliwaambia wafanyabiashara hao kuwa wengi wamekuwa wakipata hasara kutokana na kukurupuka na kutokufanya utafiti na hicho ndicho chanzo kikubwa cha kupata hasara katika biashara zao na hivyo wengine kukimbilia kuiacha kufanya biashara. Aidha, meneja huyo msaidizi alisema kuwa unaweza kufanya biashara lakini faida au hasara unazijua wewe unayehusika huku akiwashauri pia kuwa na tabia ya kuweka kumbukumbu za biashara zao kwani zitawasaidia katika siku za baadaye. Katika semina hiyo Makaranga aliomba wafanyabiashara hao kuwa na utamaduni wa kutoa risiti kwa wateja wao na kuongeza kuwa wanapaswa kujua kuwa kila wanapoanzisha biashara serikali inakuwa na asilimia 30.

Kwa upande wake Meneja wa TRA Mkoa wa Kikodi wa Kahama, Warioba Kanire, alisema kuwa walifanya utafiti ikiwa ni pamoja na kuwatembelea wafanyabiashara 762 na kugundua 99 wanastahili kuwa na mashine za kutoa risiti za kielektroniki (EFDs) .

Aliwaambia kuwa lengo la semina hiyo ni kuwajuza wafanyabiashara juu ya mabadiliko ya kodi ili waweze kupata haki zao za msingi na kuboresha huduma na kuwa chachu ya mabadiliko ya kisheria za TRA.

# Aagiza mabaraza ya 'kifisadi' kuvunjwa

**Na Munir Shemweta,** MAFIA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Erick Mapunda, kuyavunja mara moja mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji yasiyotenda haki kwenye maamuzi ya migogoro ya ardhi. Mabula alitoa agizo hilo jana, wakati wa ziara ya siku mbili wilayani Mafia, kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi pamoja na kukagua masijala ya ardhi.

Alisema, kutokana na kero nyingi za ardhi alizozipokea akiwa Mafia amebaini mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji hayafanyi kazi kwa uadilifu na hutoa maamuzi yasiyo ya haki.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, kadri mabaraza hayo yanavyotoa maamuzi hata uanzishwaji wa Baraza la Ardhi la Nyumba la wilaya hiyo hautakuwa na utendaji wa kiuadilifu.

"Ukiwa na watu wasioweza kusimamamia haki itakuwa shida sana, Mkurugenzi wa Wilaya vunja mabaraza yasiyofuata taratibu na kutoa haki kwa walalamikaji na teua wajumbe wapya," alisema Mabula.

Hatua hiyo imekuja kutokana na wananchi kulalamika mbele ya Naibu Waziri kuwa wajumbe wake hawatendi haki wakati wa kutoa maamuzi na hivyo kulalamikia uwepo wa rushwa.

Mohamed Shaban alimweleza Dk. Mabula kuwa, mabaraza ya ardhi ya kata wakati mwingine hayatendi haki na kumtaka anayeshindwa kesi kwenda Baraza la Ardhi la Nyumba la Wilaya la Mkuranga huku wakijua kuwa mlalamikaji atashindwa kwenda Mkuranga kutokana na changamoto za usafiri na hivyo kupoteza haki yake. Awali Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Erick Mapunda, alieleza kuwa mabaraza hayo yanafanya kazi na wajumbe wake wamepatiwa mafunzo ingawa changamoto zipo.

Alieleza kuwa Baraza la Kata la Kilindoni lilidaiwa kuwa chanzo cha migogoro kwa kuwa wakati mwingine halifanyi maamuzi kwa haki.



Mafundi wa ujenzi wakiendelea na kazi ya kuweka zege kwenye vituo vya daladala eneo la kituo cha Temeke Hospitali, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JKCIA yakumbusha wazazi tiba moyo

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wamehimizwa kuwapeleka watoto wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), mapema iwezekanavyo wanapogundua kuwa wana matatizo.

Kuwahi huko kutawawezesha kupata matibabu kwa wakati. Wito huo ulitolewa hivi karibuni na daktari bingwa wa magonjwa ya moyo kwa watoto (JKCI), Naiz Majani, wakati akizungumzia kuhusu kambi ya matibabu ya magonjwa ya moyo ambayo watoto wamezaliwa nayo yakiwamo matundu na mishipa ya damu ya moyo iliyomalizika mwishoni mwa wiki katika taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam.

Dk. Naiz ambaye ni msimamizi wa kambi za matibabu ya moyo zinazofanyika na JKCIA alizitaja dalili za mtoto mwenye magonjwa ya moyo kuwa ni pamoja na kutokwa na jasho kwa wingi wakati wa kunyonya.

Aidha, haongezeki uzito, hupata nimonia, kikohozi cha mara kwa mara, kushindwa kucheza, kuvimba miguu na kubadilika rangi kwenye midomo na kucha kuwa rangi ya bluu.

"Ninawaomba madaktari wanapoona dalili kama hizi kwa mtoto wawalete katika taasisi yetu kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi zaidi," alisema.

Aliongeza kuwa kuna baadhi ya matatizo ya moyo ya kuzaliwa ambayo mtoto hatakiwi kuzidi umri wa mwaka mmoja bila ya kupata matibabu.

Alieleza kuwa mwenye matatizo hayo akichelewa kutibiwa akiwa chini ya mwaka mmoja hawezi kufanyiwa upasuaji tena.

Akizungumzia kambi hiyo, Dk. Naiz alisema watoto 40 walifanyiwa upasuaji kati ya hao 17 walifanyiwa upasuaji wa kufungua kifua 17 na upasuaji wa bila kufungua kifua walikuwa 23 na kwamba hali zao zinaimarika.

# Shule binafsi zashauriwa kuwakumbuka wahitaji

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

SERIKALI imezishauri shule binafsi kuangalia uwezekano wa kusaidia watoto wa kaya maskini ambao wanatamani kusoma lakini hawana uwezo.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia elimu, Mwita Waitara, ndiye aliyetoa ushauri huo.

Naibu Waziri Waitara alizungumza hayo katika mahafali ya kidato cha nne ya Shule za Ujenzi, St. Matthew's, Victory na St. Mark's zilizopo Mkuranga mikoani Pwani.

Waitara aliyekuwa mgeni rasmi alizitaka shule binafsi kuwasaidia kusoma bure angalau wanafunzi watano kila moja, ambao familia zao zipo duni kifedha na wameshindwa kupata elimu.

"Shule za binafsi zinapata faida kubwa kutokana na kutoa huduma kwa jamii na zinatakiwa ziwaangalie wasio na uwezo na wahitaji ambao wanatamani kusoma lakini hawana uwezo kifedha. Hivyo wawachukue watoto angalau watano wawasomeshe," alisema.

Aidha, alisema kuwa serikali inauthamini mchango wa shule za binafsi kwenye elimu, akisema ni muhimu kwa vile huwawezesha wanafunzi waliokosa nafasi katika shule za serikali kusoma.

Aidha, mbali na kutambua mchango huo, pia imeahidi kuendelea kushirikiana na shule za binafsi.

Aliongeza kuwa pamoja na ushirikiano huo alionya kuwa shule zitakazo kiuka taratibu za utoaji elimu hazitavumiliwa na kwamba haitashirikiana nazo.

Akitoa salamu kwa wanafunzi wa shule hizo ambao mwezi ujao wanatarajiwa kufanya mitihani yao kidato cha nne aliwaasa wazingatie masomo kwani elimu ndiyo mkombozi wa maisha yao.

Aliupongeza uongozi wa shule hizo kwa kufanikisha michepuo yote katika shule zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa shule hizo, Peter Mutembei, alisema kuwa kutokana na Tanzania kuwa na kauli mbiu ya kuwa taifa la viwanda, shule zimeitikia wito kwa kutekeleza azma hiyo ya serikali kwa kuiunga mkono.

ama

ALHAMISI OKTOBA 3, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 17

## Je, unajua pombe na cocaine inazaa kifo?




## Mabinti maelfu kufunzwa mbinu kukabili ngono zembe, Ukimwi

Ukurasa 16



Ukurasa 14

## Wataalamu wa wizara wafukua yaliyojificha maziwa ya mama



# Mradi Sayansi Udongo Bagamoyo unavyokaribisha mageuzi kilimo

Ukurasa 18

# Tiba moyo kwa kinamama 'inalipuliwa'

**Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wagonjwa wa Moyo Uingereza kimebaini wanawake wengi nchini humo, wanakufa kwa sababu ya kutojaliwa vyema katika huduma za tiba, kama ilivyo kwa wanaume.

Wataalamu wanasema ni matokeo ya utafiti yanayotengua ya awali katika imani wanawake wengi wamedhurika, hata kufa kutokana na kutotambua maradhi hayo.

Imegundulika ndani ya kipindi cha miaka 10 sasa, zaidi ya kinamama 8,000 nchini Uingereza wamekufa kutokana na shinikizo la moyo.

Wataalamu wanaeleza kuwapo tofauti za matibabu wanavyowasimamia kimamama, kuanzia uchunguzi, matibabu na huduma baada ya hapo, ikielezwa kuwapo upendeleo kwa wanaume na kutopendelewa wanawake.

"Upendeleo huu wa kutojijua, unapunguza nafasi ya kupona kwa mwanamke," inatahadharisha ripoti hiyo ya kitabibu.

Katika ufafanuzi huo, kunaelezwa kuwapo tafsiri tofauti ya viashiria vya shinikizo kati ya wagonjwa jinsia hizo mbili, lakini inasisitizwa kuna mambo vinavyofanana katika viashiria, kama vile maumivu kifuani kwa kila mgonjwa.

Wataalamu wanahimiza kwamba kinamama, vijana, matatizo ya afya yao yanafuatiliwa kwa karibu na umakini.



Mgonjwa wa moyo. **PICHA: MAKTABA**

AFYA

# Wataalamu wa wizara wafukua yaliyojificha maziwa ya mama

• Yakitunzwa yaokoa vichanga 'malaki' • Orodha ya staili za kutoa nyonyo • Serikali ilikosimama na inavyopaswa



Mama akifurahia kumnyonyesha mtoto. **PICHA: MTANDAO**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KILA unakozunguka, simulizi ya malezi ni 'chanda na pete' na mtoto mdogo kuyapata maziwa ya mama.

Kitaalamu yanaelezwa kuwa na maji ya kutosha, yanampatia mtoto joto la kutosha na kumlinda dhidi ya baridi.

Pia kisaikolojia maisha ya kulifaidi titi na maziwa yake, kunaimarisha upendo na uhusiano kati ya mama na mtoto, ambayo ina mchango mkubwa katika ukuaji wa mwili na ubongo wake.

> "Tunaisisitiza jamii kuwa, maziwa ya mama ni msingi wa maisha kwa mtoto, hasa katika kipindi cha siku elfu moja za mtoto.

**MAZIWA YA MWANZO**

Wataalamu wa afya wanaliita 'dang'a.' Haya ni maziwa mazito, yenye rangi ya njano na yanatoka mara tu baada ya mama kujifungua na yanaendelea kutoka kwa siku tatu. Ni muhimu kwa mtoto mchanga kunyonyeshwa dang'a mara baada ya kuzaliwa.

Mtaalamu Lishe ambaye ni Mratibu wa Masuala ya Lishe kwa Kinamama, Watoto na Vijana Balehe, kutoka wizara inayosimamia afya nchini, Tufingene Malambugi, anasema dang'a ni sawa na chanjo ya kwanza kwa mtoto.

Anafafanua ni kwamba yana vitamini na kinga kwa mtoto mchanga dhidi ya maradhi katika kipindi cha mwanzo cha ukuaji na husaidia kusafisha mfumo wa chakula kwa mtoto.

Malambugi anasema, mtoto mchanga ana tumbo dogo mithili ya ngumi yake, hivyo matone machache ya maziwa ya mwanzo ya njano yanatosha kumshibisha na haishauriwi kumpa mtoto chakula aina yoyote, hata maji ya kunywa, isipokuwa dawa kama itashauriwa na mtoa huduma za afya.

"Mtoto mchanga akipewa chakula au maji, itamzuia kunyonya maziwa ya mwanzo, ambayo yana kingamwili kwa mtoto dhidi ya maradhi na mama anashauriwa kunyonyesha mara kwa mara usiku na mchana, bila ya kumhesabia mtoto. Hii itamsaidia mama kutengeneza maziwa ya mtoto kwa wingi zaidi.

"Ukimpa mtoto chakula kingine, itasababisha mama kuchelewa kuanza kutengeneza maziwa, kwani kadri mama anavyonyonyesha, ndipo anapoongeza uwezo wa kutengeneza maziwa. Mama anashauriwa kula vyakula mchanganyiko vinavyopatikana katika eneo lake na kunywa maji ya kutosha," anasema.

Aidha, anasema baada ya siku ya tatu maziwa huanza kutoka meupe yakiwa ya maji maji zaidi, kwa ajili ya kukidhi kiu ya mtoto na akiendelea kunyonya kwa dakika chache, huwa meupe na mazito kwa ajili ya kukidhi njaa yake.

"Ni muhimu mama kumnyonyesha mtoto titi moja kwanza kwa muda mrefu kidogo kama dakika 20 hadi 30 ili amalize maziwa yote katika lile titi, kabla hujamnyonyesha titi lingine. Hii itasaidia mtoto aweze kushiba na atalala kwa muda mrefu akiwa ameshiba," anaelimisha.

Kwa mujibu wa Malambugi, mtoto anapoamka, mama amnyonyeshe titi lingine, ili aweze kunyonya matiti yote mawili na kuweka uwiano, utakaomsaidia mama kuepuka matatizo ya matiti.

**YA MAMA VS MBADALA**

Ofisa huyo anasema maziwa ya wanyama na ya mama, yote yana mafuta yanayosaidia kuleta nishati lishe mwilini. Anafafanua:

"Maziwa ya aina zote mbili yana kirutubishi aina ya protini, ingawa protini zilizomo zinatofautiana kiutendaji katika mwili wa mtoto."

Kuhusu maziwa ya ng'ombe, Malambungi anasema yana protini aina ya 'Kaseini' kwa wingi zaidi, ambayo ni ngumu kuyeyushwa kuliko protini ya aina ya 'whey' iliyoko kwenye maziwa ya mama na yanayeyushwa kirahisi na kufanya kazi haraka.

Protini aina ya 'whey' katika maziwa ya mama ni kwa ajili ya kumkinga mtoto dhidi ya maradhi. Malambugi anaendelea: "Maziwa ya wanyama yenye protini ya 'kaseini' yana kinga maradhi dhidi ya maradhi ya wanyama.

"Vilevile maziwa ya kopo hayana viinilishe vya kumkinga mtoto dhidi ya maradhi na mara nyingi watoto wanaotumia maziwa ya kopo hupatwa na mzio wa mwili (allergy).

"Maziwa ya mama yana mafuta muhimu yanayohitajika katika ukuaji wa ubongo, macho na mishipa ya damu ya mtoto, pia yana kimeng'enyo aina ya "lipase" kinachosaidia kuyeyusha mafuta," anasema.

**LISHE INATUMIKAJE?**

Mtaalamu huyo anasema mafuta yaliyomo kwenye maziwa ya mama, huyeyushwa na kufyonzwa kwa ufanisi zaidi na mwili wa mtoto, kuliko yaliyomo kwenye

AFYA

# Wataalamu wa wizara wafukua yaliyojificha maziwa ya mama

maziwa ya ng'ombe au ya kopo, ambayo hayafyonzwi kwa ufanisi na kusababisha ukuaji duni wa mtoto.

"Maziwa ya mama yana Vitamini A na C kwa wingi na virutubisho vingine muhimu vinavyosaidia kumkinga mtoto dhidi ya maradhi mbalimbali, hivyo humsaidia mtoto kutokuwa na uzito pungufu, kukonda na hata udumavu.

"Maziwa ya mama yana kiasi kikubwa cha madini chuma kinachoweza kufyonzwa kirahisi, kuliko maziwa ya ng'ombe," anasema.

Aidha, anasema kuwapo madini chuma ya kutosha yanamkinga mtoto asikose wekundu wa damu mwilini na hayo yanapatikana kwa kumnyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila hata ya kupewa maji kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo.

"Baada ya hapo mtoto, anahitaji chakula cha nyongeza na cha kutosha kwa kuwa maziwa ya mama hayatoshelezi tena mahitaji ya ukuaji wa mtoto," anasema.

### MAZIWA YASIYOTOSHA

Malambugi anaorodhesha sababu za mtoto kukosa maziwa ya kutosha kutoka kwa mama, kuwa ni kuchelewa kumnyonyesha; kupanga saa maalum za unyonyeshaji; na kutomnyonyesha usiku.

Nyingine anazitaja ni mtoto anaponyonyeshwa kwa muda mfupi; hawekwi vizuri kwenye titi; kutumia chupa au vyombo bandia na kumpa vyakula vya nyongeza kabla hajatimiza umri miezi sita.

Malambugi anaeleza namna ya kukabiliana na tatizo la mama kudhani hana maziwa ya kutosha, mtoto anapaswa kuwekwa kwenye titi mara tu anapozaliwa, kuhakikisha kwamba wakati wa kumnyonyesha, sehemu chuchu yote na sehemu yake kubwa nyeusi inayozunguka chuchu, inaingia mdomoni mwa mtoto.

Pia mtoto anapaswa anyonyeshwe kila mara kwa kadri ya mahitaji yake na daima asipangiwe muda, bali anyonye mpaka aliache titi mwenyewe.

Vivyo hivyo, anapoonekana hajashiba, mtoto huyo anyonyeshwe mchana na usiku. Mlo au kinywaji kingine akiwa na umri chini ya miezi sita, inawezekana panapo ushauri wa mtoa huduma za afya.

### ULISHAJI WATOTO

Ofisa huyo anasema, mtoto anapofikisha umri wa miezi sita, huanza kuzoeshwa kulishwa vyakula vinavyoliwa na wanafamilia, chakula cha mtoto kiandaliwe katika hali ya usafi na kitunzwe katika vyombo visafi na salama, mbali na wadudu au uchafu.

Katika hilo, ofisa lishe huyo anafafanua kuwa, mikakati hiyo ya kiusafi inajumuisha na matumizi ya majisafi na salama kwa mahitaji mengi ya kufanya kazi, ikisaidia kuongeza uwezo wa mwili kusaga na kufyonza virutubisho, inayoendana na kuondoa taka mwilini kupitia mkojo na jasho.



Mama anamnyonyesha mwanawe. **PICHA: MTANDAO**

> **Mtoto anapaswa anyonyeshwe kila mara kwa kadri ya mahitaji yake na daima asipangiwe muda, bali anyonye mpaka aliache titi mwenyewe.**

Anataja nafasi nyingine ya maji safi ni kwamba inaboresha afya na lishe ya mtoto na Malambugi anafafanua: "Magonjwa yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama, yanapunguza ufyonzwaji na utumikaji wa virutubishi mwilini na kusababisha matatizo ya lishe kama upungufu wa wa damu.

"Maradhi yanayotokea mara kwa mara huwa yana uhusiano wa moja kwa moja na taratibu duni za usafi na usalama wa maji ni pamoja na kuhara, homa ya matumbo, kipindupindu, homa ya ini na minyoo."

### LISHE DUNI

"Tunawalenga watoto wa umri huu wa tangu kuzaliwa mpaka umri wa miaka miwili, kwa sababu madhara ya ukuaji na maendeleo yanatokea katika kipindi hiki," anadokeza Malambugi.

Anaendelea: "Madhara ya ukuaji hayawezi kurekebishika na matokeo yake huleta udumavu ambao huathiri maendeleo ya mwili na akili ya mtoto."

Pia anainisha viwango duni vya unyonyeshaji vinachangia kuongeza kasi ya magonjwa miongoni mwa watoto wachanga na wadogo, athari yake ya moja kwa moja katika mfumo mpana ni kuongeza gharama za matibabu na huduma za afya kwa familia na Taifa.

"Hivyo, hupunguza muda wa wazazi au walezi kufanya kazi nyingine za kujipatia kipato na kujikimu kimaisha, badala yake hutenga muda kumhudumia mtoto mgonjwa."

"Tunaisisitiza jamii kuwa, maziwa ya mama ni msingi wa maisha kwa mtoto, hasa katika kipindi cha siku elfu moja za mtoto (kuanzia kipindi cha mimba kutungwa hadi anapofikisha miaka miwii),"anasema.

Malambugi ana mtazamo kwamba, katika mtazamo wa jumla Taifa lenye watoto waliolishwa vizuri tangu utoto wao ni tija kufikia uchumi wa kati, unaolengwa na taifa hivi sasa.

### VIFO TISHIO

Ofisa Lishe Mwandamizi kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Neema Joshua, anasema tafiti zinaonyesha taratibu zisizofaa za unyonyeshaji, zina athiri maendeleo ya uhai wa watoto na inachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya watoto.

Analalamika kwamba, mwelekeo ulioko ni kwamba vifo vya watoto wachanga nchini vipo juu, akitaja wastani kuna vifo 25 hutokea kwa kila watoto wachanga 1000 wanaozaliwa hai.

Hali kadhalika, katika wastani linganifu wa aina hiyo kwamba, kuna vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja 43 kutoka katika kila kundi la watoto 1000 waliozaliwa hai.

Neema analitaja kundi lingine ni la wenye umri chini ya miaka mitano. Anasema katika hao, wastani wa kundi la watoto 1000 waliozaliwa hai, ina vifo 67.

Anabainisha kwamba ili kuondokana na vifo hivyo, kunahitajika uboreshaji wa huduma za afya kwa kuwasaidia kinamama waweze kunyonyesha watoto ipasavyo.

"Kama tukiweza kufanya uboreshaji huo, tunaweza kuzuia vifo zaidi ya 820,000 kwa mwaka vya watoto. Takriban nusu ya magonjwa ya kuhara na theluthi moja ya magonjwa ya njia ya hewa yanaweza kuzuilika kwa kunyonyesha watoto maziwa ya mama," anasema.

### HALI YA UNYONYESHAJI

Mratibu wa Lishe ya Mama na Mtoto, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, Sikitu Simon, anasema takwimu za utafiti wa hali ya lishe nchini za mwaka 2018, zinasema watoto wanaoanzishwa maziwa ya mama kwa wakati sahihi ndani ya saa moja mara tu baada ya kuzaliwa ni asilimia 53 ikilinganisha na asilimia 51 ya mwaka 2015/16.

"Watoto walionyonyeshwa maziwa pekee bila ya kupewa maji au vyakula vingine kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58 ukilinganisha na asilimia 59 ya mwaka 2015/2016," anasema.

Hata hivyo, anasema takwimu hizo zinaonyesha asilimia 31 ya watoto chini ya miaka mitano, wamedumaa ikilinganishwa na asilimia 34 ya mwaka 2015/2016.

AFYA

# Mabinti maelfu kufunzwa mbinu kukabili ngono zembe, Ukimwi

• Wanatoka mikoa 13 kusikoshikika kwa mikasa




Vijana walioko kwenye msafara wakiwa katika picha ya pamoja jijini Dar es Salaam, kabla ya kwenda mikoani.. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

SEPTEMBA 18 mwezi uliyopita, vijana sita kutoka taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali nchini, walianza msafara wa kuzunguka mikoa 13 ya Tanzania Bara na visiwani wakiwa na ujumbe maalum kuhusu afya.

Walio kwenye msafara huo wa siku 21 na asasi zao kwenye mabano ni Raheem Mohamed wa Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (Umati), Augustino Julius na Jackline Rwegasira wa Population Service International (PSI), Nasra Haruna ( Pact) Tanzania na Latifa Mohamed (Restres).

Orodha ya wasafiri hao iko chini ya viongozi wao; Halima Lila, Matilda Deus na Hilda Kwezi. Ni msafara ulioanzia mkoani Tanga na ukaelekea Manyara, Dodoma, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Mara, Kigoma hadi Katavi.

Mikoa mingine iliyomo katika ratiba ya ziara ni: Mbeya, Njombe na Dar es Salaam na mmoja wa Visiwani Zanzibar, wakiwa na ujumbe unaotamka 'Amua' wenye lengo la kuhamasisha vijana wa kike kuwa na uamuzi kuhusu masuala yanayohusu uzazi.

Msafara huo unaratibiwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Hope Center for Children, Girl & Women Tanzania (HCCGWT) ukiwa umewezeshwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mbali na wizara hiyo, wengine waliomo katika orodha kuuwezesha msafara huo ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Wizara ya Vijana, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Ili mambo yaende, msafara huo umepata msaada wa kifedha na kiufundi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), Ubalozi wa Uholanzi Tanzania na Ubalozi wa Ubelgiji Tanzania.

Msaada mwingine wanautaja kutoka Umoja wa Ulaya Tanzania (EU), Engender Health Tanzania, PACT Tanzania, Umati na Kiwohede.

> **Lengo letu ni kuzunguka mikoa yote nchini, lakini tumeamua kuanza na hiyo kwanza, kutokana na ukweli kwamba baadhi yake inakabiliwa na changamoto ya vitendo vya ukatili.**



Mratibu wa Mradi wa HCCGWT, Salha Ng'amilo (kulia), akizungumzia lengo la msafara huo. Katikati ni Mkurugenzi Mkazi wa Engender Health, Prudence Masako na mmoja wa vijana walio kwenye msafara huo, Raheem Mohamed kutoka Umati.

## ULIVYO MSAFARA

Mratibu wa Mradi kutoka HCCGWT, Salha Ng'amilo, anasema lengo la msafara huo ni kuhamasisha vijana kulinda afya zao kwa kujiepusha na vishawishi vinavyoweza kuwasababisha madhara.

"Wanazunguka wakiwa na kaulimbui isemayo 'Amua', yenye lengo la kuhamasisha vijana hasa wa kike kuwa na maamuzi kuhusu masuala yanayohusu uzazi," anasema Ng'amilo.

Anasema, msafara huo unatarajia kuwafikia vijana 300,000 kwa kila wanakokwenda wanakuta vituo vya kukutania na vijana hao, vimeshaandaliwa kwa ajili msafara na kutolewa ujumbe wa afya ya uzazi.

"Hope Centre for Children, Girls & Women Tanzania (HCCGWT) ni shirika lisilo la kiserikali linalofanya kazi Tanzania likiwa na dhima ya kuona vijana wanapata taarifa sahihi katika masuala ya afya ya uzazi na jinsia," anasema.

Kwa mujibu wa Ng'amilo, tangu shirika hilo lianze kazi nchini mwaka 2017, limehamasisha na kuwezesha mazungumzo na jamii, vijana, viongozi wa ngazi ya jamii na serikali za mitaa kuboresha haki ya huduma za afya ya uzazi.

Mratibu huyo anaongeza kwamba, msafara huo pia unalenga kuadhimisha miaka 25 ya Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo, uliofanyika jijini Cairo nchini Misri.

"Mwaka huu ulimwengu unaadhimisha miaka 25 tangu kufanyika mkutano huo, ambao viongozi wa nchi 179 walipitisha mpangokazi ulioainisha afya ya uzazi kama msingi wa kuleta maendeleo ya kitaifa na kimataifa," anasema.

## KULIKONI MIKOA?

Ng'amilo anasema mikoa hiyo imechaguliwa, kwa madai kwamba inakabiliwa na changamoto za mimba za utotoni, ndoa za utotoni, kuongezeka maambukizi ya Ukimwi, ukatili wa kijinsia na ukeketaji.

"Lengo letu ni kuzunguka mikoa yote nchini, lakini tumeamua kuanza na hiyo kwanza, kutokana na ukweli kwamba baadhi yake inakabiliwa na changamoto ya vitendo vya ukatili," anasema.

Anasema afya bora ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii na kwamba serikali ina lengo la kuinua hali ya afya kwa wananchi wote mahali popote walipo ikiwa ni mijini au vijijini.

"Mtoto wa kike ana haki ya kulindwa hadi kufikia umri halisi wa kuolewa au kuzaa siyo kama ilivyo sasa, baadhi yao hubebeshwa mimba au kuozwa wakiwa na umri mdogo, hali ambayo ni hatari kwa afya zao," anasema.

Anasema, kwa kuzingatia hilo taasisi yao imeona kuna haja ya kufikisha elimu ya kumwezesha mtoto wa kike kuwa na uamuzi kuhusu afya yake ili kuhakikisha anakuwa salama.

"Sisi kama taasisi isiyo ya kiserikali hatuna budi kuunga mkono juhudi hizo za serikali kwa kutoa elimu ambayo itawasaidia vijana kuwa makini ili kuwa makini kwa kuwa na afya thabiti kimwili, kiakili na kijamii," anasema.

> **Wanazunguka wakiwa na kaulimbui isemayo 'Amua', yenye lengo la kuhamasisha vijana hasa wa kike kuwa na maamuzi kuhusu masuala yanayohusu uzazi.**

## NCHI ILIKOSIMAMIA

Tanzania imewahi kutajwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), kuwa na viwango vya juu vya matukio ya ndoa za utotoni, kupitia ripoti ya utafiti wake wa mwaka 2016 uliitaja kuwa ni nchi ya tatu barani Afrika.

Mwaka 2012 Shirika la Watoto Duniani (UNICEF), likitaja baadhi ya mikoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni, miongoni mwa mikoa iliyotajwa na asilimia zake katika mabano; Shinyanga (59); Tabora (58), Mara (55), Dodoma (51), Lindi (480, Mbeya (45), Morogoro (420 na Singida (42).

Mikoa mingine ni Rukwa (40), Ruvuma (39), Mwanza (37), Kagera (36), Mtwara (35), Manyara (34), Pwani (33), Tanga (29) na Arusha (27), Kilimanjaro (27), Kigoma (26), Dar es Salaam (190 na Iringa (8), huku sababu za kuwapo hali hiyo zikitajwa kuwa ni mila potofu zinazoendekezwa na baadhi ya jamii.

# Je, unajua pombe na cocaine inazaa kifo?

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU wa afya wametafiti na kubaini mtumiaji wa dawa za kulevya na hasa aina ya Cocaine na pombe kali kwa wakati mmoja, mara zote wanaishia kuchanganyikiwa, hatua ambayo haina mwisho mzuri kimaisha.

Madaktari wanatadharisha kwamba, ni mwanzo wa tabia inayoishia kifo, watu wakijiua wenyewe kwa namna tofauti.

Nchini Uingereza hadi sasa kumegundulika mikasa mbalimbali ya vifo, mfano mmojawapo ukimhusu kijana wa umri wa miaka 21, ambaye katika kufuatilia kifo chake, baba yake na polisi walikuta dawa za kulevya aina ya cocaine gramu nane na pombe kali.

Ilipofuatiliwa kwa kina, ilibainika alijiunga na kundi jipya la marafiki wakiwa watumiaji wa vilevi. Maiti yake ilipatikana baada ya kujirusha kutoka sehemu ya juu na ilikutwa ameacha ujumbe aliyourekodi kusikitikia matumizi hayo ya kilevi. Inaaminika alitambua kwamba ingemwondolea uhai.

"Kuchanganya 'kinachochangamsha' na cha 'kudumaza' kunauvuruga ubongo na kukufanya usijue mahali uliko," anasema.

Katika hilo, dada wa kijana huyo aliyefariki anaongeza:"Napenda kumfikiria zamani, alikuwa kijana mzuri tu. Kufikiria jambo kama hili (kujiua) linalombadili katika namna hii tata, inaonyesha nini angeweza kukufanyia."

Takwimu zinaonyesha nchini Uingereza kulikofanyika utafiti huo mdogo, kumekuwapo na ongezeko la vifo vitokanavyo na dawa za kulevya na pombe, katika miongo miwili iliyopita, huku matumizi ya dawa za kulevya aina ya cocaine inaongezeka maradufu.

Mtaalamu bingwa wa masuala ya matatizo ya akili



Pombe iliyochanganywa na dawa ya kulevya. **PICHA : MTANDAO**

yatokanayo na ulevi, Profesa Julia Sinclaina, kutoka Chuo cha Maradhi ya Akili cha Royal, Uingereza, anasema pombe na cocaine ni vitu viwili tofauti katika mfumo wa matumizi yake mwilini.

"Pombe inadumaza na inaongeza kiwango cha 'gaba' (tindikali) katika ubongo, ambayo ni kama 'hendibreki' inayotufanya tusijihisi kufanya kitu.

"Unaongeza na 'cocaine' kuzichaganya na kuongeza kasi ya mtu bila ya kuwa na kizuizi kutenda jambo ambalo ilikuwa vigumu kwake kufanya. Ni kama kuvuka barabara, huku kukiwapo magari yanayopita kwa kasi," anasema Profesa Sinclaina.

Baadhi ya tafiti nchini Marekani, zina ufafanuzi kwamba mchanyiko huo wa vilevi, unaongeza vifo kwa kiwango cha mara 16 ya maamuzi ambayo mtu angefanyiwa katiika hali ya kawaida.

Sasa wataalamu wanapendekeza wasomi waingie maktaba na maabara, kufanya utafiti wa kina kuhusu eneo hilo ili kufukua mengi yanayohusiana nayo.

Baadhi ya wataalamu madaktari wana maoni kwamba, pindi mtu anapotumia mchanganyiko huo, mwili wake unaanza kupatwa na shinikizo la damu, hasira na akili kushindwa kufanya uamuzi wa busara.

Profesa Sinclair anaeleza:"Watu wanafuatilia vinavyounda pombe na cocaine…lakini hawajui kila mtu ana mapokeo yake."

Inaelezwa kwamba, hapakuwapo na mwongozo rasmi wa kitaaluma kufafanua jambo hilo, hata vifo vyake hadi ufumbuzi wa awali uliofanywa kupitia utafiti na Profesa Sinclair, anasema vifo vyake ni vingi sana.

Hata hivyo, katika mazingira ya ulevi wa namna hiyo kuna ushuhuda wa vifo vya namna tofauti, kama vile kusababisha watu kujiua kwa kujinyonga.

MAZINGIRA

# Mradi Sayansi Udongo Bagamoy unavyokaribisha mageuzi kilim

## • Mlima mpunga avuna ziada gunia 10 • Dk. Msolla: Majaribio mazao tuko juu • DC Kawawa: Msiwatelekeze wakulima wang



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari-Mlingano), Dk. Catherine Senkoro, akimwelezea Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Kawawa, (mwenye blauzi nyeusi na miwani) akieleza mbolea ilivyoleta ufanisi katika shamba la wakulima, baada ya kufanyiwa tathmini ya udongo.

**Na Beatrice Philemon**

***WIKI iliyopita katika safu ya jarida hili, kulikuwapo makala kuhusiana na utafiti wa afya ya udongo na tija yake. Endelea kupata elimu hiyo katika matokeo ya tafiti nyinginezo.***

UKIZUNGUMZIA suala la afya ya udongo hapa nchini si wakulima wote wanafahamu masuala ya afya udongo na aina gani ya lishe inatakiwa kwenye udongo huo, ili kuongeza tija na kuzalisha mazao yenye ubora unaoweza kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi.

Baada ya kugundua upungufu huo, asilimia kubwa ya wakulima nchini hawafahamu undani wa hayo katika kilimo, hivi sasa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI-Mlingano) yenye makao makuu mkoani Tanga, imeanza kujikita katika tathmini ya afya ya udongo kwa kuipima.

Mkurugenzi wa TARI-Mlingano, Dk. Catherine Senkoro, alipotembelea mradi wa umwagiliaji wa Bagamoyo Irrigation Development Project (BIDP), kutathmini afya ya udongo na matumizi ya mbolea inayowasaidia kulima mazao, kulingana na kiwango cha afya ya udongo na matumizi ya mbolea sahihi ya kupanda na kukuzia.

> **“Kupitia kilimo hiki nimeweza kununua kiwanja changu ingawa bado sijaanza ujenzi na isingekuwa kilimo hiki nisingeweza kununua.**

Majumuisho ya awali ni ushuhuda kwamba unaleta ufanisi mkubwa kwa wakulima wa mpunga katika eneo hilo.

Anasema TARI-Mlingano imeamua kujikita katika eneo hilo kuangalia kiwango cha afya ya udongo na virutubisho vinavyotakiwa, ili mkulima aweze kulima kulingana na afya ya udongo, pia kutumia viwango sahihi vya mbolea katika kilimo.

“Afya ya udongo ni muhimu katika kuzalisha mazao yenye tija na mmea, ili uweze kutoa mazao bora unatakiwa uwe na virutubisho 16 na kama kiwango cha virutubisho kwenye mmea ni kidogo, mmea uwezi kukua vizuri na kutoa chakula cha kutosha,” anasema.

### MATOKEO VIPIMO

Dk. Senkoro anasema, kuna aina za mbolea alizozikagua zenye virutubisho vingi kwa mpunga na kuleta ufanisi kwa wakulima katika mradi wa BIDP, kabla ya wakulima kuzipata mbolea hizo.

Watafiti kutoka TARI-Mlingano, walienda katika mradi wa BIDP na kuchukua sampuli za udongo katika mashamba 12 ya mradi, wazopima udongo wake maabara na tathmini yake ilionyesha mashamba yalikuwa na ukosefu wa virutubisho aina ya Nitrojeni, Phosphorus, Sulphur na Zinc.

Baada ya hapo, TARI-Mlingano kwa kushirikiana na kampuni ya OCP Africa ya Morocco yenye ofisi zake nchini, waliamua kuchagua mashamba yenye afya duni, ikawapatia mbolea aina kadhaa wajaribu kupanda na kukuzia mashamba yao.

Kila mkulima aliyefanyiwa tathmini ya udongo, alipewa mfuko wa kilo 25 kwa ekari na mifuko mingine miwili ya mbolea aina tofauti kuwasaidia wajue umuhimu wa kutumia mbolea aina na viwango sahihi, katika kutafuta tija shambani.

Inaelezwa kwamba mbolea hizo zilifanya vizuri na kuleta matokeo chanya shambani na sasa inaendelea kuwasaidia wakulima hao kupata mpunga mwingi, tofauti na miaka ya nyuma.

Anasema wakulima wanatarajia kupata mavuno mengi kutokana na kutumia mbolea sahihi kulingana na afya ya udongo.

Mbali na hilo, anawashukuru wakulima na kuwaruhusu kuangalia aina za mbolea, jinsi zilivyofanya kazi vizuri shambani na kutoruhusu kuongea na watu kujua wanasemaje kuhusu mbolea hizi.


“Tumeongea na kampuni ya OCP Tanzania, wamesema watashirikiana na sisi kuhakikisha mbolea hizi zinapatikana na nyie muwe karibu na watafiti kutoka TARI-Mlingano, Kituo cha Utafiti wa kilimo cha Mikocheni, Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kibaha na Kituo cha Utafiti wa Mazao ya Kilimo cha Mikocheni (MARI), ili muweze kusaidiwa kulingana na mazao mnayolima,” anasema.

### MKULIMA BAGAMOYO

Mkulima Mwinyi Abdallah, mkazi wa Bagamoyo Mjini, anaishukuru TARI-Mlingano na OCP Africa kumpatia mbolea kilo 19 za kupandia na kilo 70 kwa ajili ya kukuzia na mbegu ya mpunga kilo 15 alizopanda katika shamba lake lenye ukubwa wa nusu ekari.

“Namshukuru Mungu mbolea imeleta mafanikio makubwa katika shamba langu. Mpunga umestawi vizuri sana na ninatarajia kuvuna magunia 35 hadi 40, tofauti na napokuwa natumia mbolea za aina nyingine,” anasema.

Kabla ya kutumia mbolea hizo, anasema alitumia zingine katika shamba lake lenye ukubwa wa robo ekari na kupata magunia kati ya 20 na 25 kwa msimu wa





Mkulima aliyefanikiwa, Mwinyi Abdallah, akiwa katika shamba lake la mpunga. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

mavuno, ambayo ni kidogo cha mavuno.

Mwinyi anaishukuru Tari Mlingano na OCP Africa, kufanya tathmini ya afya udongo katika shamba lake na baadaye kumpatia mbolea na mbegu kulingana na afya ya udongo, ambazo zimeleta ufanisi mkubwa.

Anasema, alianza kujikita katika kilimo cha mpunga miaka miwili iliyopita na kilichomvutia, akilenga katika biashara, chakula na maendeleo.

"Kupitia kilimo hiki nimeweza kununua kiwanja changu ingawa bado sijaanza ujenzi na isingekuwa kilimo hiki nisingeweza kununua," anasema.

**DC ZAINABU KAWAWA**

Mkuu huyo anaishukuru Tari-Mlingano na OCP kuwasaidia wakulima katika kutambua na kupata mbolea sahihi kwa ajili ya mpunga na kuwasaidia tathmini ya afya ya udongo.

Mkuu huyo wa Wilaya anaishukuru Tari Mlingano kutathmini afya ya udongo, kutambua aina gani ya udongo inayohitaji virutubisho, ili mazao wanayolima ya ustawi kwa wingi na tija.

Pia Zainabu anakiri mabadiliko makubwa katika mashamba yaliyofanyiwa utafiti ana anafafanua: "Hivi sasa mkulima ataweza kuvuna magunia 35 hadi40 ya mpunga kwa ekari kutoka gunia 25 hadi 30 kwa ekari baada ya kutumia mbolea hizi."

> **Wakati wa utekelezaji, wakulima watajifunza matumizi ya mbolea na mkulima atajifunza kwa kuona.**



Mwinyi Abdallah na wakulima wenzake, akimwelezea Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Kawawa (mwenye miwani), kuhusu tathmini ya afya ya udongo, ufanisi wake na mafunzo ya kilimo biashara waliopewa na mafanikio yake.

Anawashukuru watafiti kuwasaidia wakulima kwa kilimo cha kiteknolojia, kitakachowasaidia kuvuna mazao mengi ya chakula na biashara na rai yake ni kampuni hiyo ya kigeni, kuwahakikisha wakulima upatikanaji mbolea kwa wakati.

"Mmewaonyesha bidhaa nzuri. Basi mhakikishe mbolea hii inapatikana na wakulima watakuwa tayari kutumia mbolea. Wakiikosa hii mbolea watakuja ofisini kwangu kulalamika na mimi kama Mkuu wa Wilaya, sitaki wakulima wangu wapate shida," anasema Zainab.

Mkuu wa Wilaya anasema katika hilo wanapaswa kuwasaidia wakulima wa mpunga, wapate mbolea mashambani, kwa sababu asilimia kubwa hawana uwezo wa kwenda jijini Dar-es Salaam kuzinunua.

**DK. MSHINDO MSOLLA**

Meneja wa kampuni ya OCP Tanzania, Dk. Mshindo Msolla, anasema mpaka sasa kampuni yake imeishaleta mbolea tani 10,000 za aina mbili kwa ajili ya kuwasaidia wakulima.

Pia anasema kampuni imejikita kutengeneza mbolea kulingana na mahitaji ya afya ya udongo na mazao, akizisifia zina bei nafuu.

Mpaka sasa kampuni ya OCP Tanzania imezalisha mbolea kwa ajili ya mazao ya pamba, matunda, mboga, kahawa, alizeti na viazi mviringo.

Kwa mujibu wa Dk. Msolla, mbolea hizo zimeishasambazwa katika mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya, Mtwara, Lindi, Dodoma na Singida, ikifanya vizuri kwa wakulima wa mpunga, mahindi, alizeti, vitunguu, mtama na pamba.

Anasema kuna mbolea maalumu kwa ajili ya pamba na mpaka sasa kuna baadhi ya mikoa inayofanya vizuri kwenye mahindi katika mikoa ya karibu ya majaribio.

Aidha, Dk. Msolla anasema mbolea zote mbili zimetoa mavuno zaidi kwenye mahindi na mpunga, ikilinganishwa na mbolea ya kupandia iliyozoeleka awali.

Akizungumzia mbolea ya zao la pamba, anasema mpaka sasa wamepeleka mbolea kwenye wilaya zinazozalisha za mkoa wa Mwanza, Simiyu, Geita na Tabora.

Anasema ripoti kutoka Mwanza inasema uzalishaji umeongezeka sana, mmea mmoja wa pamba umeweza kutoa vitumba 120, jambo ambalo siyo la kawaida na tani kilo 1,300 kwa ekari, ikilinganisha na kilo 300 za pamba kwa msimu wa kilimo.

Vilevile katika mikoa inayozalisha pamba, wanatarajia kupeleka mifuko 500 ya mbolea yenye kilo tano kila moja kwa ajili ya mashamba ya maonyesho na watakuwa na mashamba 500 ya wakulima kujifunza.

Anasema mifuko hiyo itasambazwa katika wilaya 20 za mikoa yote, inayolima pamba na mbolea hii itatolewa bure kwa ajili ya maonyesho.

"Wakati wa utekelezaji, wakulima watajifunza matumizi ya mbolea na mkulima atajifunza kwa kuona," anasema.

Anasema kampuni anayotumikia inafanya kazi kwa kushirkiana na Wizara ya Kilimo na inatoa huduma mbalimbali, ikiwamo kufanya tathmini ya afya ya udongo, kupima udongo, mafunzo ya kilimo biashara na matumizi sahii ya mbolea.

AFYA

# India yatangaza marufuku matumizi sigara elektroniki

- Vinara wa pili uvutaji duniani

***Wiki mbili zilizopita, jarida hili lilieleza matumizi ya sigara za kielektroniki zinavyopigwa vita nchini Marekani na kuzua mijadala mkubwa kiserikali. India, ikiwa katika orodha ya vinara duniani wa matumizi ya tumbaku pamoja na Marekani, imechukua maamuzi magumu ya kupiga marufuku. Imekuwaje? Makala hii ina undani.***



Mama mzee raia wa India akivuta sigara. **PICHA ZOTE: MTANADAO**

SUALA la matumizi ya sigara za kielektroniki, ambazo zililenga kupunguza ulevi wa sigara za kawaida, badala yake imekuwa kinyume ikibeba athari za kiafya maradufu. Ni hali inayokinzana na madhumuni ya kubuniwa sigara za aina hiyo.

Hivi sasa nchini India mtazamo wa kifikra wa aina hiyo uko katika hatua zaidi, kutokana na Baraza la Mawaziri kumetangaza marufuku ya uzalishaji, uingizaji na mauzo ya sigara za aina hiyo, kwamba zina athari kubwa katika afya ya umma na watumiaji.

Waziri wa Fedha, Nirmala Sitharaman, anasema sababu kuu ya hatua kuchukuliwa hatua hiyo, ni kama ilivyokuwa marejeo ya mjadala unaoendelea nchini Marekani hivi sasa, kwamba "inateketeza afya ya vijana."

Hata hivyo agizo hilo halijawekwa wazi kuhusu uwapo wa vifaa vyake katika nchi hiyo ambayo ina wavutaji sigara wastani wa milioni 100, ambayo kimsingi ni wastani wa mara mbili ya raia wote wa Tanzania.

Aina hiyo ya sigara inayotumia betri, mahitaji yake yanajumuisha mchanganyiko wa vimelea vya nikotini, maji inayounda mvuke, ikielezwa kiafya ambayo bado ni janga.

Kupitia marufuku hiyo ya uvutaji sigara za kielektroniki, inaangukia katika adhabu ya kifungo cha miaka mitatu. Waziri wa Fedha anafafanua: "Hii ina maana marufuku ya uzalishaji, uingizaji, na upelekaji nje, mauzo, usambazaji na matangazo yanayohusu sigara za kielektroniki."

Anasema ushahidi kutoka nchini humo- India na Marekani, kwamba vijana wengi wanaumizwa nayo.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), wakati kasi ya wavutaji sigara halisi ikipoungua duniani, kinyume chake watumiaji wa sigara za kielektroniki wanaongezeka maradufu, idadi yao iko wastani wa milioni 41 kwa mujibu wa takwimu za hadi mwaka jana.

Pia, watafiti wa kundi la Euromonitor, wanasema idadi ya wavutaji sigara hizo huenda wataongezeka kufikia milioni 55 mwaka 2021.

Hatu ya India kupiga marufuku sigara hizo, imekuja baada ya Jimbo la New York nchini Marekani, kuchukua hatua kama hiyo ya kupiga marufuku kilevi hicho kinachoendana na mbinu za kiteknolojia, ikiwaumiza zaidi vijana.

> **Sifa nyingine kuhusu kasi ya uvutaji sigara kwa jumla katika nchi zilizoendelea inashuka, huku katika nchi zinazoendelea na zenye uchumi wa kati, kasi ya uvutaji inaongezeka maradufu.**



Mkazi wa India akivuta sigara bandia.

Hata hivyo, kasi ya India katika utumiaji wa sigara hizo za kielektroniki, haijazifikia nchi kama Marekani, Uingereza na Ufaransa.

### SIGARA DUNIANI

WHO, inasema India kunakokadiriwa kushika nafasi ya nchi tatu vinara kuwa na wavutaji wengi sigara, asilimia 12 ya walevi wake wanatoka katika nchi hizo, huku kukiwapo wastani wa vifo milioni 10 kila mwaka.

Makadirio ya WHO mwaka 2002, ilibaini katika kundi hilo la wavutaji asilimia 70 ni wanaume watu wazima na kinamama watu wazima walikuwa kati ya asilimia 13 hadi 15 ya raia wake.

Nchi hiyo inatajwa kushika nafasi ya kuwa na wavutaji wengi wa bidhaa za tumbaku, nyuma ya China na kila mwaka kuna watu 900,000 wanakufa kutokana na magonjwa yanayohusiana na tumbaku

Nchini China, hadi kufikia mwaka 2014 takwimu zinaonyesha inazalisha na kutumia zaidi ya theluthi mbili (asilimia 34) ya sigara zinazozalishwa duniani kote.

Nako, wakati kuna wavutaji zaidi ya bilioni moja (mara 20 ya Watanzania wote), kati yao wavutaji milioni 800 ni wanaume.

Pia kuna maeneo kama nchi za Indonesia na Bangladesh, ambako zaidi ya nusu ya wakazi wake ni wavuta sigara

Sifa nyingine kuhusu kasi ya uvutaji sigara kwa jumla katika nchi zilizoendelea inashuka, huku katika nchi zinazoendelea na zenye uchumi wa kati, kasi ya uvutaji inaongezeka maradufu.

Ufafanuzi kuhusu mabadiliko hayo, inaelezwa kuwapo uhusiano wa karibu, kati ya tabia ya 'ulevi' wa uvutaji na hali ya uchumi wa mtu kutengemaa.

Pia inaelezwa katika kila vifo 10, mojawapo inatokana na sigara, huku jarida la Tiba la Lancet likisema vifo vyote vya matumizi ya bidhaa ya tumbaku, viko katika nchi nne ambazo ni vinara wa sigara duniani; China, India, Marekani na Russia.





# Asasi sasa zaomba kukutana na JPM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MUUNGANO wa asasi za kiraia wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini umemwomba Rais John Magufuli, kuwa na mkutano na asasi za kiraia ili kusikiliza hoja zao.

Zimeeleza kuwa kama ambavyo, Rais alivyokutana na wafanyabiashara, wachimba madini na watendaji wa kata, ingekuwa vyema kama angekutana na asasi hizo ili zimweleze changamoto zinazowakabili.

Wadau hao walitoa ombi hilo juzi jijini Mbeya wakati wa majadiliano ya asasi hizo zilizowahusisha wawakilishi kutoka mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe.

Walisema baada ya Rais John Magufuli kuonana na makundi mbalimbali nchini, nao sasa ni zamu yao.

Mwenyekiti wa Muungano wa Asasi za Kiraia Mkoa wa Mbeya (Mbengonet), Simon Mwang'onda, alisema asasi za kiraia ni muhimu katika maendeleo ya taifa kwani zinasaidia kutoa hamasa katika maeneo mengi.

Alisema baadhi ya asasi hizo zinahusika na masuala ya afya, mazingira, elimu na kilimo, lakini zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinazifanya zishindwe kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Alisema kutokana na changamoto hizo wameona ni vyema waombe kuonana na Rais ili wapate nafasi ya kuelezea changamoto zinazowakabili na kuona namna ya kuzitatua.

"Hivi karibu Rais alikutana na makundi mbalimbali ya kijamii, aliwaona wafanyabiashara, alikutana na wachimbaji na mara ya mwisho watendaji kata, sasa tunaomba na sisi tupate nafasi ya kuonana naye ili tueleze changamoto zinazotukabili," alisema Mwang'onda.

Alisisitiza kuwa Rais Magufuli ni msikivu na wanaamini atawaelewa na kuwakaribisha kufanya naye majadiliano yatakayowasaidia kuboresha utendaji kazi wao pamoja na kulisaidia taifa kupata maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Child Support Tanzania (CST), Noela Msuya, alisema majadiliano waliyofanya yalikuwa na lengo la kuboresha utendaji kazi wa asasi hizo.

Alisema majadiliano hayo yalifanyika kwa kushirikiana na Shirika la Foundation For Civil Society ambalo ndilo linadhamini shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

Alisema majadiliano hayo pia yalilenga kupata namna bora ya ushirikiano kati ya serikali na asasi za kiraia katika kuwaletea wananchi maendeleo.

"Majadiliano haya ni kwa ajili ya maendeleo na tunajikita zaidi kwenye masuala ya hayo, kama kuboresha muungano wetu, kutetea maendeleo ya taifa letu na ndiyo maana tunaona ni vema tushirikiane na serikali," alisema Msuya.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye majadiliano hayo alizitaka asasi hizo kuepuka kujiingiza kwenye masuala ya kisiasa ambayo ni tofauti na malengo yao.

Alizitaka zisiogope kuzungumza na serikali pale zinapoona kuna mambo ambayo hayaendi sawa.

Alisema serikali ipo tayari kufanya kazi na makundi ya aina yoyote yenye malengo chanya ya kuwasaidia wananchi na hivyo akawataka viongozi wa asasi hizo kuendelea kushirikiana na viongozi na taasisi za umma.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati), wakisoma ramani ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini katika eneo la Mitengo, Mtwara. Kushoto ni Meneja wa Mradi, Godwin Maro. **PICHA: PMO**

# Zoezi la usalama Songwe laleta taharuki, kiwewe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ABIRIA, watumiaji na wadau wengine wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe mkoani Mbeya, wamekumbwa na kiwewe kufuatia zoezi la usalama lililofanyika uwanjani hapo.

Taharuki hiyo ilitokea juzi wakati zoezi la kiusalama lilipofanyika likitanguliwa na taarifa kuwa kulikuwa na mabomu ya kutega kwenye jengo la abiria. Vile vile kulikuwa na maelezo kuwa moja ya ndege iliyokuwa ikitokea nchini Afrika Kusini kuelekea Mashariki ya Mbali kupata hitilafu ikiwa angani na hivyo kutakiwa kutua kwa dharura katika uwanja huo hivyo watu wote wakatakiwa kuchukua tahadhari. Taarifa hizo zilizua kizazaa uwanjani hapo watu wakitimua mbio kuelekea barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) kwa ajili ya kujiokoa huku mmoja wa maofisa wa uwanja huo akitoa maelekezo ya wanakakotakiwa kuelekea kwa usalama.

Katika purukushani za kujiokoa ambazo ziliambatana na kelele, baadhi ya watu walikuwa wanaanguka na kupoteza fahamu kutokana na mshtuko huku baadhi wakibubujikwa na machozi.

Vyombo mbalimbali vya Ulinzi na Usalama wakiwamo wapiganaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, vilisambaa katika eneo hilo kwa ajili ya uokoaji, huku watoa huduma za afya kutoka katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya ya Ifisi wakiwahudumia waliopata matatizo.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Jerome Ngowi, alisema alipigiwa simu na Meneja wa Uwanja huo, akiomba msaada wa Jeshi la Polisi kutokana na kuwepo kwa hali ya hatari ndani ya jengo la abiria na hivyo akawahi kufika eneo hilo na wafanyakazi wake wakashirikiana na vyombo vingine kuweka hali sawa.

"Baada ya kutuliza hali hiyo zikaibuka tena taarifa kuwa kuna ajali ya ndege, kwa hiyo tukaanza tena kupambana lakini nashukuru tulifanikiwa kuituliza hali hiyo," alisema Kamanda Ngowi na kuongeza. "Ninachoshukuru ni kwamba sasa wananchi wameanza kuelewa maana wameonekana kukimbia kwenda mbali na eneo la tukio tofauti na awali ambapo walikuwa wanakimbilia ajali wakijifanya wanasaidia kuokoa kumbe wanakwenda kupora," aliongeza.

Meneja wa Uwanja wa Songwe, Pius Kazeze, alifafanua kuwa kilichokuwa kimetokea uwanjani hapo lilikuwa ni zoezi la kupima uwanja huo pamoja na wadau wake kulingana na miongozo ya kimataifa ya uendeshaji wa viwanja vya ndege. Alisema baada ya kutoa taarifa hiyo vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama vilivyoombwa kutoa msaada viliitikia kwa haraka na kufika eneo la tukio kwa ajili ya kusaidia kuokoa.

Alisisitiza kuwa zoezi hilo halikuathiri ratiba za kuruka na kutua ndege katika uwanja huo kutokana na kufanyika muda ambao hakuna ratiba ya ndege.

"Tunaofanya zoezi ni sisi na sisi wenyewe ndio tunaohudumia ndege kwa hiyo tulipanga kulifanya muda ambao hakuna ndege inayotua wala kupaa ili kuepusha kuvuruga ratiba," alisema Kazeze.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema taarifa ya kufanyika tukio hilo alikuwa nayo lakini alifanya siri ili kupima uwezo wa vyombo vyake vya usalama.

# TRA Mbeya yapaa, yakusanya bil. 7/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato (TRA) Mkoa wa Mbeya imevuka lengo la ukusanyaji wa mapato mwezi uliopita (Septemba) kwa kufikia asilimia 161, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Eunice Mwinuka, wakati wa kikao na wanahabari na kuwapongeza wafanyabiashara wa mkoa huo kwa mwitikio wa kulipa kodi.

Alisema lengo la mamlaka hiyo kwa Septemba lilikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 4.804 lakini wamekusanya Sh. bilioni 7.7.

"Nawaomba wananchi waendelee kulipa kodi kwa hiari ili tuweze kuwa na mwendelezo mzuri wa ukusanyaji wa mapato kama tulivyofanikiwa mwezi Septemba. Tukifanya hivyo tutaiwezesha serikali kutuhudumia vizuri," alisema Mwinuka.

Alisema pamoja na mafanikio hayo, lakini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo baadhi ya wafanyabiashara kuchezea mashine za kielektroniki (EFDs) ambazo zinatumika kukusanya mapato na hivyo kutoa taarifa zisizo sahihi.

Awali Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, alisema kitaifa mamlaka hiyo ilikusanya Sh. trilioni 1.767 sawa na asilimia 97.2 ya lengo kiwango ambacho pia hakijawahi kukusanywa ndani ya mwezi mmoja.

Alisema makusanyo hayo yanatoa tafsiri kuwa wananchi wameanza kuwa na uelewa wa kutosha katika kulipa kodi kwa hiari na kwamba elimu ikiendelea kutolewa mapato yataongezeka zaidi.

"Lakini pia tumeziba mianya ya uvujaji wa mapato na watu wamekuwa na utayari wa kulipa mapato na ikizingatiwa kuwa mwezi Septemba ni miongoni mwa robo za wananchi kulipa kodi zao," alisema Dk. Mhede.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Helena Ntahena, alisema mafanikio hayo ya TRA yanatokana na mazingira mazuri ya ukusanyaji kodi ambayo yamewekwa na serikali.



# Katambi amkalia kooni mkandarasi

Na Paul Mabeja, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ametoa siku tatu kwa mkandarasi wa Kampuni ya KEC ya nchini India kuvunja uzio wa ujenzi wa mradi wa upanuzi uzalishaji wa umeme kutokana na kujengwa chini ya kiwango.

Alitoa agizo hilo jana, wakati alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye ujenzi wa mradi huo unaogharimu Sh. bilioni 125 katika eneo cha umeme zuzu. Akikagua mradi huo, alibaini ujenzi wa uzio wa mradi huo kujengwa chini ya kiwango kutokana na matofali yaliyotumika kukosa ubora.

"Matofali haya yaliyotumika kujenga uzio huu hayana ubora kutokana na kubomoka hata ukiyashika kwa mkono tu bila kutumia vipimo vyovyote hali hii hatuwezi kuifumbia macho, ni lazima ukuta huu uvunjwe na mkandarasi kwa gharama zake mwenyewe," aliagiza Katambi.

Katambi aliliagiza Shirika la Umeme nchini (Tanesco), kuusimamia mradi huo kwa karibu ili kumbana mkandarasi huyo kujenga katika ubora unaotakiwa.

"Hapa leo wapo wenyewe hakuna mtu hata mmoja wa Tanesco, sasa hali hii inatishia sana kwani mradi huu unaweza kuchakachuliwa kwa kiwango kikubwa sana na fedha za Watanzania zikaliwa bila kuwapo na tija yoyote," alisema Katambi.

Kwa upande wake, Mhandisi wa Tanesco, Shafii Kiula, alisema tayari wameshamwandikia barua mkandarasi wa mradi huo kuuvunja ukuta kwa gharama zake na kuanza upya ujenzi kutokana na matofali yaliyotumika kukosa ubora mara baada ya kufanyiwa vipimo.

"Hivi sasa tumemwagiza mkandarasi kuhakikisha kuwa ukuta huu anauvunja wote na kujengwa upya, lakini matofali atakayoyatumia ni lazima tuyapime kwa awamu ya kwanza baadaye siku saba na baadaye baada ya siku 28 ili yaweze kufuzu katika awamu zote hizo," alieleza Mhandisi Kiula.

Naye mkandarasi wa mradi huo, Suraj Prakash, alisema watatekeleza maagizo hayo na kuvunja ukuta huo huku akidai kuwa haikuwa lengo lao kujenga chini ya kiwango bali changamoto ilikuwa ni upatikanaji wa vipimo vya kupima ubora wa matofali.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, akipima ubora wa matofali yaliyotumika katika ujezi wa ukuta katika mradi wa upanuzi wa uzalishaji umeme katika kituo cha Zuzu, nje kidogo ya jiji la Dodoma, jana. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wanaotelekeza wazee kuchukuliwa hatua

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

SERIKALI imeombwa kuzichukulia hatua kali baadhi ya familia ambazo zinatelekeza wazazi au walezi wao kwa kushindwa kutoa huduma za matunzo huku wakiwa na uwezo kifedha.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Katibu wa Baraza la Wazee Wilaya ya Dodoma, Veronica Mveyekule, katika maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani.

Akisoma risala katibu huyo alisema: "Kuna baadhi ya watoto waliozaliwa au kulelewa na wazee hawa na wana uwezo wa kifedha, lakini wamewatelekeza wazazi wao hawataki kuwatunza, tunaomba serikali kuwachukulia hatua kali ili kuwatunza wazee wao."

Alisema wazee hao walijinyima na kuhangaika na kuwatunza wao, lakini baada ya kukua watoto hao wamekuwa hawawajali na kuwatelekeza mitaani na hivyo kuwa mzigo kwenye jamii.

Mveyekule alisema wazee wanakabiliwa na changamoto ya gharama kubwa za kununua dawa kwenye maduka kutokana na kukosekana kwa hospitali.

Waliomba halmashauri zote kuhakikisha wanawapatia mikopo kupitia asilimia zinazotengwa kwa ajili ya makundi mbalimbali kwenye maeneo yao kwa kuwa wamekuwa wakiikosa fursa hiyo kwa sababu bado kuna wengine wana uwezo wa kuzalisha uchumi.

Alisema kuna jumla ya wazee 21,445 katika kata 41 za Jiji la Dodoma wanawake wakiwa ni 12,052.

Pia alitaka kuundwa kwa mabaraza ya wazee kuanzia ngazi ya mtaa hadi mkoa ili kuwapa fursa wazee kushirikishwa kujadili changamoto na kuziwakilisha kwenye ngazi za uongozi wa serikali pamoja na mabaraza ya madiwani.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema serikali inawajali wazee ndio maana ilitunga sera za wazee mwaka 2003 ikiwa na lengo la kuwahudumia kundi hilo.

Akijibu risala yao, Katambi aliagiza kama kuna watoto wameshindwa kutunza wazazi wao na wana uwezo wa kifedha jamii ipeleke majina hayo kwa viongozi wa wilaya ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Katambi alisema katika sera hiyo serikali iliweka mkazo mkubwa wa kuhakikisha wazee wote wanatibiwa bure kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Alieleza kuwa wazee 4,551 walihudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya bila malipo wakitumia vitambulisho vya wazee walivyotengenezewa na serikali.

## CCM Dodoma wampongeza JPM

Na Peter Mkwavila, DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, kimempongeza Rais John Magufuli kwa hatua yake ya kuruhusu washtakiwa kosa la uhujumu uchumi kuomba msamaha na kurejesha fedha.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa chama hicho mkoani hapa, Godwin Mkanwa, wakati wa ufunguzi wa kongamano la kimataifa lililoandaliwa na Kanisa la Tanzania Fellowship, linalofanyika kwa kushirikisha makanisa yote ya ndani na nje ya nchi.

Pia aliliomba kanisa hilo kuwa na tabia ya kutembelea kwenye magereza ili kuwahimiza wenye makosa kama hayo kuomba msamaha.

Mkanwa alisema uamuzi wa kuwataka wenye makosa ya uhujumu uchumi kuomba msamaha ni kitendo cha uzalendo kwa Rais hivyo kama kanisa ni wajibu wao kuwahubiria watu hao wenye makosa ili waweze kuomba msamaha na kusamehewa.

"Ninyi watumishi wa Mungu nendeni huko mkawakumbushe maana kuna wengine wamekaa huko mpaka wamechanganyikiwa sasa muende huko mkawakumbushe waone haja ya kukiri makosa yao," alisema.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini nchini kuhamasisha jamii hasa vijana kufanya kazi za kujiingizia vipato ili kwenda sambamba na falsafa ya hapa kazi tu.

Kwa upande wake, Askofu Godfrey Malasi wa Tanzania Fellowship of Churches, alisema kanisa hilo hufanya makongamano kama hayo kila mwaka pamoja na kusaidia kutoa msaada kwa jamii.

Alisema kwa mwaka huu kongamano hilo linafanyika jijini Dodoma na wamepanga kutembelea katika Gereza la Isanga na kutoa misaada kwa wafungwa na kuwapa neno la kuwafariji na kutia matumaini.

Alisema vijana wengi wameharibika kutokana na kutowekewa misingi imara na kufundishwa neno la Mungu tangu wakiwa wadogo, kanisa lina kazi kubwa ya kuendelea kuokoa roho za watu na kuendelea kutoa maonyo mbalimbali katika nyumba za ibada.





## SMZ kuagiza matrekta 100

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imesema kutokana na uhaba wa matrekta ya kilimo nchini, serikali ina mpango wa kuongeza matrekta 100 ili kusaidia kuondosha usumbufu na kukidhi mahitaji ya wakulima.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Makame Ali Ussi, alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mwakilishi wa Kijitoupele, Ali Suleiman Ali, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kuongeza matrekta ya kilimo ili kuwasaidia wakulima.

Hatua hiyo, alisema itasaidia kupunguza changamoto za wakulima kuchelewa kulimiwa mashamba yao pale muda unapofika.

Alisema matrekta hayo yatagaiwa katika halmashauri mbalimbali za Unguja na Pemba ili yaweze kutumika kwa ajili ya kilimo.

Naibu Waziri alitumia fursa hiyo kuwataka wajumbe wa baraza hilo kuwashajihisha wananchi kuhakikisha wanalipa fedha mapema kwa ajili ya kupata matrekta ya kulimiwa ili kuondoa usumbufu.

Akijibu swali la msingi lililoulizwa na mwakilishi huyo, aliyetaka kujua kiasi cha fedha kinacholipwa kwa eka moja kwa uchimbaji na uburugaji, Makame alisema wakulima kwa eka moja wanatakiwa kulipa Sh. 30,000 kwa ajili ya kuchimbuliwa na Sh. 30,000 kwa ajili ya kuburugiwa ikiwa ni njia ya ruzuku.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, serikali inafanya hivyo kutokana na kuweka kipaumbele katika kilimo cha mpunga kulinganisha na mazao mengine ya nafaka.

"Mazao mengine kama vile mihogo, ndizi, viazi vikuu na viazi vitamu na mazao ya mboga yanalimwa kutokana na umuhimu wake," alisema.

Pia alisema serikali inatoa ruzuku kwa wakulima wa mpunga kwa lengo la kuwapunguzia gharama zinazotokana na uzalishaji wa zao hilo.

Sambamba na hayo, alisema serikali imefanya hivyo ili kusaidia kuwahamasisha wananchi kulima kilimo hicho kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula katika kaya na taifa kwa ujumla.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe (kulia), akizungumza na Waziri wa Biashara, Balozi Amina Salum Ali, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Balozi Iddi awapa CCM somo zito

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka viongozi wa majimbo wakiwamo wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia chama hicho, kutumia vyombo vya habari kueleza mambo wanayoyafanya ili wananchi kufahamu mwelekeo wa chama chao.

Balozi Iddi aliyasema hayo jana, wakati akizungumza kwenye hafla ya kutangaza kuingia sokoni gazeti la Uhuru wa Kijani iliyofanyika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui.

Alisema CCM na serikali imekuwa ikifanya mambo mengi kupitia ilani yake ya uchaguzi, lakini hayatangazwi na kusababisha watu ambao hawakitakii mema chama kusema uongo.

"Vikao vya mara kwa mara vya Halmashauri Kuu vimekuwa vikikisisitiza hili. Yako mengi yanayofanywa na chama na hata maendeleo yanayofanywa na serikali zetu, lakini hamsemi wala kuyatangaza na kuacha watu wengine watusemee uongo," alisema.

Balozi Iddi ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alisema umefika wakati kwa viongozi kutumia fursa hiyo kutangaza maendeleo yao majimboni ili kuwaziba midomo wale ambao wanaosema CCM haijafanya kitu.

"Sasa ni fursa adhimu kwetu kutangaza ili wale wasiokitendea mema chama chetu waache mara moja kuwapotosha wananchi," alisema na kuongeza kuwa wakati umefika kwa viongozi wa majimbo kuitangaza miradi inayofanyika.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdallah Juma Sadallah, alisema wananchi nataka wapate habari mbalimbali kwa ajili ya maendeleo.

Alisema, uwepo wa gazeti hilo ni njia pekee ya kuwaunganisha wanaCCM na wananchi katika kuona harakati zao za kisiasa wanazofanya majimboni zinasikika kwa wananchi.

Hivyo, aliomba uongozi wa Uhuru ya Kijani kuwa ni jambo la busara kuona nafasi ya Zanzibar zinawiana kimkakati kwani wote wana ilani moja, katiba moja na kuongozwa na chama kimoja.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Uhuru Media Group, Ernest Sungura, alisema kuanzishwa kwa gazeti hilo kunatokana na kuona gazeti la Uhuru halijatumika kimkakati na kutekeleza agizo la Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais John Magufuli kuanzisha uhuru ya kijani kwa kuandika mambo yaliyofanywa katika majimbo na viongozi wakuu.

# Chanzo matokeo mabaya mtihani chaanikwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema sababu za kufanya vibaya kwa shule za Kiembesamaki, Mpendae, Tumekuja na Haile Selassie kwa mitihani ya kidato cha sita yaliyotangazwa hivi karibuni ni utoro wa wanafunzi.

Sababu zingine ni idadi kubwa ya wanafunzi madarasani na upungufu wa walimu wa sayansi hasa masomo ya hisabati na fizikia.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Simai Mohamed Said, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana wakati akijibu swali lililoulizwa na Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said.

Katika swali hiyo, Machano alitaka kujua sababu zipi za msingi zilizofanya wanafunzi kufeli katika shule hizo kwa kiwango cha kutisha. Alisema mbali na sababu hizo, pia mwamko mdogo wa wanafunzi hasa kwa shule za vijijini pamoja na utandawazi uliokithiri kwa wanafunzi kutojikita zaidi katika masomo yao na ushirikiano mdogo baina ya wazazi na walimu kwa kufuatilia maendeleo ya watoto wao, yanachangia wanafunzi kutofanya vizuri.

Kuhusu hatua zilizochukuliwa na wizara kutatua matatizo hayo, Naibu Waziri alisema serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwamo kuajiri walimu wa sayansi.

Alisema mbinu zingine ni kuleta walimu wa kujitolea kutoka Nigeria kwa masomo ya Sayansi hasa Hisabati na Fizikia pamoja kuhamasisha jamii kupitia madiwani, masheha, wazazi na wanafunzi kuhusu suala la utoro na umuhimu wa elimu kwa wanafunzi. Hata hivyo alisema wizara pia itafanya ziara za ufuatiliaji wa mara kwa mara ambazo zinajumuisha viongozi wakuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na maofisa kutoka idara ya elimu ya sekondari.

Mkakati mwingine kawa mujibu wa Naibu Waziri ni wizara kupeleka vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vitabu na vifaa vya maabara ili kutatua tatizo la wanafunzi kufeli.

# Mtumishi wa afya ajinyonga, aacha ujumbe

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MTUMISHI wa afya, Moses Amasha Mbilinyi (26), aliyekuwa anafanya kazi kwenye Kituo cha Afya Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, amedaiwa kujinyonga nje ya nyumba ambayo alikuwa amepanga katika kijiji cha Mbika Ushetu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Audax Majaliwa, tukio hilo limetokea Septemba 29, mwaka huu kati ya majira ya saa 3 usiku hadi saa 5, ambapo mtumishi huyo alitumia waya wa 'extension' kujinyonga na kusababisha kifo chake.

Alisema mtumishi huyo alikuwa amepanga nyumba kwenye kijiji cha Mbika Halmashauri ya Ushetu eneo la kituo chake cha kazi na baada ya kufika majira ya usiku, alitoka nje ya nyumba hiyo na kuamua kujinyonga kwenye mti kwa kutumia waya wa extension.

"Tulipofika eneo la tukio tulikuta Mbilinyi ameacha ujumbe wa maandishi usemao 'chanda' kama kikitokea chochote nimeacha viwanja viwili Kahama anavijua Malubalo, viwili Nyamilangano, kimoja sijalipia laki tano, hivyo ni mali ya Nancy," Majaliwa alikariri taarifa ya Mbilinyi.

Aidha, alisema chanzo cha tukio hilo kinadaiwa msongo wa mawazo na kwamba Jeshi la Polisi linaendelea kuchunguza tukio hilo.

Majaliwa alisema kuwa mwili wa Mbilinyi umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola akizungumza na wananchi wa Mji Mdogo wa Matai wilayani Kalambo, Mkoa wa Rukwa, jana. Lugola ametoa siku saba kwa Jeshi la Polisi mkoani humo, kuwasaka na kuwatia mbaroni wabakaji wanne waliokimbilia nchini Zambia. **PICHA: WMNN**

# Waziri akataa taarifa anwani za makazi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, ameikataa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa anwani za makazi na postikodi ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema wakati wa ziara yake wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Nditiye alikataa taarifa hiyo ya utekelezaji iliyowasilishwa na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Godwin Barongo, wakati akiwasilisha taarifa yake kwa kuwa haina utekelezaji wowote uliofanyika wa kuchagua majina ya mitaa ili serikali iweze kuweka namba za nyumba, vibao kwa malengo ya kukamilisha anwani za makazi na postikodi ili kila mwananchi apate anwani yake na atambulike mahali anapoishi.

Alifafanua kuwa mapema mwanzoni mwa mwaka huu aliambatana na Naibu Waziri wa ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi, Mwita Waitara na kuwa na kikao cha pamoja kati ya madiwani na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema na Buchosa, ambapo wataalamu wa wizarani na wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), waliendesha mafunzo ya kujenga uelewa kwa madiwani na watendaji kwa malengo ya kuwawezesha kufanikisha kazi ya kuchagua majina ya mitaa.

"Tunachohitaji ni majina ya mitaa, ninasikitishwa na suala la madiwani wanapopata ugumu wa kuchagua majina ya mitaa ni lazima madiwani wakae tupate majina ya mitaa na ulikuwa ni taarifa kuwa tunakuja ila hukufanya jitihada zozote kutekeleza," alisema Nditiye.

Alisema serikali itafikiria upya na kuamua kuchukua madaraka ya madiwani ili kuweka majina ya mitaa kwa kuwa sasa hivi simu zinatumika kufanya miamala mbalimbali na hii itasaidia huduma na bidhaa zifikishwe kwa wananchi, kwa kuwa anwani za makazi na postikodi ni muhimu kwa uchumi na usalama wa nchi yetu na tunataka kila mwananchi atambulike anapoishi.

Ofisa Masoko wa Shirika la Posta mkoani Mwanza, Rose Kavemba, alisema kinachohitajika ni kurasimisha mitaa, kupata majina kutoka kwa viongozi wa vijiji, mitaa na kwa madiwani kisha kutenga itakayowaongoza kufanya utekelezaji kwa kuwa kuna changamoto mkiwaachia madiwani wanavutana.

Naye Mratibu wa Kitaifa wa Mpango wa Makazi na Postikodi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Jampyon Mbugi, alisema kuwa ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huo, kila halmashauri inatakiwa iunde kamati kuendana na mwongozo wa mpango huo.

# Wanafunzi 71 wapewa ujauzito

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAFUNZI 71 wilayani Shinyanga Vijijini wamepewa ujauzito na kuacha masomo.

Hayo yamebainishwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Deus Mhoja.

Alisema takwimu hizo ni za kuanzia Julai mwaka jana hadi Juni mwaka huu, na kufafanua kuwa wanafunzi waliopewa ujauzito sita wa shule za msingi na 65 sekondari, hivyo wanafunzi 71 kuacha masomo.

Mhoja alibainisha hayo juzi alipokuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Hoja Mahimba, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani, ambayo kiwilaya mkoani Shinyanga yalifanyika Kata ya Tinde Shinyanga Vijijini.

Alisema wazee ni hazina kubwa katika taifa, hivyo wanapaswa kusimamia maadili ya vijana hasa kwa wanafunzi kike, kuacha tabia ya kufanya mapenzi katika umri mdogo, ili kutokomeza tatizo hilo la mimba ambalo limekuwa likizima ndoto zao na kusababisha taifa kukosa wataalamu wa baadaye.

"Licha ya serikali kuendelea kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili wazee likiwamo suala la matibabu na sisi tunawaomba msimamie maadili ya vijana hasa wanafunzi wa kike, waache kufanya ngono katika umri mdogo ili wapate kutimiza ndoto zao," alisema Mhoja.

"Sasa hivi mnalalamika hakuna madirisha ya wazee kwenye baadhi ya huduma za afya, tatizo ambalo linasababisha ni kuwapo kwa upungufu wa wataalamu wa afya na madaktari bingwa wa magonjwa ya wazee, lakini kama watoto wetu wakaacha ngono zembe na kutimiza ndoto zao, na imani changamoto hii itakwisha," aliongeza.

Naye Katibu wa Baraza la Wazee halmashauri hiyo, Boniphace Boazi, akisoma risala, alisema changamoto kubwa ambayo inawakabili ni ukosefu wa matibabu, ambapo kuna jumla ya wazee 12,922 na waliopewa vitambulisho vya matibabu wapo 5,568, na 7,354 hawana vitambulisho hivyo.

## HABARI KIMATAIFA

# Vita yazuka Mali, askari 25 wauawa

**BOULKESSI,** Mali

WANAJESHI 25 wa Mali waliuawa katika mapigano Jumapili usiku, ambayo yameendelea hadi juzi yanayohusisha Jeshi la Mali na watu wanaoshukiwa kuwa wanamgambo wa Kiislamu.

Kundi hilo la watu wenye silaha walidhibiti kwa muda mfupi ngome za Jeshi la Mali katika kisa ambacho kinaelezwa kuwa wanajeshi wengine 60 hawajulikani waliko.

**Askari wengine 60 wa Mali hawajulikani waliko kwa wakati huu na jeshi limepata hasara kubwa kwa upande wa vifaa.**

Bado haijafahamika idadi rasmi ya watu waliouawa katika mapigano hayo makali ya siku mbili yaliyotokea katika Mji wa Boulkessi. Kwa sasa, serikali ya Mali ndiyo pekee inayotoa taarifa rasmi.

Kwa mujibu wa msemaji wa kikosi cha wanajeshi wa Mali, kilicho chini ya usimamizi wa jeshi la pamoja la G5 Sahel, kikosi hicho kimepoteza askari 25, kulingana na ripoti ya awali.

Askari wengine 60 wa Mali hawajulikani waliko kwa wakati huu na jeshi limepata hasara kubwa kwa upande wa vifaa.

Zaidi ya wanajihadi 15 wameuawa katika mapigano hayo, kwa mujibu wa Waziri wa Mawasiliano,Yaya Sangare, aliyeongeza kuwa Jeshi la Mali juzi Jumanne ilirejesha kwenye ngome zake.

Alithibitisha kwamba washambuliaji walidhibiti kwa saa kadhaa ngome za kikosi cha Jeshi la G5 Sahel kutoka Mali.

Lakini katika hali ya kukabiliana na adui, washirika wa Mali katika uwanja wa vita ambao ni kikosi cha jeshi la Ufaransa cha Barkhane na Umoja wa Mataifa, waliingilia kijeshi Boulkessi na kuokoa jahazi, alisema Waziri Yaya Sangare. **RADIO UFARANSA**

## Wakimbizi waanza kurejea Burundi

**BUJUMBURA,** Burundi

KAZI ya kuwarejesha Burundi wakimbizi wa nchi hiyo walioko kwenye kambi za wakimbizi nchini Tanzania inaendelea, licha ya madai ya kuwapo ukinzani kutoka kwa baadhi ya wale wasiotaka kurejeshwa.

Serikali za Burundi na Tanzania Agosti, mwaka huu zilikubaliana kuwa wakimbizi waliokuwa wakiishi Tanzania wataanza kurudi nyumbani kuanzia Oktoba mosi mwaka huu.

Nestor Bimenyimana, ofisa wa juu wa serikali ya Burundi anayehusika na mradi wa kuwarudisha nyumbani wakimbizi, ameliambia Shirika la Habari la Uingereza la Reuters kuwa mpango huo utaanza kutekelezwa baada ya makubaliano ya serikali yake na Tanzania.

Aidha, alisema kuwa kundi la kwanza, litawajumuisha wakimbizi 1,000 ambao Bimenyimana, alisema wanaorudi kwa hiari yao.

Hata hivyo, duru kutoka kwa baadhi ya wakimbizi zinasema kuwa wengine zaidi ya 900 wametakiwa kujiorodhesha mbele ya mamlaka za Tanzania.

Wakimbizi walisema wana wasiwasi kuwa kazi hiyo itawarudisha makwao kwa nguvu.

Mnamo Agosti mwaka huu, Tanzania iliagiza wakimbizi kutoka nchini Burundi kurudishwa makwao na kusema kuwa hali ya kiusalama katika taifa hilo sasa imeimarika.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Tanzania, Kangi Lugola, alitangaza kuwa wakimbizi 2,000 watarudishwa Burundi kufikia Oktoba mosi.

Tanzania imekuwa inalinyooshea kidole cha lawama Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia wakimbizi la UNHCR kwamba ndio linakataa wakimbizi hao kurudishwa nchini Burundi.

Tanzania inashikilia msimamo kuwa sababu iliyoifanya kuwapatia hadhi ya ukimbizi raia hao wa Burundi kwa sasa hazipo na kwamba ina kila sababu ya kuwataka warudi makwao.

Mvutano kati ya Shirika hilo la wakimbizi la Umoja wa Mataifa na Serikali ya Tanzania kuhusu suala la kuwarejesha makwao wakimbizi wa Burundi umekuwa ukiendelea kwa miaka kadhaa sasa.

Mwezi Agosti mwaka 2017, Serikali ya Tanzania ililipatia Shirika la UNHCR siku saba kuanza kuwarudisha wakimbizi wa Burundi ambao wanataka kurudi kwao kwa hiari, ama sivyo serikali ifanye zoezi hilo yenyewe.

Tanzania ndiyo nchi inayohifadhi wakimbizi wengi zaidi kutoka Burundi kuliko nchi nyingine yoyote ile katika ukanda wa Afrika Mashariki. **RADIO UFARANSA**



Ndivyo maduka ya pombe yalivyokuwa nchini Urusi kabla watu wengi kuacha pombe. **PICHA: AFP**

# Warusi sasa waiasi Vodka

**MOSCOW,** Urusi

MATUMIZI ya pombe nchini Urusi yamepungua kwa asilimia 43 kutoka mwaka 2003 mpaka 2016, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Matokeo haya yanakuja baada ya taifa hilo kuchukua hatua kadhaa za kuwasukuma watu kubadili mifumo yao ya maisha na kuishi kwa kuzingatia afya zao.

Awali Urusi ilifahamika kama nchi inayoongoza katika matumizi ya unywaji wa pombe duniani.

"Ni kwa muda mrefu matumizi ya pombe kwa kiwango kikubwa yamekuwa yakitajwa kuwa sababu ya vifo vingi vijana ambao ndiyo nguvu kazi wa taifa hilo la Urusi," ripoti ilisema.

Lakini kuanzia mwaka 2003 mpaka 2018, matumizi ya pombe yamepungua halikadhalika, idadi ya vifo pia imepungua, kutokana na matokeo hayo chanya kutokea ndiyo sababu ya kuhusisha sababu ya vifo na pombe.

Mwaka 2018, umri wa kuishi nchini Urusi ulivunja rekodi kihistoria na kuwa miaka 68 wanaume na wanawake 78.

Hatua za kukabiliana na matumizi ya pombe zilianzishwa na rais wa zamani Dmitry Medvedev, ambaye alipiga marufuku matangazo ya pombe, aliongeza kodi katika pombe na kupiga marufuku mauzo ya pombe kufanyika katika muda fulani

Mjini Moscow, maduka madogo (vioski) ambayo yalikuwa yanajaa pombe kali za Vodka na bia yamefungwa muda mrefu au yanauza samaki sasa. **BBC**

## Pompeo awalalamikia Democrat

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani amekishutumu Chama cha Democrats kwa unyanyasaji wa wajumbe wa Republican.

Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompeo, alisema Democrats inawanyanyasa watu wa Republican ili kuwakingia kifua dhidi ya uchunguzi unaomlenga Rais Donald Trump. Pompeo aliilaumu kamati ya bunge inayoongozwa na Democrats kwamba inajaribu kutumia nguvu yake kuwanyanyasa wafanyakazi wake.

Aliandika katika ukurasa wake wa Twitter kuwa mombi ya maofisa wake watano kufika kwenye kamati maalum ya bunge ya uchunguzi huo "hayatawezekana".

Wajumbe wa kamati maalumu ya bunge la Congress wanafuatilia shutuma dhidi ya Rais Trump kumshinikiza Rais wa Ukraine kufanya uchunguzi wa kashfa za rushwa dhidi ya Joe Biden ambaye ni mpinzani wake kisiasa. **BBC**

# Ma-RC wapewa maagizo mazito korosho

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa yote inayolima korosho nchini wahakikishe wanasimamia vizuri zao hilo na wasiruhusu kuingizwa kwa mfumo mpya wa ununuzi ambao haujaeleweka kwa wadau na wanunuzi.

"Mabadiliko ya mifumo yalitolewa na baadhi ya viongozi ambao sio waaminifu, serikali iko macho itawachukulia hatua viongozi wa vyama vya ushirika wasiokuwa waaminifu. Tunataka mfumo wenye manufaa ndio utumike." Alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Mtwara baada ya kukagua ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini inayojengwa katika eneo la Mitengo, wilayani Mtwara.

Waziri Mkuu amesema msimu wa korosho kwa mwaka huu unatarajiwa kutangazwa hivi karibuni, hivyo ni lazima kwa wakuu wa mikoa inayolima korosho wakajiandaa vizuri ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

Waziri Mkuu aliendelea kuwasisitiza wafanyabiashara kutojihusisha na ununuzi wa korosho kwa njia ya kangomba kwamba: "Kangomba imepigwa marufuku, watakaojihusisha moto utawawakia huko huko. Tunataka wakulima wenyewe ndio wanufaike."

Pia Waziri Mkuu alitoa wito kwa wakulima wa zao la korosho kuendelea kujiimarisha na wahakikishe wanajiwekea akiba kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo kwa sababu, "serikali itaendelea kusimamia zao hili ili wakulima wapate tija." Mapema, Waziri Mkuu alitembelea ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini na kukagua kazi ya ujenzi inayoendelea hospitalini hapo, ambapo amesema itakapomalizika itawapunguzia wananchi safari ya kwenda Muhimbili kufuata huduma.

Alisema serikali imejikita katika kuboresha huduma mbalimbali za wananchi zikiwamo za afya, hivyo wananchi wa Kanda ya Kusini watapata matibabu ya kibingwa karibu na maeneo yao.



Mkuu wa Mawasiliano ya Masoko na Huduma za Fedha wa Zantel, Sakyi Opoku (wa pili kushoto), akipeana mkono na Mkuu wa Huduma za Teknolojia na Uendeshaji wa Benki ya TPB, Jema Msuya, baada ya uzinduzi wa ushirikiano, mjini Zanzibar jana, ambapo watumiaji wa huduma ya EzyPesa ya Zantel wataweza kupata huduma za kibenki za benki hiyo. Wengine ni Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohamed Khamis Mussa (kushoto) na Mkurugenzi wa Masoko na Uendelezaji wa Biashara wa TPB, Deo Kwiyukwa. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## Kimbunga chapindua mtumbwi hifadhini

INATOKA UK. 3

Alisema mtalii huyo alilokolewa na kuwa nahodha anaendelea kutafutwa.

**KAULI YA TMA**

Naye Meneja wa Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa wa TMA, Samuel Mbuya, alidhibitisha kuwapo na dhoruba ya upepo katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Arusha juzi.

Alisema tukio hilo lilisababishwa na mkusanyiko wa mawingu ya radi na kutengeneza mkondo wa mawingu kuanzia Kusini mwa Kenya na kuelekea maeneo ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

"Upepo ulifika kasi ya kilometa 50 kwa saa na dhoruba hiyo ilidumu kwa kipindi cha dakika 30 katika eneo husika, hali hiyo ilifuatiwa na vipindi vya mvua na ngurumo kutokana na mawingu hayo," Mbuya aliiambia Nipashe jana.

Alisema baada ya tukio hilo, hali ya hewa ilirudi kawaida na mamlaka ilitoa taarifa ya kuwataka kuendelea na majukumu yao kama kawaida.

"TMA inatoa taarifa kwa wananchi kuendelea na majukumu yao kama kawaida, lakini wanatakiwa kufuatilia taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa," Mbuya alisema.

**Imeandikwa na Daniel Sabuni, Arusha na Mary Geofrey, Dar**

# Washtakiwa zaidi wajipeleka kwa DPP

INATOKA UK. 2

Pia inadaiwa kati ya tarehe hizo, Mansoor alijipatia Sh. milioni tatu kutoka kwa Wakati Katondo kama malipo ya kiwanja kilichoko Ukuni. Pia anadaiwa alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Ofisa wa Takukuru, Gogo Migutah kama malipo ya kiwanja kilichopo eneo hilo hilo.

Katika mashtaka ya tano, inadaiwa Mansoor alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa Ekwabi Majungu ambaye pia ni ofisa wa Takukuru kama malipo ya kiwanja hicho.

Mansoor anadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017, maeneo ya Upanga jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini, alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa John Sangwa kama malipo ya kiwanja cha eneo hilo. Inadaiwa kuwa mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Takukuru, alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Rose Shingela kwa ajili ya malipo hayo.

Katika mashtaka ya utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Januari 2013 na Mei 2018 huko maeneo ya Upanga, mshtakiwa alijipatia Sh. 1,477,243,000 wakati akijua kuwa fedha hizo ni haramu na ni zao la kosa tangulizi la kughushi.

**WAMBURA NDANI**

Wakati kesi hiyo ilipotajwa jana, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo aliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hata hivyo, baada ya wakili huyo kutoa hoja hizo, Wambura alinyoosha mkono kuomba kuzungumza na hatimaye kuruhusiwa. "Mheshimiwa Hakimu nimemwandikia barua DPP kuomba msamaha na kukiri makosa yangu. Naomba Jamhuri waharakishe nipate majibu ya barua yangu," alidai Wambura.

Wankyo alidai kuwa amesikia hoja za mshtakiwa na kwamba atafuatilia na kuzifanyia kazi.

Hakimu Mhina alisema kesi hiyo itatajwa Oktoba 16, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi kigogo huyo wa mpira wa miguu nchini, anakabiliwa na mashtaka 17, likiwamo la kughushi, shtaka moja la kutoa na kuwasilisha nyaraka za uongo, mashtaka 13 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na mashtaka mawili ya kutakatisha fedha haramu.

Katika shtaka la kwanza ambalo ni la kughushi, mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo Julai 6, 2004 sehemu isiyojulikana ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

Ilidaiwa siku na tarehe za tukio la kwanza Wambura kwa nia ya kutapeli alitengeneza barua ya kughushi ambayo haina kumbukumbu namba akionyesha imeandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Jeck System anadai kurejeshewa malipo ya mkopo wa Dola za Kimarekani 30,000 pamoja na riba aliyokuwa ameikopesha TFF.

Katika shtaka la kutoa na kuwasilisha nyaraka ya uongo, mshtakiwa alitoa barua iliyokuwa haina kumbukumbu namba ya Julai 6, 2004, akijifanya kwamba ni barua iliyoandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Jeck System Ltd, akionyesha kuwa anadai mkopo wa Dola 30,000 pamoja na riba waliokopeshwa TFF huku akijua kuwa siyo kweli.

Pia katika mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, Wambura anadaiwa kutenda kosa hilo, Juni 17, 2015 huko katika ofisi za TFF, ambapo kwa nia ya udanganyifu, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 10 kutoka TFF kwa kuonyesha kuwa ni malipo ya Dola 30,000 pamoja na riba kutoka kwenye kampuni hiyo ya Jeck jambo ambalo siyo kweli.

Katika shtaka la utakatishaji fedha, Wambura anadai, kati ya Agosti 15 na Oktoba 21, 2014, makao makuu ya shirikisho hilo, alijipatia Sh. milioni 25 kutoka TFF, huku akijua fedha hizo ni zao la kosa la kughushi.

**TIBAIJUKA AACHIA MZIGO**

MBUNGE wa Muleba Kusini (CCM), Profesa Anna Tibaijuka amesema uongozi wa Shule ya Sekondari ya Barbro Johansson Model Girls utarejesha fedha za msaada ulizopokea kutoka kwa mfanyabiashara James Rugemarila (zilizoibua sakata la Escrow) ili kumsaidia kulipa na hatimaye kusamehewa. Akihojiwa katika kituo kimoja cha runinga nchini, Prof. Tibaijuka alisema uongozi wa shule hiyo umekaa kikao na kuamua kurejesha fedha hizo walizopokea ili kumsaidia mtuhumiwa huyo anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kutoka mahabusu.

"Msamaha wa Rais unapotoka ni fursa adimu, sasa fursa ukiichezea utabaki kujuta mwenyewe na sisi tunarudisha mezani mchango tuliopokea," alisema.

Profesa Tibaijuka alisema fedha alizokuwa amewapa zilishatumika kujenga mabweni, hivyo wanazotaka kurudisha watazitafuta kutoka katika vyanzo vingine.

Naye Mbunge Bariadi, Andrew Chenge, ambaye alipokea kati ya Sh. milioni 40.2 hadi Sh. bilioni 1.6, jana aliieleza Nipashe kwa njia ya simu kuwa, yeye hahusiki na suala hilo.

"Hayo hayanihusu, msinipotezee muda wangu. Mimi nipo naendelea na maisha yangu huku Bariadi," alisema Chenge.

**Imeandikwa na HELLEN MWANGO na MARY GEOFREY**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA


**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: **0713 525954 / 0787 822000.**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI



**John John Msolla** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1328/0099 kilichotolewa na Barza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika Shule ya Sekondari Pio.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **MOS/RB/2767/19**

215442002

### KUPOTEA KWA KADI

JM SERENGETI ESSENTIALS LIMITED inatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaj yenye namba ya usajili T403 BPH aina ya TOYOTA HIACE, Chasis namba LH1251003025.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: CHA/BI/RB/189/2019

215443002

**JAHMURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi 146/2019**

**Ombi la UPENDO PETER kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu PETER JACOB LUMWE.**

**Kwa: YEYOTE ANAYETAKIWA**
**TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 14/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

215443202

IN THE RMS COURT / DISTRICT COURT OF MOSHI
AT MOSHI
MISC.CIVIL APPL NO.14 OF 2019
FRANCIS PAUL KANG'ONGOLE…APPL
VERSUS
DEMETRIUS STEPHAN MGALAMI………DEFENDANT

**NOTICE OF MENTION**

TO: DEMETRIUS STEPHAN MGALAMI
OF P.O. BOX 9133
DAR-ES-SALAAM

Take Notice that the above case has been fixed for mention in the RMS court at Moshi on 10th the day of October 2019 at 9:00am Oclock in the forenoon.

You may appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day of document under which you intend to rely in support of your case.

TAKE FURTHER NOTICE that, default of your appearance on that day before mention the court will proceed with the matter in your absence.

A copy of the petition of appeal, Judgement and decree are attached hereto.

Given under my hand and seal of this Court this 23rd day of September, 2019

15443702

IN THE RMS COURT / DISTRICT COURT OF MOSHI AT MOSHI
MISC.CIVIL APPL/CASE/MATRIMONIAL CAUSE NO.13 OF 2019
FRANCIS PAUL KANG'ONGOLE………PLAINTIFF/APPL
VERSUS
DEMETRIUS STEPHAN MGALAMI…………DEFENDANT

**NOTICE OF MENTION**

TO: DEMETRIUS STEPHAN MGALAMI
OF P.O. BOX 9133
DAR-ES-SALAAM

Take Notice that the above case has been fixed for mention in the RMS court at Moshi on 10th the day of October2019 at 9:00am Oclock in the forenoon.

You may appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day of document under which you intend to rely in support of your case.


TAKE FURTHER NOTICE that, default of your appearance on that day before mention the court will proceed with the matter in your absence.

A copy of the petition of appeal, Judgement and decree are attached hereto.

Given under my hand and seal of this Court this 23rd day of September, 2019

15443702

### KUPOTEA KWA CHETI



**Gloria Nyamahanga** anatangaza kupotea kwa cheti cha Ualimu chenye index namba EA.No 068784 kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Ifunda mwaka 2002.

Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/MSI/RB/345084/2019

215441802

### KUPOTEA KWA KADI

FRANCIS CLEMENEL Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC.108 BQZ aina ya SANLG Nyekundu.

Yeyote atakaiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya Polisi: STK/RB/TR/11821/2018.

215442502


**JAHMURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi 146/2019**

**Ombi la UPENDO PETER kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu PETER JACOB LUMWE.**

**Kwa: YEYOTE ANAYETAKIWA**
**TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 14/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.


215443202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 69..2019**
**Mdai: MATILDA PETER MUSHI**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: BLANCE THADEI SHIRIMA**

**Kwa:**
**BLANCE THADEI**
**BWAWA LA KIHONDA**
**MOROGORO**

**Ombi la Mdai: MATILDA PETER MUSHI**

**Madai ya: TARAKA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO (3) NA TSH 300,000(LAKI TATU).**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 03 mwezi 10 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 09 mwaka 2019.

115442902

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI**
**WA MIRATHI KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MWANZA**

**SHAURI LA MIRATHI NA 1/2019**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MR EMMANUEL MAKARANGA NYACHEMO**

**MWOMBAJI: MR WILLIAM MAKARANGA NYACHEMO**


**TAARIFA YA KAWAIDA**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanashauriwa kufikisha madai yao mahakamani iwapo wanaona inastahili kufanya hivyo, kabla ya kutolewa kibali kwa aliyeomba usimamizi wa mirathi hiyo.

Upingaji juu ya kutolewa kibali cha usimamizi wa mirathi itabidi iandikishwe rasmi mahakamani mnamo au kabla ya tarehe 03/10/2019.
Imetolewa leo tarehe 06/09/2019

115443602

### KUPOTEA KWA CHETI



**Maria O. Silinu** anatangaza kupotea kwa Leaving Certificate na Transcript yenye index namba S3822/0053 iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika Shule ya Sekondari Mother Theresa of Calcuta Girls.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa :
**DAR/URA/RB/341325/2019**

215442202

### KUPOTEA KWA KADI

Tanzania Rent A Car Ltd inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T403 BPH aina ya TOYOTA HIACE, Chasis namba LH1251003025.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/OST/345785/2019

215442302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA: 74/2019**

**GODIAN JOSEFU RWECHUNGURA ………………MDAI**

**DHIDI YA**

**ZIPORA IBRAHIM BYASHARA ……………… MDAIWA**

**KWA: ZIPORA IBRAHIM BYASHARA**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na: 74/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 07.10.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 05.09.2019

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

115443902

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MBEYA**
**AT MBEYA**

**COMMERCIAL CASE NO.3 OF 2019**

**NMB BANK PLC……………………………………PLAINTIFF**

**VERSUS**

**LAUDEN EDWARD MBAMBA…………………1st DEFANDANT**
**SARAH OKINGI MWITIKA……………………2nd DEFENDANT**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TO:1. LAUDEN EDWARD MBAMBA**
**2. SARAH OKING MWITIKA**

**TAKE NOTICE THAT** theplaintiff has instituted a suit against you with particulars of claims set out in the plaint filed in this court.
Service of summons to you has been ordered by meaning of publication.You are hereby summoned to appear in this court in person or by an Advocate or by an agent duly authorized on 16th day of October 2019 at 8:30 am,when this suit will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** that should you default to enter appearance in court on the day and time mentioned above,the suit will proceed and judgement may be given in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this...01....day of...10....2019.

115443802


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KOCHA WA RIVER PLATE AWAPUUZA BOCA JUNIORS




**BUENOS AIRES,** Argentina

KOCHA Marcelo Gallardo amepuuzia madai ya Boca Juniors baada ya River Plate kupata ushindi wa mabao 2-0 kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini, Copa Libertadores, juzi katika Uwanja wa El Monumental.

Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini) ni michuano sawa kama ilivyo Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo ni mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani humo.

River ambao ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo walijiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga fainali shukrani kwa mabao ya Rafael Santos Borre aliyefunga kwa njia ya penalti kabla ya Ignacio Fernandez kufunga la pili dakika ya 70.

Mwamuzi, Raphael Claus alilazimika kutumia VAR ili kuwapa penalti River iliyowapa bao la kwanza na Nicolas Capaldo alionyeshwa kadi nyekundu kwa kumchezea faulo Enzo Perez. Mshambuliaji wa Boca, Ramon Abila alilalamika maamuzi ya waamuzi wa mchezaji huo, huku kocha Gustavo Alfaro akiwashutumu wachezaji wa River kwa kujiangusha.

"Tunajua kwamba mara zote wachezaji wa River wanajirusha na wanatafuta penalti," alisema Alfaro. Lakini Gallardo amepuuzia madai hayo, akisisitiza kwamba shutuma hizo zinakuja ili kuzima ubora wa River.

"Yeyote anayetaka kuzungumza kuhusu waamuzi mwache azungumze, kwani kila kitu kipo wazi kwa kile kilichotokea," alisema.

"Tulishinda kwa sababu tulikuwa na kikosi bora na tulionyesha mchezo wa kuvutia na ndio maana tukapata matokeo mazuri na si vinginevyo."

River kama wakishinda mchezo wao wa marudiano watakutana kwenye fainali kati ya Gremio au Flamengo.

## Pochettino aikatia tamaa Tottenham

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amebainisha kwamba, Tottenham "imekata tamaa" baada ya kukumbana na kipigo cha 'mbwa koko' kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati walipopigwa mabao 7-2 na Bayern Munich juzi, Jumanne.

Na kocha huyo ameonya kwamba, Spurs watakuwa na msimu mgumu zaidi. Msimu uliopita Tottenham walikuwa washindi wa pili wa michuano hiyo baada ya kufungwa na Liverpool kwenye fainali.

Spurs, ambao walianza kufunga kwenye mchezo huo wa Kundi B kupitia kwa Son Heung-min kabla ya kujikuta wakitandikwa mabao saba kwa mara ya kwanza kwenye uwanja wao wa nyumbani katika mashindano makubwa, huku Serge Gnabry akipiga manne peke yake.

Pochettino, ambaye majaliwa yake hapo kwenye dimba la Etihad bado hayajulikani kutokana na kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Real Madrid na Manchester United, aliwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo: "Hisia katika dakika za mwisho wakati tuliporuhusu mabao matatu – ilionyesha kama vile timu imechoka na imekata tamaa kabisa.

"Ni vigumu kuzungumza kwa sasa. Sikuwaambia chochote wachezaji baada ya mchezo, tunatakiwa kukaa pamoja, lakini unaweza kuona hatuzungumzi kwa sasa," alisema Pochettino.

"Katika hali hii unatakiwa kuwa kimya na kutulia, baadaye tutazungumza, lakini kwa sasa utulivu ndio unaohitajika."






## *Sarri atoa msimamo kwa Ronaldo, Higuain, Dybala*

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri hajashawishika na wazo la kuwaanzisha pamoja kwenye safu ya ushambuliaji, Cristiano Ronaldo, Gonzalo Higuain na Paulo Dybala akihofia timu kukosa uwiano.

Juve walikuwa kwenye utawala Jumanne katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa Kundi D wakati waliwafunga Bayern Leverkusen huku Higuain na Ronaldo wakifunga pamoja na Federico Bernardeschi na kupata mabao 3-0 kwenye dimba la Allianz.

Safu ya ushambuliaji ya Juve ilianza kwa pamoja Higuain na Ronaldo kisha Dybala akaingia kuchukua nafasi ya Muargentina mwenzake dakika ya 83 na akatengeneza bao la Ronaldo.

Hata hivyo, wakati mpango wa kuwachezesha Ronaldo, Higuain na Dybala mbele kwa pamoja unaonekana kuwa wa kuvutia, Sarri haoni kama unaweza kuwa na afya.

"Kama nikikaa baa, linaonekana kama wazo zuri kwa upande wangu. Lakini kama nikiwa kwenye benchi, natakiwa kuangalia uwiano wa timu," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Kama timu baadaye itakuwa kwenye uwiano mzuri, tunaweza kujaribu, lakini kwa sasa bado haijakaa sawa."

HABARI MICHEZO

# Higuain: Nitathibitisha ubora wangu Juventus

**TURIN,** Italia

GONZALO Higuain amesema mpango wake wa sasa ndani ya Juventus msimu huu ni kutaka kuthibitisha ubora wake kwenye klabu hiyo baada ya kuwa na kipindi kigumu mara mbili cha kucheza kwa mkopo nje ya Turin.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina alionyesha kiwango cha kuvutia wakati Bianconeri hao wakiibuka na ushindi wa kuvutia wa mabao 3-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayer Leverkusen, huku yeye akifunga bao la kwanza na kutengeneza bao la pili kwa Federico Bernardeschi.

Higuain hakuwa na kipindi cha kuvutia wakati akicheza kwa mkopo kule AC Milan na Chelsea wakati wa kipindi cha msimu wa 2018-19.

Alianza kunolewa na kocha wa sasa wa Juve, Maurizio Sarri pale Napoli kabla ya kumchukua Chelsea.

"Nimekuja hapa na malengo makubwa, nataka kuthibitisha kwamba naweza kukaa kwa muda mrefu," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

Higuain alipata mapokezi ya heshima kwa mashabiki kusimama kwenye mchezo huo, ambao ulimshuhudia Cristiano Ronaldo akifunga bao la tatu.

"Kiwango kilikuwa ni cha kuvutia mno, tulicheza kwa malengo ya kupata ushindi. Nina furaha kwa bao na kiwango tulichokionyesha," aliongeza kusema.






# STERLING AMTAKA FODEN KIKOSI CHA ENGLAND

**MANCHESTER,** England

RAHEEM Sterling ametaka mchezaji mwenzake wa Manchester City, Phil Foden kuitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England baada ya wote wawili kufunga kwenye mchezo wa ushindi wa 2-0 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Dinamo Zagreb, juzi Jumanne.

Foden anatajwa kama nyota wa baadaye na aliungana na Sterling kufunga kwenye mchezo huo uliopigwa katika dimba la Etihad.

Kinda huyo amecheza dakika 10 kwenye Ligi Kuu msimu huu, lakini Sterling anahisi kwamba Foden anatakiwa kuwapo kwenye kikosi cha England maarufu kama 'Simba Watatu' kinachonolewa na kocha, Gareth Southgate.

"Namtaka Phil kwenye kikosi cha timu ya taifa, kama akiendelea hivi atakuwa pale siku moja," alisema Sterling akiiambia BT Sport.

"Tumewaona wao (Dinamo) wakicheza vizuri na ilikuwa ngumu kwetu kupenya ngome yao mara kadhaa.

"Alionyesha kiwango cha kuvutia na naamini ana nafasi kubwa kwenye timu ya taifa na kila mmoja aliyemwona anaweza kukubaliana na mimi."

Foden ana nafasi nyingine ya kuonyesha kiwango chake, kwenye mchezo ujao wa Ligi Kuu Jumapili wakati Man City watakapocheza dhidi ya Wolves.

# *Zidane akerwa na kiwango Madrid*

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amelielezea bao la kwanza la Club Brugge kama "utani" wakati Real Madrid walipoonyesha mchezo wa ovyo kipindi cha kwanza na kulazimishwa sare ya mabao 2-2, juzi Jumanne.

Madrid walikuwa nyuma kwa mabao mawili kabla ya kipindi cha pili kwenye mchezo huo wa pili wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, huku Emmanuel Bonaventure Dennis akifunga mawili.

Dennis alishindwa kuituliza pasi ya Percy Tau, lakini mpira ukajaa wavuni na kumpita golikipa Thibaut Courtois katika dakika ya tisa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 mzaliwa wa Nigeria, alifunga bao la pili katika dakika ya 39 wakati alipomfunga kirahisi Courtois, ambaye alitolewa kipindi cha pili na nafasi yake kuchukuliwa na Nacho Fernandez.

Sergio Ramos alirudisha matumaini ya Madrid kwa kufunga bao la kwanza dakika 10 baada ya kipindi cha pili na Casemiro akasawazisha dakika tano kabla ya mpira kumalizika, lakini Zidane aliachwa hajaridhika na kiwango ilichoonyesha timu yake katika kipindi cha kwanza.

"Ni matokeo mabaya, lakini tulijibu vizuri," alisema akiambia Movistar. "Hatuwezi kuwa na furaha - bao la kwanza lilikuwa ni utani.

"Lakini bado nina mtazamo chanya - wachezaji walibadilisha mchezo katika kipindi cha pili na walionekana kurudi vizuri kwenye mchezo.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GNABRY: KIPIGO SPURS NI SHANGWE ARSENAL

●●● Kufunga mabao manne ni hisia ya kushangaza, nadhani mashabiki wote wa Gunners...

**LONDON,** England

SERGE Gnabry amefunguka kuwa mabao manne aliyofunga wakati Bayern Munich ikiichapa Tottenham 7-2, ana uhakika mashabiki wa timu yake ya zamani, Arsenal watakuwa wamefurahia uchezaji wake.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Tottenham Hotspur, mashabiki walishangazwa na kipigo hicho wakati Spurs wakiwa wa kwanza kufunga bao la kuongoza kupitia kwa Son Heung-min.**

Lakini Joshua Kimmich na Robert Lewandowski waliihakikishia Bayern inakwenda mapumziko ikiwa mbele, kabla ya Gnabry kutupia mara mbili katika dakika mbili za mwanzo za kipindi cha pili.

Bao la penalti la Harry Kane, lilionekana kuiweka Spurs katika mstari, lakini Bayern iliwatibulia kwa kuibuka na ushindi, na Gnabry akiongeza mawili huku kwa upande wa Lewandowski akipiga bao lake la 14 msimu huu.

Gnabry, ambaye alitokea shule ya makinda ya Arsenal, alikumbuka mizizi yake baada ya kuongoza mauaji kwa wapinzani hao wa jadi wa 'Gunners'. Akizungumza na Sky Sport Deutschland, Gnabry alisema: "Ni vigumu kuliweka hili katika maneno, kushinda 7-2. Hakuna yeyote kati yetu alikuwa ameweza kulifikiria hilo.

"Kufunga mabao manne pia ni hisia ya kushangaza. Nadhani mashabiki wote wa Arsenal watakuwa wamelifurahia hilo!

"Ni wazi ni matokeo mazuri kwetu na tunakwenda kuifurahia jioni hii."

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani alitupia katika mtandao wa Twitter, akiwamaliza zaidi mashabiki wa Spurs kama alivyoandika: "Kaskazini mwa London ni Nyekundu!".

Kwa kipigo hicho, inamaana Tottenham imeruhusu mabao saba kwa mara ya kwanza nyumbani kwenye mashindano makubwa.

Kikosi hicho cha Mauricio Pochettino, kilifungwa na Liverpool kwenye mechi ya fainali, lakini juzi Spurs ilishindwa kufurukuta dhidi ya Bayern katika mechi hiyo ya Kundi B, hivyo hadi sasa tayari kimeruhusu mabao tisa kutinga nyavuni mwake baada ya mechi ya kwanza ugenini kukubali kipigo cha mabao mawili dhidi ya Olympiacos.

Sasa Pochettino atahitaji kujipanga vizuri ili angalau kuvuna pointi zote tatu Spurs itakapoifuata Red Star Belgrade, ambao wanashika nafasi ya pili baada ya kuichapa miamba ya Ugiriki, Olympiakos.

## ZISIKUPITE

### BARCA KURUDI KWA WILLIAN

BARCELONA inazingatia kutoa ofa nyingine kwa mshambuliaji wa Chelsea, Mbrazil Willian, 31, ambaye bado hajatia saini mkataba mpya na klabu hiyo na atakuwa huru majira ya joto. ***(Mundo Deportivo, via Express)***

### DEMBELE AGEUKIWA UNITED

MANCHESTER United inataka kumsajili mshambuliaji Moussa Dembele na kiungo wa Newcastle United, Muingereza Sean Longstaff, 21, katika dirisha la Januari. ***(Star)***

### OZIL AIPASUA KICHWA ARSENAL

ARSENAL inahofia itashindwa kumtoa Mesut Ozil, 30, katika dirisha la Januari, licha ya kujiandaa kulipa sehemu ya mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki. ***(Mail)***

### DONNARUMMA AIGOMEA MILAN

KIPA Gianluigi Donnarumma, amekataa mkataba mpya utakaomwezesha kulipwa pauni milioni 5.3 kwa mwaka kutoka kwa AC Milan. ***(Corriere dello Sport, via Sun)***

### RODRIGUEZ ATAKIWA INTER

MSHAMBULIAJI wa Burnley, Muingereza Jay Rodriguez, 30, anahusishwa na kujiunga Inter Milan dirisha la Januari. ***(Calcio Mercato - in Italian)***

### WENGER APATA OFA KIBAO

KOCHA wa zamani wa 'Gunners', Arsene Wenger, 69, amesema "amekuwa akipokea maombi" tangu aondoke kaskazini mwa London na sasa anaendelea kupima wapi pa kufanya kazi. ***(Mirror)***

### ALLEGRI AWINDA KAZI UNITED

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri amekuwa akijifunza Kingereza akiwa anawinda kazi Ligi Kuu na kuinoa Manchester United ikiwa ndiyo lengo lake kuu. ***(Guardian)***

### SANCHEZ AFURAHIA SOKA INTER

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez, amesema "amepata mapenzi katika soka kwa mara nyingine" baada ya kutolewa kwa mkopo Inter. ***(Eurosport)***

### RIO: KANE ONDOKA SPURS

BEKI wa zamani wa England, Rio Ferdinand ametoa ushauri kwa mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane, 26, kuondoka Spurs kama anataka kutwaa makombe makubwa. ***(Mail)***

### TRIPPIER AFUNGUKA ATLETICO

BEKI wa Atletico Madrid na England, Kieran Trippier, 29, amesema "hakuhitaji kufikiri mara mbili kuhusu kuondoka" Tottenham kwenda Hispania. ***(Football.London)***

### COSTA KUUZWA QATAR

ATLETICO Madrid ipo katika mazungumzo na Al Rayyan ya Qatar kuhusu kuiuzia straika Mhispania Diego Costa, 30. ***(AS Diario - in Spanish)***

### NEWCASTLE YAJADILI KIPIGO

KOCHA wa Newcastle United, Steve Bruce amehoji uwezo wa wachezaji wake na matamanio ya kuichezea klabu hiyo baada ya kupoteza 5-0 dhidi ya Leicester City Jumapili. ***(Telegraph)***

# COASTAL UNION YAIFUATA YANGA KWA TAHADHARI

Na Mwandishi Wetu

KIKOSI cha Coastal Union kutoka Tanga kinatarajiwa kuwasili jijini Dar es Salaam kesho kwa ajili ya kuifuata Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Uhuru, imeelezwa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema wanakuja Dar es Salaam kwa kazi moja ya kusaka ushindi.**

Mgunda alisema ligi ya msimu huu itakuwa ngumu zaidi, kwa sababu ya idadi ya timu zitakazoshuka daraja ni nyingi, tofauti na ilivyokuwa katika msimu uliopita.

Kocha huyo alisema wanafahamu Yanga imetoka katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini hilo haliwatii wasiwasi kwa sababu kila mchezo huwa na dakika zake 90.

"Tunakuja kutafuta ushindi, kupata pointi mapema ndiyo kutatusaidia kukaa mahali salama katika msimamo wa ligi, msimu huu mambo ni magumu zaidi ya msimu uliopita, hatutaki kukaribia mstari wa kushuka daraja," alisema Mgunda.

Coastal Union itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya ugenini ya bao 1-1 dhidi ya Ruvu Shooting ya Mlandizi, Pwani.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Coastal Union ambayo imecheza mechi tatu, ina pointi nne na iko katika nafasi ya tisa wakati wapinzani wao, Yanga ambao leo wanawakaribisha Polisi Tanzania hawana pointi hata moja, lakini wamecheza mchezo mmoja tu.



Mchezaji wa Tenisi, Isihaka Mpate, akipiga mpira kurudisha kwa mpinzani wake wakati akifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bella kunogesha riadha shuleni Atlas

**Na Faustine Feliciane**

MASHINDANO ya riadha ya kilomita 21 yaliyoandaliwa na Shule za Atlas za jijini Dar es Salaam yamepangwa kufanyika Oktoba 14, mwaka huu huku wanamuziki, Christian Bella na Beca Ibrozama, wakitarajiwa kutoa burudani.

Mashindano hayo yameandaliwa maalum kwa ajili ya kuchangisha fedha zitakazotumika kujenga maktaba ya kisasa ya umma.

Akizungumza jana jijini, Makamu Mkuu wa Shule ya Msingi Atlas Madale, Joseph Njingo, alisema kupitia harambee na ushiriki wa mbio hizo, wanatarajia kukusanya kiasi cha zaidi ya Dola za Marekani 750,000 katika kipindi cha miaka mitatu ili kukamilisha ujenzi huo.

Njingo alisema mashindano hayo ya riadha yatakayokuwa pia na mbio za kilomita 10 na tano na yataenda sambamba na mahafali ya shule hizo.

"Tunatarajia kuwa na wakimbiaji 2,000. Wapo pia kutoka nje, pamoja na shughuli nyingine pia kutakuwa na burudani mbalimbali," alisema Njingo.

Aliongeza kuwa mashindano hayo ya riadha yamepata baraka zote kutoka Shirikisho la Riadha Tanzania (RT) na watasimamia kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mbio hizo.

Alisema zawadi kwa mshindi wa kwanza wa mbio za kilomita 21 ni Sh. milioni moja, mshindi wa pili ataondoka na Sh. 760,000 wakati atakayefuatia atapewa Sh. 500,000 huku mshindi wa nne na watano wakipata Sh. 300,000 na Sh. 200,000 kila mmoja.

Naye Mkurugenzi wa shule hizo, Sylvanus Rugambwa, alisema mashindano hayo yanaendana na kaulimbiu ya shule hizo huku akiwataka wadau kutoka sehemu mbalimbali kushiriki mbio hizo na kuongeza kwamba maktaba itakayojengwa hapo itawasaidia Watanzania wote.

## *Zanzibar Heroes kuimarishwa zaidi*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya Soka ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), Hemed Morocco, anatarajia kutangaza benchi lake la ufundi kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati ifikapo keshokutwa, imeelezwa.

Mashindano ya Kombe la Chalenji yanatarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu jijini Kampala, Uganda.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa jana, Morocco, alisema anatarajia kufanya kikao na viongozi wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), akiwamo Mkurugenzi wa Ufundi wa shirikisho hilo ili kuona namna gani atateua wasaidizi wake kwa ajili ya kupata mafanikio katika mashindano hayo.

Morocco alisema matarajio yake ni kuona Zanzibar Heroes inafanya vizuri katika michuano hiyo na anahitaji kupata muda wa kuchagua benchi lake la ufundi.

"Nimeingia leo (jana), kutokea Mwanza, ningeweza pia kulitaja leo (jana), benchi la ufundi, lakini nimeona nisubiri hadi Jumamosi, tukae na Mkurugenzi wa Ufundi na viongozi wa ZFF," alisema Morocco.

Aliongeza kwa kuwataka wadau wa timu hiyo wasiwe na wasiwasi kwa sababu watajipanga kupata makocha ambao wataisaidia timu yao kufikia malengo.

Pia kocha huyo ameishukuru ZFF kwa kuendelea kuwaamini na kumpa timu hiyo kwa mara nyingine huku akiahidi itafanya kile ambacho Wazanzibar wengi wanakihitaji ikiwamo kufanya vizuri katika mashindano hayo.

## Prisons wajipanga kurejesha ushindani

**Na Mwandishi Wetu**


KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons ya jijini Mbeya, Adolph Rishard, amesema kikosi chake kimerejea kwenye ushindani na anaamini kitafanya vema katika msimu huu wa Ligi Kuu Bara unaoendelea.

Rishard aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wake wamezoeana na anaamini wataendelea kufanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata.

"Nilifurahi sana kupata ushindi dhidi ya Mtibwa Sugar pale Jamhuri, tulianza vema na tulifanikiwa kumaliza mchezo katika kipindi cha kwanza, wenzetu waliamka katika kipindi cha pili, wakatusumbua, lakini tayari bao tulilofunga mapema lilitulinda," alisema Rishard.

Aliongeza kuwa bado ligi iko mwanzoni, hivyo hakuna timu inayoweza kutamba itanyakua ubingwa na kupata nafasi ya moja kwa moja kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika hapo mwakani.

Michezo
Alhamisi Oktoba 3, 2019
Nipashe



Gnabry: Kipigo Spurs ni shangwe Arsenal UKURASA 30

USIKU MGUMU...



Winga wa Bayern Munich, Kingsley Coman, akihaha kumtoka kiungo wa Tottenham, Harry Winks (kulia) katika mechi ya Kundi B ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur juzi usiku na wenyeji hao kuchezea kichapo cha 'mbwa mwizi' cha mabao 7-2. **HABARI UK.28**

# YANGA KUISHUSHIA POLISI HASIRA ZOTE

## Zahera afunguka siri ya ushindi kwa wachezaji, Matola asema wanaweka kando kipigo walichowapa...

**Na Somoe Ng'itu**

TUMEREJEA! Ikiwa na maumivu ya kung'olewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga inatarajia kuwakaribisha "Maafande" wa Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam leo.

**Hii itakuwa ni mara ya pili kwa Yanga kucheza na Polisi Tanzania, mara ya kwanza ilikuwa kwenye mchezo wa kirafiki na wawakilishi hao pekee wa nchi waliobaki kwenye mashindano ya kimataifa walifungwa mabao 2-0.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema akili na nguvu zao sasa zinaitazama Ligi Kuu Tanzania Bara na leo wanapambana kuhakikisha wanashinda ili kurejesha furaha kwa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo.

Zahera alisema kuwa anafahamu Polisi Tanzania ni moja ya timu mpya kwenye Ligi Kuu, lakini inaundwa na wachezaji wenye uzoefu na ligi hiyo, hivyo amejiandaa kukabiliana na ushindani kutoka kwa kikosi hicho.

"Tuko tayari, tunajua ligi ina ushindani, kila timu inataka kushinda, na wachezaji wa timu nyingine wanataka kuonyesha wanaweza kutufunga, nimewaambia wachezaji wangu wawe makini na watulie wanapokuwa na mpira, utulivu husaidia kupata matokeo ya ushindi," alisema kocha huyo.

Suleiman Matola, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, aliliambia gazeti hili kuwa anatarajia mchezo huo utakuwa na ushindani, kwa sababu anakutana na timu yenye uzoefu wa ligi hiyo na mashindano mengine mbalimbali.

Matola alisema wataingia uwanjani wakisahau ushindi walioupata katika mchezo wa kirafiki, huku akiongeza kwamba kikosi cha Yanga sasa kimeimarika zaidi.

"Ni mchezo mgumu, Yanga ni timu kubwa, imetoka katika mashindano ya kimataifa na sasa inataka kuonyesha ubora wao, lakini sisi pia tumejipanga imara kuwakabili, hatukuwa na matokeo mazuri katika mchezo uliopita, hivyo tunahitaji kushinda ili kujiweka kwenye nafasi nzuri," alisema Matola.

Aliongeza kuwa watacheza kwa tahadhari zaidi katika mchezo huo na amewaandaa nyota wake kutokuwa na hofu dhidi ya vigogo hao.

Mabingwa watetezi Simba waliocheza mechi nne na wana pointi 12 kibindoni ndio wanaongoza katika msimamo wa ligi hiyo wakati Polisi Tanzania iliyocheza mechi mbili ina pointi tatu na Yanga wanaoburuza mkia wamecheza mchezo mmoja hawana pointi.

Ligi hiyo itaendelea tena Jumapili kwa Yanga kuwakaribisha Coastal Union kutoka jijini Tanga na baada ya hapo itasimama kupisha kalenda ya kimataifa ya Fifa na CAF.

## Aussems ateswa na mabao Simba

**Na Somoe Ng'itu**

ILI kuhakikisha kikosi chake kinaendelea kuwa imara kwa ajili ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaoushikilia, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema ataandaa programu maalumu itakayosaidia kulinda viwango vya wachezaji wake, lakini pia akitaka kuona wanafunga mabao mengi.

Simba ambayo inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 12, itashuka tena uwanjani Oktoba 23, mwaka huu kuvaana na Azam FC na baadaye itasafiri kuelekea Singida kuwafuata Singida United na Mwadui FC iliyoko mkoani Shinyanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema wanalazimika kupanga programu mpya za mazoezi zitakazoendana na Kalenda za Shirikisho la Soka Afrika (Caf), ambayo inatoa muda kwa timu za Taifa kucheza mechi za kirafiki na za mashindano.

Aussems alisema anaamini baada ya kupisha ratiba hiyo, kikosi chake kitaendelea kufanya vema kwenye mechi za ligi na mashindano ya Kombe la FA ambayo yataanza ifikapo Desemba mwaka huu.

"Tunahitaji kujipanga kutokana na kalenda, huwezi kufanya mazoezi magumu wakati mechi inayofuata ni zaidi ya siku 20, lakini ni muhimu kuendelea kuwa katika kiwango kizuri na tayari kupambana," alisema kocha huyo.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa anahitaji kuona wanapata ushindi katika mechi zote za mzunguko wa kwanza, huku pia nyota wake wakifunga mabao mengi katika kila mchezo.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kinaendelea na mazoezi baada ya kutoka kuwapa wachezaji mapumziko ya siku mbili waliporejea kutoka Kanda ya Ziwa.

"Tulitamani kuwa na mechi nyingine wiki hii, lakini tunaheshimu ratiba, tunajua imetolewa kwa kuipa kipaumbele michuano yote," alisema kwa kifupi meneja huyo.

Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, ndiye anayeongoza kwa kupachika mabao mengi, a

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002